

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 27 Juni, 2011

(Mkutano Ulianze Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 121

Chama Tawala Kuzuiwa Kutekeleza Sera Zake

MHE. MOHAMED H. MISSANGA aliuliza:-

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 Chama cha Mapinduzi (CCM) ambacho kilishinda, kilipewa ridhaa ya kuongoza nchi na kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi ambayo inaeleza kuwa wananchi wanayo haki ya kuchangia katika Miradi ya Maendeleo nchini:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa si haki kwa Vyama vya Upinzani kuwakataza wananchi wasichangie Miradi mbalimbali ya Maendeleo na kwamba hali hiyo inazuia Chama Tawala kutekeleza sera zake?

(b) Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inaweza kuchangia wafadhili kusitisha misaada yao kwa kukosekana ushiriki wa wananchi katika miradi hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, shughuli za Vyama vya siasa hapa nchini zinatawaliwa na Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992 na marekebisho yake mbalimbali pamoa na Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa za mwaka 2007. Hivyo, ni wajibu wa

Vyama vyote vya siasa kuzingatia sheria na Kanuni hizo katika kudumisha amani, utulivu na mshikimano uliopo kijamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2010, Chama cha Mapinduzi (CCM) kilishinda na kupata ridhaa ya wananchi kuongoza nchi kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Hivyo kinachotekelezwa kwa miaka hii mitano ni Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 ambacho ndicho Chama Tawala. Katika ilani hiyo, tuliahidi kuwashirikisha wananchi kuleta maendeleo yao na ndicho kinachofanyika hivi sasa. Kitendo cha baadhi ya Vyama vya Upinzani kuwakataza wananchi wasichangie miradi yao ya maendeleo ni kuzuia chama tawala kutekeleza sera zake na ni kinyume cha Kanuni ya 4(1) (b) ya Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa.

(b) Mheshimiwa Spika, washirika wetu wa maendeleo wanatambua na kuthamini michango ya wananchi katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Tuna programu na miradi mbalimbali ambayo Serikali ina mikataba na Mashirika ya Maendeleo ambayo tumekubaliana kwamba wananchi watachangia kama *TASAF*, *ASDP* na kadhalika. Ni imani ya Serikali kwamba wafadhili makini hawawezi kamwe kukatishwa tamaa na kauli za baadhi ya vyama vya siasa kuwachochea wananchi wasichangie miradi inayowahusu kwa ajili ya maendeleo yao wenyewe.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake fasaha, nadhani wananchi wamesikia na wanaohusika wamesikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huko sasa katika maeneo ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi kumeingia vurugu kwamba huyu anasema hivi, huyu anasema hapana, huyu changia, huyu usichangie, kiasi kwamba wananchi wamekuwa *demoralised* katika mambo yao na baadhi ya miradi imeanza kukwama.

Ni nini sasa kauli ya Serikali hapa Bungeni itakayowaongoza wananchi ili wasibabaishwe katika kujiletea maendeleo yao wenyewe na wafadhili wetu wasikatishwe tamaa? Nini kauli ya Serikali hivi sasa? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wapo baadhi ya wenzetu wa Vyama vya Upinzani wamekuwa wanakataza wananchi kuchangia michango hata yenye nia njema na hili limejitokeza sana katika jimbo jirani na Mheshimiwa Missanga, Jimbo la Singida Vijijini na hii ni kutokana na hotuba kubwa, nyingi ambazo zimefanywa na Mheshimiwa Mbunge na hasa hotuba ya tarehe 23 Januari, 2011 ambayo vielelezo vyake vyote

ninavyo. Nayo hii imesaidia sana katika kuwachochea wananchi na kuwazuia wasifanye hivyo. (*Makofit*)

Kauli yetu kama Serikali tunataka kuwaambia wananchi wakumbuke kwamba hii si sera ngeni, tangu enzi ya Mwalimu tulisema nchi hii ni ya Ujamaa na Kujitegemea. Kujitegemea ndiyo huku; yako mambo ambayo wananchi tunaweza tukafanya wenyewe, yako mambo ambayo yanaweza kufanya na Serikali, yako mambo yanaweza kufanya na Wafadhili, lakini yako mambo ambayo tunaweza kufanya wenyewe. Huku ndiyo kujitegemea. Kwa hiyo, haiwezekani leo ghafla nchi ya kwetu maskini kama hii tukaachana na sera hii. Inawezekana wenzetu baadhi yao pengine wameingia katikati hawakujua chimbuko hasa la Sera hii ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na ndiyo msingi ambao umetufikisha hapa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Jimbo la Singida Vijijini, wamekuwa wakifanya mambo mengi sana. Kwa mfano jambo ambalo limezuiwa kule *WFP* wanatoa chakula hivi sasa katika jimbo hilo kwa ajili ya kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi, wanatoa chakula cha mchana kwa wanafunzi.

Katika mkataba ambao wanavijiji wamesaini na Halmashauri na wale wafadhili ni kwamba wale wanakijiji wao wasaidie kujenga jiko tu na kushusha kile chakula kwenye gari, hizo ndizo kazi wanazofanya. Sasa ili ujenge jiko maana majiko wanayotumia ni makubwa kidogo, yanatumia mkaa maalum, hilo lazima uhitaji mchango kidogo. Sasa wenzetu wanasema hapana, msijenge jiko. Kwa hiyo, chakula kile hakiwezekani kuliwa tena wala kupikwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna sekondari ya Mkinya imekwama kujenga Maabara. Vifaa vyote vipo lakini wananchi lazima watoe vifaa vichache vile vinavyohitajika kwa upande wao kwa sababu kuna mikataba na makubaliano.

Kwa hiyo, kwa ufupi Mheshimiwa Missanga, Serikali inasema, michango kwa ajili ya maendeleo ni ruksa kwa ajili ya miradi ya wananchi. Michango hii iliishatolewa maelekezo kwa utaratibu, iko michango ambayo inatungiwa sheria, *by laws* zetu, itachangwa na risiti na wananchi wanayo ruksa ya kuihoji ile michango na matumizi yake katika maeneo yao.

Hatutarajii kwamba kuna kiongozi mwendawazimu atachangisha michango ya lazima isiyokuwa na utaratibu. Wananchi wachangishwe michango, watumie fedha zao kwa matumizi yale ambayo wamekubaliana, wahoji matumizi yake. Lakini ni mwiko kabisa kwa viongozi wa siasa kurukia na kuingia kuzuia mambo ambayo hawayajui. Tunataka tuwaachie wananchi tufanye maendeleo ili nchi yetu iweze kusonga mbele. (*Makofit*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*), ameonesha kwamba 25% ya fedha ambazo zinapitishwa na Bajeti zinatumika vibaya kwa Serikali Kuu, na 10% kwa Serikali za Mitaa zinatumika

vibaya. Lakini pia ameonesha kwamba michango ambayo wananchi wanaichanga haioneshwi katika taarifa za fedha ambazo wananchi wanapewa.

Serikali haioni kwamba haina haki ya kuchangisha watu wakati fedha za kodi za wananchi ambazo zinatozwa hazitumiki jinsi inavyotakiwa na wananchi hawapewi taarifa za fedha hizo? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo mawili tofauti. Ziko fedha za Serikali zinazotolewa kwa ajili ya shughuli maalum za maendeleo. Ni kweli *CAG* amesema hazitumiki vizuri, hatua kwa wale waliosababisha kutotumika vizuri lazima zichukuliwe kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninachosema hapa ni michango, michango nayo lazima itolewe kwa sababu uko utaratibu wa nchi hii kuchangia miradi ya maendeleo. Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, ni Mjumbe wa Halmashauri ya Kigoma, anajua upo utaratibu. Juzi hapa tumerekebisha hata sheria ya *Finance Bill* kwamba kodi zile sasa zitungiwe sheria kule kule chini waamue duka hili shilingi ngapi na nini, sheria kama hizo zipo.

Kwa hiyo, michango kama hii ambayo imeelekezwa kwenye sheria lazima ikusanywe. Lakini pia uko wajibu wa kawaida wa wawakusanyaji wa kodi kutoa taarifa kwa mamlaka au kwa wananchi kuhusiana na fedha na matumizi yake. Sasa udhaifu wa kutowajibika usiunganishwe na wajibu. Uko udhaifu wa baadhi ya watendaji wa kutokutoa taarifa, lakini huo hauwezi kufuta wajibu wa watu kuchangia michango ya maendeleo. (*Makofi*)

SPIKA: Wakati huo huo mwezi huu niliwatuma Istanbul, Mheshimiwa Esther N. Matiko na Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile, kushiriki katika Mkutano wa *IPU* kuhusu mambo ya nchi zinazoendelea. Kwa hiyo, ikaonekana nchi zinazoendelea toka mwaka 2001 wakati wa *Brussels Conference* zilikuwa 23, kwa sasa zimekuwa 43 sasa *argument* yao wanasema hii mipango kwa kiwango kikubwa Wabunge hawakushirikishwa, lakini wanasema Wabunge ndiyo wawakilishi wa wananchi hivyo inabidi wawasadie wananchi kwa kushirikiana nao katika kujiletea Maendeleo ya Serikali zao.

Pia wanasema Wabunge lazima wasimamie Matumizi ya fedha zile zinazolengwa kwa wananchi. Kwa hiyo, hili suala linakuwa *relevant*. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nimeona tu nisimame na mimi niseme kidogo juu ya jambo hili. Shughuli za wananchi vijijini zina sura mbili; yako maeneo ambako wanachangia kwa maana ya kutoa fedha ambazo ndiyo tunaita michango, lakini

yako maeneo ambayo tunaomba nguvukazi yao iwe ndiyo sehemu ya mchango wao katika kujiletea maendeleo, yote ni matokeo ya kazi.

Tunachosema ni nini? Suala la Mtanzania kufanya kazi, kushiriki katika mambo ambayo ni ya kumsaidia yeye mwenyewe kujiletea maendeleo yake ni lazima wote tulisemee kwa nguvu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili nataka niwakumbushe tu kwamba Katiba yetu sasa hivi ndivyo inavyosema, Ibara ya 25 ‘Wajibu wa Jamii’ kazi pekee ndiyo huzaa utajiri wa mali katika jamii, ndiyo chimbuko la ustawi wa wananchi na kipimo cha utu na kila mtu anao wajibu:-

- (i) Kushiriki kwa kujituma na kwa uaminifu katika kazi halali na ya uzalishaji mali.
- (ii) Kutimiza nidhamu ya kazi na kujitahidi kufikia malengo ya uzalishaji mali ya binafsi na yale malengo ya pamoja yanayotakiwa au yaliyowekwa na sheria.

Kazi hizi akizifanya haziwezi kutafsiriwa kwamba ni shuruti, ni kazi halali na lazima zifanyike. Kwa hiyo, nataka niwasih sana Vyama vyote tusaidie wananchi wajue kwamba kuchanga nguvu zao au kuchanga kutokana na raslimali walijonayo ni wajibu wa kila Mtanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimweleze Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwamba hatuwezi kuacha kupeleka fedha kwenye maeneo eti tu kuna mapungufu katika usimamizi. Tukifanya hivyo tutaumiza watu wengi ambao wako *innocent* na mahitaji yale.

Tukabane koo sisi kwa wale wote ambao hawatekelezi wajibu wao wa kusimamia fedha vizuri, lakini siwezi kuacha mimi leo kupeleka fedha kwenye Jimbo lako kwa sababu halmashauri yako Mtumishi mmoja alizembea na akasababisha suala hilo kuibua mjadala mbele ya CAG, hata kidogo! tutakuwa hatuwatendei haki. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nadhani tulione kwa mtazamo chanya lakini tuendelee kuzungumza pale ambapo usimamizi pengine hauko makini. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa ufanuzi wa ziada.

Na. 122

Kupunguza Matumizi Makubwa ya Serikali

MHE. LETICIA M. NYERERE aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupunguza matumizi makubwa ambayo hayana uwiano na hali halisi ya umaskini wa nchi yetu kwa kuendelea kutunga Sheria za kuunda Mamlaka, Taasisi na Wakala mbalimbali?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka, Taasisi na Wakala mbali mbali za Serikali huundwa kwa madhumuni ya kuboresha utendaji, kuongeza tija, ufanisi na hivyo kuwezesha huduma mbalimbali muhimu za kijamii kupatikana kwa urahisi na kwa manufaa ya Wananchi.

Baadhi ya vyombo hivyo huundwa baada ya Sheria inayovianzisha kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Bunge lako Tukufu hupitisha Sheria hizo baada ya kujiridhisha kwamba ni kweli kuna umuhimu na tija kuanzisha vyombo hivyo na kwamba uanzishajji huo umezingatia hali halisi ya mahitaji kiuchumi na kijamii pamoja na wakati uliopo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna mamlaka, taasisi na wakala wowote wa Serikali uliyoundwa bila utafiti wa kina na bila kuzingatia hali halisi ya mahitaji ya wakati husika.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake na sasa naomba nimwulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo.

(a)Je, Serikali inajiandaaje kuwa na Sera ya kupunguza mtandao wa taasisi ambazo zinaweza kuunganishwa kwa pamoja kwa mfano, *Tanzania Investment Bank* na *Housing Finance Project*?

(b)Je, Serikali ina mikakati gani ya kupunguza matumizi Serikalini ili pesa zielekezwe katika maendeleo ya vijiji, vikiwemo vijiji vya jimbo ninalotoka la Kwimba na mkoa wa Mwanza na Tanzania kwa ujumla?

SPIKA: Ahsante kwa kuuliza vizuri maswali mafupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, na mimi nampongeza sana Mheshimiwa Leticia Nyerere, kwa kuuliza vizuri maswali yanayoleweka na bila jaziba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kwa dhati kama ambavyo tumesema na tumejipanga katika kipindi cha miaka mitano ijayo kufanya lolote liwezekanalo ili kuhakikisha tunapunguza gharama za uendeshaji wa Serikali.

Hili jambo bahati nzuri na Wabunge wote mmeliunga mkono katika mpango wa miaka mitano, limeandikwa vizuri sasa Serikali inachukua hatua ya kuhakikisha hilo analolisema Mheshimiwa Leticia Nyerere linatekelezwa. Yako maeneo mengi ya kuangalia, lengo letu ni hilo hilo alilosema Mheshimiwa Mbunge kwamba chochote tutakachokiokoa katika mpango wetu wa miaka mitano (5) wa kupunguza gharama za uendeshaji katika maeneo mbalimbali kiende kikasaidie shughuli mbalimbali za ujenzi wa taifa na huduma za maendeleo katika vijiji vyetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Leticia Nyerere nakubali wazo lako na kama Wabunge wengine wana mawazo ya ziada baada ya kupitisha ule mpango tutaendelea kuyapokea ili lengo letu liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili Mheshimiwa Mbunge ametoa maoni ya kuunganisha hivi vyombo viwili. Kwa kuwa kwa mtazamo wako ni kwamba kuunganishwa kwa vyombo hivi viwili kunaweza kukasaidia mkakati wa Serikali wa kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali.

Fikra za mpango mkubwa wa kupunguza gharama, siyo haya mambo madogo madogo yanayosemwa semwa hapa ndani, maana kuna watu wanazungumza vitu vidogo vidogo, sisi Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) tunazungumza jambo kubwa zaidi na pana la kupunguza gharama za uendeshaji.

Kwa hiyo, mawazo yako tutayachukua, yataboreshwa na yatashirikishwa katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano. (*Makofi*)

Na. 123

Barabara Kupitia Hifadhi ya Shaghayu

MHE. MSTAAFU BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI aliuliza:-

Mwaka 2005 Mheshimiwa Rais aliahidi kupatikana kwa kibali cha kupitisha barabara katika msitu wa hifadhi ya Shaghayu ili kuunganisha Kata ya Mbaramo na Kata ya Mlalo:-

Je, ni lini kibali hicho kitapatikana ili kuwaondolea wananchi adha ya usumbufu wa usafiri unaowakibili wananchi wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mstaafu Brigadia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo linalopendekezwa kujenga barabara ya kupitia hifadhi ya Shaghayu ni hifadhi ya msitu wa Taifa wa Shaghayu ambao upo katika maeneo ya Kata ya Mlalo na Mbaramo. Msitu huo ni chanzo kikuu cha mito mitatu (3) ya maji ambayo ni Mto Tewe, Kingwi ambao ndio mto mkubwa wa maji yake hutumika katika Kiwanda cha Korona ya Mkonge na Mto wa tatu ni Baghai ambao husaidia kilimo cha umwagiliaji bonde la Mng'aro na Lunguza katika Tarafa ya Umba.

Aidha, msitu huu wa Shaghayu ni chanzo kikubwa cha mto Umba ambao tayari kuna ushirikiano wa kimataifa ujulikanao kama “Lake Jipe – Chala – Umba River Ecosystem” ambao ni kati ya Tanzania na Kenya.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza ahadi hiyo kwa vitendo, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilituma maombi ya kibali Wizara la Maliasili na Utalii kwa ajili ya kujenga barabara kupitia msitu wa Shaghayu kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais.

Wizara ilishauri mambo mawili ambayo ni kufanyika tathmini ya athari za kimazingira (*Environmental Impact Assessment*) na kutafuta mbadala wa kujenga barabara kwa lengo la kuwashudumia wananchi wa maeneo hayo. Katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 zilitengwa shilingi milioni 95 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara mbadala iliyopendekezwa wakati taratibu za kufanyika kwa tathmini ya athari za kimazingira katika barabara itakayopita katikati ya msitu zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, njia mbadala iliyopendekezwa na Halmashauri ya kupitisha barabara ni kutoka Mlalo – Kijiji cha Bungo kupitia Kijiji cha Bagai, Tewe, Wangwi na kuingia Kata ya Mbaramo. Ujenzi wa barabara hii utasaidia kutoa huduma kwa wananchi wa vijiji vingi zaidi kuliko kukatisha ndani ya hifadhi ya msitu wa Shaghayu. Katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuendelea kuifanyia matengenezo barabara hiyo ili iweze kupitika wakati wote.

MHE. BRG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini barabara mbadala ambayo itajengwa sio badala ya *Environmental Impact Assessment* ambayo Rais alikuwa ameagiza. Tokea Rais atoe maagizo hayo mpaka mwaka 2008 sasa hivi hii ni Bajeti ya tatu tunapitisha na shilingi zinazohitajika ni shilingi 60,000,000/=.

Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba pamoja na kujenga barabara hii mbadala bado barabara ile ambayo ni ya kukatisha kwenye msitu wa Shaghayi itajengwa au itafanyiwa hiyo *Environment Impact Assessment*?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) : Mheshimiwa Spika, ninachosema hapa na tunachosema sisi kama Serikali ni kwamba barabara ambayo imezungumzwa ni barabara

ambayo inaonekana kama inapitia katika hifadhi ya Taifa. Hapa nimekuja na *correspondence* zote na barua zote ambazo zinahusika na barabara hii. Ninajua kabisa kwamba Mheshimiwa Mbunge atakuwa anajua zaidi kuliko mimi kwa sababu hivi karibuni sijaenda Lushoto. Barabara hii ili iweze kutengenezwa na iweze kufanyiwa marekebisho yote yanayozungumzwa lazima tupate taarifa inayotoka katika maliasili na utalii kwa maana Wizara na *NEMC* ndicho tunachokisema hapa. Tukishapata hiyo, hii ni kawaida kabisa barabara nyingine zote hapa Tanzania unapojenga barabara ile lazima uhakikishe kwanza umepata hiyo *Assessment* ili uweze kupitisha barabara pale.

Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba hii ni kwa miaka mitatu iliyopita kwamba ni shilingi 60,000,000/=. *Issue* hapa inayozungumzwa sio kiasi cha pesa, *issue* inayozungumzwa hapa ni kwamba wadau wote tukisharidhiana maana yake ni kwamba kazi hii itafanyika. Hapa sisi hatuna msuli wala hatuna uwezo wa kuzuia maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais akishatoa maelekezo sisi kazi yetu ni kutekeleza, lakini tunachofanya ni kuangalia haya ambayo tunayoyazungumza hapo. Naomba Mheshimiwa Ngwilizi tushirikiane naye tuzungumze vizuri kwa karibu tuweze kujua hasa hasa anachosema ni nini ili tukatekeleza haya maagizo ya Mheshimiwa Rais.

Na. 124

Upungufu wa Watumishi Na Vifaa Vituo vya Afya na Zahanati Nchini

MHE. DUSTAN D. MKAPA (K.n.y. MHE. JUMA A. NJWAYO) aliuliza:-

Dhana ya kujenga Vituo vya afya na Zahanati lengo lake ni kurahisisha kufikisha huduma za afya karibu na wananchi, lakini tatizo la ukosefu kwa Matabibu na Wauguzi na vifaa vya kutendea kazi kwa baadhi ya vituo vya zahanati hizo kama ilivyo kwa zahanati za Dinembo, Lukokoda, Nanhyanga, Ngunja, Namindondi, Likolombe, na Chaume Wilayani Tandahimba unaoathiri sana dhana hii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inapeleka watumishi na vitendea kazi kwenye zahanati hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ina Hospitali 1 ya Wilaya, Vituo vya Afya viwili (2) na Zahanati 29. Aidha ina jumla ya watumishi 230 wa kada mbalimbali za afya. Kati ya hao watumishi wa Hospitali ya Wilaya ni 127 na 113 wanahudumia vituo vya afya na zahanati. Aidha, zahanati zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge zinahitaji kuwa na watumishi 70 wa afya. Watumishi waliopo ni 26 na upungufu ni watumishi 44.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na upungufu huo wa watumishi, Halmashauri katika mwaka 2011/2012 imeidhinisha kibali cha kuajiri watumishi 48 wa kada

mbalimbali za afya. Mchanganuo wa watumishi walioombewa kibali hicho ni kama ifuatavyo:-

Na.	Kada	Idadi
1. <i>Nurse II</i>		10
2. <i>Medical Attendant</i>		10
3. <i>Assistant Nursing Office II</i>		13
4. <i>Technologist II</i>	2	
5. <i>Records Management Assistant II</i>		2
6. <i>Assistant Technologist (Pharmacy)</i>		1
7. <i>Clinical Assistant</i>		10
JUMLA		48

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya kutolea huduma za afya, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 imetenga shilingi milioni 26,680,000/= kwa ajili ya kununua vifaa mbalimbali vya kutolea huduma za afya ili kupunguza upungufu wa vifaa uliopo. Mpango huu utatekelezwa katika zahanati za Dinembo, Lukokoda, Mahnyanga, Ngunja, Namindondi, Likolombe na Chaume.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Serikali kwa kutumia mtindo huu wa kuomba vibali kutoka Serikalini haioni kwamba inaondoa dhana nzima ya kupeleka madaraka mikoani (*D by D*)?

Pili, matatizo haya yaliyopo Tandahimba yanawakumba vile vile wananchi wa Wilaya Nanyumbu na tatizo la vitendea kazi na watumishi kama ilivyo katika Tandahimba. Vile vile tuna matatizo ya magari ya wagonjwa hasa katika vituo vya afya vya Michiga na Nanyumbu.

Je, Serikali itatusaidiaje kuondoa kero hizo katika Wilaya yetu ya Nanyumbu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, “*D by D*” ni (*Decentralisation by Devolution*) maana yake ni kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi na wakati huo huo kupeleka rasilimali watu na vifaa vingine kwa wananchi.

Maelekezo ya Serikali ni kwamba kwa kufanya hivyo tunakuwa na Tume Ajira ambayo iko kule kule, lakini wakati huo huo kuna Tume Ajira ambayo iko Utumishi pale. Anachozungumza pale Mheshimiwa Mkapa nakielewa utaratibu tuliokuwa tunatumia kule nyuma ni kwamba kwa kuititia ile Kamati ya Ajira mambo yote yalikuwa yanafanyika pale, lakini masuala kama ya Daktari na kama unapopata watumishi hawa unajua kwamba huyu ni mtumishi *sensitive* Halmashauri zenyewe zilikuwa haziwezi kupata watu wa namna hiyo hakuna *mechanism* hatuna utaratibu wa kusaidia, ndiyo maana tuko katika Kamisheni ile ile katika Utumishi.

Lakini kama ni mlinzi, mpishi unazungumzia watu wanaofagia pale kwenye Halmashauri ndicho anachokisema Mheshimiwa Mkapa kwamba je hili nalo linahitaji hilo. Tulipokutana kwenye *Association of Local Authorities of Tanzania* tulisema habari hii na tukasema kwamba Halmashauri zinazotakiwa kufanya ni kuomba kibali na ndiyo maana hapa tunazungumzia. Kibali hapa ni muhimu kwa sababu ukisema tu Nanyumbu ajiri, Siha ajiri kila mtu anaajiri utakuja hapa sasa itakuwa *problem* ya Bajeti.

Kwa hiyo tukasema tufanye hivyo na ndicho kinachofanyika sasa hivi. Kusema Halmashauri zinaweza kupata na sisi tunachozungumza ni suala la kupata kibali kwa maana ya Bajeti. Wakati huo huo tumeshakubaliana kwamba wale ambao wamekubaliwa wala hatuna haja ya kwenda kwenye Halmashauri ni moja kwa moja watu kutoka Wizara ya Afya waende *direct* kwenda huko.

Swali la pili, nataka nikiri hapa sikulisikia vizuri, lakini nilichosikia nimesikia magari, vifaa na vitu vingine ambavyo vinavyozunguzwa hapa. Vifaa hivi vimekuwa vinatolewa na tumekuwa tunapeleka hapa *ambulance*, tumekwenda kupeleka magari kutegemeana na hali halisi ya Bajeti yetu. Nataka niseme tu tunarekodi hii tunairejesta hapa pale inapotokea kwa kweli tunaona kwamba namna ya kusaidia na Nanyumbu ni Halmashauri ya Wilaya ndogo ambayo imeanza juzi juzi tu.

Kwa hiyo akileta maombi kama haya ni muafaka kabisa na nimefika katika Wilaya ya Nanyumbu najua matatizo waliyonayo. Ilizaliwa siku moja na siku ilipozaliwa Wilaya ya Siha. Kwa hiyo nina nasaba nayo nafahamu tuwasiliane tuone jinsi ambavyo tunaweza tukasaidia katika hilo. (*Makofi*)

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la Tandahimba limeenea mpaka mkoa wa Lindi Wilaya ya Ruanga. Wilaya ya Ruangwa wamejitolea kujenga *theatre room*, *X-Ray room*, wodi ya watoto, *waiting maternity room*, lakini mpaka sasa hatuna *X-ray*, hatuna *ultra sound*, operesheni *set*, vitanda havitoshi na dawa hazitoshi na wafanyakazi hawatoshi. Mheshimiwa Mbunge Kassim Majaliwa amejitahidi kuzungumzia suala hili, lakini naona bado hatujasaidiwa, naomba sana angalau kitu kimoja tuweze kusaidiwa. Ahsante sana.

SPIKA: Haya hata sio swalii ni ombi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, haya matatizo anayoyasema Mheshimiwa Mikidadi ni kweli. Labda niweke vizuri Mbunge huyu anayezungumza hapa wa Viti Maalum ana mambo makubwa sana amefanya katika nchi hii sijui kama Taifa hili linafahamu kwamba amefanya nini.

Huyu amenunua pikipiki zile za bhajaji za kubebia wagonjwa, wale mavu amekuwa anasaidia. Kwa hiyo, ninaelewa kwamba Mheshimiwa Mikidadi

anapozungumza tatizo hili maana yake nini? Amenunua kwa hela zake na kwa nguvu zake yeye mwenyewe kama Mbunge.

Mimi napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Serikali kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Mikidadi kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na anapouliza swali hili naweza nikaelewa kabisa kwamba ana maana gani anachokifanya hapa. Yeye pamoja na Mheshimiwa Majaliwa, Mheshimiwa Majaliwa tuko naye pale ni Naibu Waziri mwenzangu, hili jambo wanalizungumza pamoja na kwamba ni Waziri pale lakini huwezi kusema kwamba kwa vile huyu Waziri sasa twende tupeleke.

Nasema tumelipokea jambo hili tunakwenda kuliangalia vizuri sambamba na wale wengine wote ambao wana matatizo haya yaliyozungumzwa ya *X-ray*, *ultra sound* na vitu vingine ili tumeweza kuona jinsi ambavyo tunaweza tukasaidia katika Halmashauri hii iliyozungumzwa.

Na. 125

Wakulima Kusumbuliwa Wanaposafirisha Mazao Yao

MHE. SELEMANI S. BUNGARA aliuliza:-

Zao la ufuta ni moja kati ya mazao muhimu sana Mkoani Lindi hususan katika Wilaya ya Kilwa na kwamba katika msimu uliopita wakulima walipata usumbufu wa kukamatwa wakati wakisafirisha ufuta wao kuuza katika masoko yenze bei nzuri:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wakulima kuhusu viongozi wenye tabia ya kusumbua wakulima wanaposafirisha mazao yao wakati wa msimu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA aijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemmani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia uzoefu na manufaa yaliyopatikana kwa wakulima wa Mtwara na Lindi misimu 2007/2008 hadi 2009/2010 kwa zao la korosho, Serikali ya Mkoa iliamua kuendelea kutumia utaratibu wa stakabadhi ghalani katika msimu wa 2010/2011 kwa mazao ya ufuta na korosho. Mfumo huu unamhakikishia mkulima kupata bei nzuri kutokana na ushindani unaojitokeza kwa wanunuvi wanaonunua mazao hayo kwa mnada na kwa vipimo sahihi.

Kwa mfano, katika msimu wa 2010/2011 Mkoa wa Lindi ulipanga bei dira ya ufuta kuwa shilingi 1,000/= kwa kilo moja, bei hii pia ilitumika kama bei ya awali ambapo baadaye wakulima walilipwa malipo ya pili ya nyongeza ya kati ya shilingi 200/= hadi 300/= ikilinganishwa na bei ya wanunuvi binafsi waliotaa bei moja ya wastani wa shilingi 1,200/= kwa kilo.

Hata hivyo, bei hizo za wanunuzi binafsi hazitoi thamani halisi ya mazao kwani wanawapunja wakulima kwa kutumia mizani ambazo hazina viwango.

Mheshimiwa Spika, kutowana na manufaa yaliyopatikana katika utekelezaji wa utaratibu wa stakabadhi za mazao ghalani katika mazao ya korosho na ufuta Serikali ina mpango wa kueneza mfumo huu katika mazao mengine katika kuboresha zaidi mfumo wa soko la mazao ya mkulima.

Aidha, Serikali inatarajia kuanzisha utaratibu wa “*Commodity Exchange*” ambao utawezesha uwepo wa uwazi zaidi kati ya mwuzaji na mnunuzi kwa manufaa ya wote.

Mheshimiwa Spika, utaratibu nilioeleza hapo juu wa stakabadhi ghalani ndiyo njia bora zaidi kwa wakulima kupata soko zuri, la uhakika na bila kuwapunja wakulima hawa.

Aidha, uwepo wa mfumo huo hauzuii wafanyabiashara binafsi wanaofuata sheria na kununua mazao kutoka kwa wakulima kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa wakulima wa ufuta wa Wilaya ya Kilwa hawapo tayari kuuza ufuta kwa bei ya shilingi 1,000/= kwa kilo kama ilivyoamuliwa na Mkuu wa Mkao wa Lindi. Na kwa kuwa vyombo vyaya dola vinatumika kwa kuwazuia wakulima hao wasiuze ufuta katika masoko mengine.

Je, Serikali itawaeleza nini wakulima hao ili wapate fursa za kuuza ufuta huo kwa wakati na kwa bei iliyokuwa nzuri zaidi?

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri umesema kwamba ufuta mwaka jana nyongeza zao waliongezewa shilingi 200/= mpaka shilingi 300/=, wakati mimi natoka Wilaya ya Kilwa kuna watu mpaka sasa hivi hawajalipwa na bei ya nyongeza haikuzidi Shilingi 120/=.

Je, unawaambia nini wakulima wa Kilwa waongezewe hela yao na wasiolipwa walipwe? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, wakulima wa Mkao wa Mtwara na Lindi kwa muda mrefu sana wamepunjwa katika kuuza mazao yao. Serikali ilipoanzisha mtindo wa stakabadhi ghalani bei ya korosho imepanda kwa mfano mwaka huu dira ya bei ilikuwa shilingi 800/=, lakini baada ya malipo ya tatu wameuza kilo moja ya korosho kwa shilingi 1,600/=.

Sasa Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Lindi baada ya kuona manufaa yaliyopatikana katika mtindo wa stakabadhi ghalani katika zao la korosho. Katika kikao *duel constituted* Kikaazimia kwamba sasa utaratibu wa mfumo wa stakabadhi ghalani sio tu uwe katika korosho sasa uhamie katika zao la ufuta. Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa ambacho Mheshimiwa Bungara naye ni Mjumbe.

Kutokana na hilo sasa wako watu binafsi kule wanunuwa ufuta kilo shilingi 1,200/=. Juzi baada ya kuanza mtindo wa stakabadhi ghalani wale waliouza kwenye mnada kilo ya ufuta imeuzwa shilingi 1,750/=. Wale walangazi wanunuwa kati ya shilingi 1,100/=. Kwa hiyo nataka niseme si kweli kwamba Serikali ya Mkoa wa Lindi inawaghasi wale wafanyabiashara binafsi. Wafanyabiashara binafsi wanakaribishwa waende wakashindane kwenye mnada na wenzao.

Sasa kauli hii ya Serikali itafanya nini kuhusu wale wanaoendelea, Serikali itaendelea kuwakamata wafanyabiashara binafsi wanaonunuwa ufuta nje ya utaratibu uliowekwa na Serikali ya Mkoa.

MBUNGE FULANI: Taarifa Mheshimiwa?

SPIKA: Wakati wa maswali hakuna taarifa tunaendelea.

Na. 126

Mradi wa Umeme Vijijini

MHE. KABWE Z. ZITTO aliuliza:-

- (a) Ni lini *TANESCO* itafikisha umeme vijiji vya Bitale, Mkongoro na Kalinzi kutokea Mahembe ambapo tayari mradi umeanza?
- (b) Mradi wa Umeme Vijijini (*Rural Electrification*) katika Jimbo la Kigoma Kaskazini utagharimu kiasi gani cha fedha na Serikali ina mpango gani wa kupata fedha za kugharamia mradi kama huo?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Kijiji cha Mahembe ulikamilika mwezi oktoba, 2010. Baada ya mradi wa Mto Malagarasi kuahirishwa kwa sababu za kimazingira, Viji vya Bitale, Mkongoro na Kalinzi vitapatiwa umeme kutoka Mjini Kigoma. Chini ya mpango uliopo sasa, viji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vya Bitale, Mkongoro na Kalinzi vitapatiwa umeme kutokea Mwandiga badala ya Mahembe kama ilivyokuwa imepangwa awali.

Sababu za kutounganisha vijiji hivyo kutokea Mahembe ni kuwa baadhi ya vijiji kama Kiganza na Nyakibera vingerukwa, gharama akubwa za ujenzi wa njia ya umeme kutokana na jiografia ya njia hiyo kuwa ya milima na ugumu wa kuifanyia matengenezo njia hiyo ya umeme ikitokea hitilafu yoyote kwenye njia hiyo.

Njia ya Mwandiga inafuata barabara, hivyo ni rahisi katika ujenzi wake na vijiji vingi zaidi vitapitiwa. Punde fedha zitakapopatikana kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) mradi huu utakamilika ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili.

(b) Mradi wa umeme katika jimbo la Kigoma Kaskazini utagharimu shilingi bilioni 5.46. Fedha hizi ni kwa ajili ya kupeleka umeme kutoka Mwandiga hadi vijiji vya Kiganza, Bitale, Mkongoro, Kalinzi, Matyazo, Mkabango, Nyarubanda, Nyakimwe, Mnana na Manyovu. Maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo yaliwasilishwa *REA* mwezi Mei, 2011. Utekelezaji wa mradi huu utaanza mara baada ya kupata fedha kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*).

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri. La pili, kwa kuwa tumeamua katika juhudzi za kumaliza uchakachua ji wa mafuta. Kupandisha kodi ya mafuta ya taa mpaka shilingi 400/- na tunafahamu kwamba watumiaji wa mafuta ya taa ni wananchi maskini wa vijiji. Serikali haionti kwamba ni vema pesa hizo zinazotokana na kodi za mafuta ya taa zipelekwe *REA* ili *REA* iwe na fedha nyingi zaidi na kuweza kutekeleza miradi siyo tu ya Kigoma Kaskazini kama jinsi itakavyotekelawa bali ya nchi nzima? (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kumshukuru Mheshimiwa Zitto kwa kuridhika na jibu ambalo tumempatia katika suala lake. Lakini la pili ombi la Mheshimiwa Zitto na naamini ni ombi la Waheshimiwa Wabunge wengi, niseme kwa niaba ya Serikali tunalipokea na maamuzi yake yatazingatia utaratibu wa kawaida, Serikali nzima iko hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesikia, Waziri wa Fedha yupo na wadau wote ambao wanashiriki katika maamuzi kuhusu jambo hili. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Kafulila, swali lingine la nyongeza, lakini usiharibu hali ya hewa. (*Kicheko*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa miradi ambayo ameizungumza Mheshimiwa Waziri ya kule Kalinzi kwamba itapata umeme kutokea mjini baada ya mradi wa Malagarasi kushindikana kwa sababu ambazo siwezi kuzungumza leo. Lakini kwa kuwa Kata ya Simbo, kwa maana ya vijiji vya Simbo, Machazo, Kandaga Mlela, kijiografia viko karibu zaidi kutokea mjini kuliko kule Kalinzi. Mheshimiwa Waziri anavizungumziaje vijiji hivi katika dhana nzima ya kutumia umeme wa ziada kuweza kufikia vijiji hivyo.

SPIKA: Ahsante sana swali zuri, Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Zitto, swali la Mheshimiwa David Kafulila ni kama ombi na mimi narudia kusema ambayo tumekuwa tukisema hapa kwamba dhamira ya Serikali ni kuvifikishia vijiji vingi zaidi umeme. Naamini kuptitia utaratibu wa Wakala wa Nishati Vijiji, ombi lake Mheshimiwa Kafulila kama yalivyomaombi ya Waheshimiwa Wengi tutayazingatia na hasa kwa kuzingatia kwamba sasa Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano ya Taifa letu, tumejielekeza zaidi katika kuimarisha sekta ndogo ya Umeme ambako naamini fedha pia zitaendelea kuwa mingi kuwezesha utekelezaji wa miradi mingi ikiwemo miradi ya Mheshimiwa David Kafulila.

SPIKA: Ahsante tunaenda kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari, pole kwa matatizo.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa pole nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote nawashukuru kwa kunifariji wakati wa kifo cha mtoto wangu mpendwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, napenda sasa swali lake namba 127 liweze kupatiwa majibu.

Na. 127

Kujenga Upya Jengo la Karakana la Polisi Wete

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (K.n.y. MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI) aliuliza:-

Ufanisi na utendaji kazi ni pamoja na kuwa na mahali pazuri pa kufanya kazi. Jengo la Karakana la Polisi Wete ni bovu sana kiasi cha kusababisha mafundi wake kufanya kazi chini ya miti.

Je, ni lini jengo hilo litajengwa upya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa jengo la Karakana la Polisi, Wete ni bovu. Kwa hiyo, Wizara yangu imetenga fedha kiasi cha shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo. Fedha hizi zimetengwa katika Bajeti ya mwaka 2011/2012.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pamoja na kuishukuru na kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kuitengeta milioni ishirini karakana hii kwa kuifanyia ukarabati naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la karakana ya Kaskazini Pemba Wilaya ya Wete ya Polisi, tatizo lake linalingana sana na tatizo la karakana ya Polisi ya Mkao wa Kusini iliyoko katika Mkao wa Chakechake; na kwa kuwa katika Mkao huu wa Kusini Pemba, Polisi wamejengewa ofisi ya kisasa kwa kweli nashukuru sana. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuwajengea karakana nzuri ya kisasa Mkao wa Kusini Pemba ili ilingane na jengo lile la kisasa? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri Serikali imetenga milioni 20 kwa ukarabati karakana ile ya Wete.

Je, Serikali itaanza lini kazi hii ya ukarabati na kumalizika lini? Kwa sababu inaweza ikatengwa hela lakini kazi ikawa haifanyiki, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la kwanza. Karakana hizi tunazo katika nchi nzima na shabaha ya kuwa nazo hizi ni katika kukata matumizi kwa sababu magari ya polisi yanavyopelekwa mahali pengine kwa mafundi binafsi au katika gereji za watu wengine gharama zinakuwa kubwa. (*Makofi*)

Tunapokuwa na zetu sisi wenyewe tunadhibiti gharama hizi. Kwa hiyo, hili suala sio la Wete au Chakechake au mahala pengine popote. Ni suala la nchi nzima, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ninakupa kauli kwamba tunavyopata zile fedha ndivyo tunavyoweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba karakana zinakuwepo na zinazidi kuboreshwa. Kwa hiyo, hilo tunalo katika mipango yetu.

Kuhusu swalii lako la pili, lilikuwa linahusu majengo?

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Jengo, kwa sababu wamejengewa jengo jipya la kisasa pale Wilaya ya ChakeChake Mkao wa Kusini Pemba. Je, Serikali itajenga karakana ya kisasa iendane na lile jengo?

SPIKA: Mheshimiwa Faida umefanya kienyeji, unatakiwa kumwuliza Spika kwanza.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, samahani, nadhani nilipokuwa nikijibu sehemu ya kwanza nitakuwa pia nimejibu sehemu ya pili kwamba tunao mpango mzima kuzitazama karakana zote lakini tatizo tulilonalo liko kwenye fedha na tunapopata fedha ndivyo tutakuwa tunatengeneza karakana hizi nchi nzima.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu ya kutia moyo ya Mheshimiwa Alhaj Kagasheki, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninamwomba nimwulize kama ifuatavyo:-

Ni vizuri sana unapokuwa na nyumba ukatengeneza mahali pa kupikia. Lakini inasikitisha ikiwa hiyo nyumba yenyewe itakuwa inaning'inia madirisha. Anayo habari kuwa lile jengo la Makao Makuu ya Polisi ya Mkoa wa Kaskazini nalo linahitaji ukarabati?

SPIKA: Ahsante sana, haya ndiyo maswali mafupi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Al-habib Khalifa, naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge na nasema kwa nia nzuri. Eneo letu la Polisi ndiyo eneo la usalama wa nchi hii. Ni kweli yapo mapungufu lakini wakati mwingine sidhani ni jambo jema kwenda kwa undani na kuonyesha yale mapungufu yetu tuliyokuanayo.

Tunavyo vyombo ambavyo tunaweza tukazungumzia na tukajieleza vizuri zaidi. Hofu yangu na hofu ya Serikali tunapoyatangaza yale madhaifu ya Polisi pote dunia nzima yapo mapungufu lakini tunachelea kwamba tunapokwenda katika undani wa mapungufu yetu tunawapa faida wale ambaa ni maadui zetu. Kwa sababu tusichukulie ile amani na usalama wa Tanzania unakuwepo tu hivihivi bila kufanyiwa kazi. Kazi inafanyika, nataka hili tulitizame katika mtizamo huo. Zipo *forum* tutazungumza na kweli tutaelezana na kweli tunataka Wabunge watusaidie kuona ni njia gani tunaweza tukaboresha matatizo ya Polisi.

Lakini ninapokuja katika swali la Mheshimiwa Khalifa nasema hivi. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi. Matatizo ya majengo ya askari yanaendana na matatizo mengine mengi kama vile vitendea kazi upande wa Serikali. Hakika tungekuwa tuna fedha za kutosha haya yasingekuwepo hata kidogo. Lakini kwa kuwa tunakwenda kwa mujibu wa fedha zinazopatikana ndiyo maana tunakwenda awamu kwa awamu. Nimhakikishie taarifa za jengo hilo tunazo lakini tutakwenda tunafanya kadri ya uwezo wa fedha tutakuwa nao.

Na. 128

Nyumba za Makazi za Askari Polisi Bububu Zanzibar

MHE. JUMA SURURU JUMA aliuliza:-

Serikali ilijenga nyumba kwa ajili ya makazi ya askari wa Kituo cha Polisi Bububu Zanzibar kwa muda mrefu sana nyumba hizo zinafanyiwa ukarabati:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza kujenga nyumba hizo za askari hao ambao wapo kituoni hapo?
- (b) Je, Serikali inajua kwamba katika eneo hilo kuna jengo la zamani ambalo likifanyiwa ukarabati litasaidia makazi ya askari hao pamoja na familia zao?
- (c) Je, Serikali inajua kwamba hakuna gari katika kituo hicho hali ambayo husababisha ufuutiliaji wa uhalifu hasa wakati wa usiku kuwa na tabu sana?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inajenga nyumba za makazi ya askari katika Kituo cha Bububu Zanzibar. Jengo hilo tunalojenga lini uwezo wa kuchukua askari 96. Ujenzi huo upo katika hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012.

(b) Mheshimiwa Spika, pia ni kweli kwamba katika eneo hilo lipo jengo la zamani ambalo askari hulitumia kwa kujihifadhi. Kwa sasa mkakati wetu ni kukamilisha kwanza ujenzi wa jengo jipya ndipo tufikirie kukarabati jengo la zamani.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba kituo hicho hakina gari kinayo pikipiki moja. Kwa sasa Serikali haina uwezo wa kununua magari kwa ajili ya vituo vya Daraja C. Kituo kama hiki cha Bububu ambacho ni cha daraja C kinatakiwa kipate huduma ya gari kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Mjini Magharibi.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri naomba kumwuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wizara imeahidi kulimaliza suala hili la ujenzi wa nyumba ya askari katika mwaka 2011/2012 na kwa kuwa Jimbo letu la Bububu sasa hivi limekuwa na wakazi wengi na kituo hiki kimekuwa ni kidogo. Je, Wizara haioni kuna haja ya kuongeza Kituo hiki kidogo cha Polisi katika maeneo ya Kijichi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuweka Vituo kama hiki anachosema Kituo kidogo anachokizungumzia viro vigezo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili ninalichukua kama ombi tutalitizama kwa vigezo tulivyonavyo vya kuanzisha vituo vya namna hii, na kama itakuwa inakidhi vigezo ambavyo vimewekwa basi hapana shaka tutafanya kila jitihada kuona hili linafanyika.

Lakini kubwa zaidi tutatizama vigezo na tukiona hali inakwendana na vigezo ambavyo tumeweke basi tutaweza kulitizama. Lakini nimwombe Mheshimiwa Mbunge tunaweza tukazungumza zaidi baada ya mahojiano haya.

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu swali dogo la nyongoza. Kwa kuwa malalamiko ya makazi na vituo vya Polisi yamekuwa ni mengi nchini kuhusu nyumba zao ambapo Wabunge tunashuhudia majengo ya Polisi tangu mwaka 1945 kama vile Mkoani, Mtambile na Ngerengere; na kwa kuwa majibu ya Serikali siku zote yamekuwa kwamba iko katika mpango na tunajiandaa mfuko ukiruhusu.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatupatia ratiba ili mtu ajijue katika eneo lake jengo hili litatengenezwa mwaka 2013 au 2025?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, malalamiko anayoyasema hata sisi kama Waziri mwenye dhamana tumekuwa tunayasema na hata katika hotuba yake ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri yatakuwepo. Tatizo ambalo tumekuanalo na tumekuwa tunalisema ni upatikanaji wa fedha. Sidhani kama Serikali haipendi Askari wawe na makazi au kuwepo na majengo ambayo yanastahili askari wake.

Lakini nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba si maneno tu, azingatie kwamba jitihada zinafanyika na majengo mengi yanaanza kujengwa. Zanzibar tumeshajenga majengo mapya ya askari wanapokaa. Hapa Tanzania Bara tumeanza na kweli utaratibu tunaoenda nao sasa ni wa kupata fedha nje ya Bajeti ya Serikali ili kuweza kujenga majengo ya askari.

Sasa anapoomba apewe ratiba nataka nimwambie kwamba nikikupa ratiba hapa hakika wewe mwenyewe ukinitizama usoni utasema nakwambia uongo kwa maana ya kusema kwamba tunakwenda kwa mujibu wa fedha zinazopatikana na Tanzania ni kubwa, mahitaji ni makubwa ya nchi nzima, vituo vya polisi viko nchi nzima na kadhalika.

Kwa hiyo, ni vigumu sana hapa Waziri akaja akakutamkia kwamba 2015 itakuwa hivi 2018 itakuwa hivi. Naomba hilo uvumilie na tutakwenda na mipango ambayo tunakwenda nayo lakini jitihada na nia ya Serikali iko palepale.

Na. 129

Tanzania Kutoendelea Kimichezo

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM (K.n.y. MHE SALIM HEMED KHAMIS) aliuliza:-

Nchi yetu imekuwa ikirudi nyuma katika michezo mbalimbali Kitaifa na Kimataifa badala ya kusonga mbele:-

- (a) Je, tatizo ni nini?
- (b) Je, suluhisho ni lipi?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, nininapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nininapenda kumhakikishia Mhehsimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani kuwa, siyo kweli kwamba, nchi yetu imekuwa ikirudi nyuma katika michezo mbalimbali Kitaifa na Kimataifa. Kumekuwepo na mafanikio katika michezo ya mpira wa miguu, netiboli na kadhalika, japo siyo katika kiwango cha juu. Hata hivyo, nininapenda kukiri kuwa, nchi yetu imekuwa ikitabiliwa na matatizo mbalimbali katika suala zima la maendeleo ya michezo, jambo ambalo limekuwa likichangia kutofanya vizuri katika mashindano mbalimbali hususan yale ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo hayo ni kama ifuatavyo:-

- Ufinyu wa Bajeti ya Serikali na mamlaka nyinginez, hususan katika Sekta ya Michezo.

- Kukosa misingi imara ya kuendeleza vipaji vyya michezo katika ngazo mbalimbali.

- Ukosefu wa uongozi bora katika vyama na vilabu vingi vyya michezo.

- Ushirikishwaji usiokidhi utashi wa wadau katika kupanga na kutoa maamuzi mbalimbali yenye lengo la kuendeleza michezo.

- Usimamizi usioridhisha katika utekelezaji wa mipango iliyoandaliwa kuendeleza michezo hasa vyama vyya michezo katika ngazi mbalimbali.

- Hamasa ndogo mionganii mwa viongozi wa ngazi mbalimbali za kijamii katika kufanya maamuzi ya kusaidia Sekta ya Michezo kama chachu ya maendeleo ya nchi.

(a) Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na baadhi ya matatizo haya, Wizara yangu hivi sasa inakamilisha Rasimu ya Marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Michezo, ambayo itatoa mwelekeo wa maendeleo ya michezo nchini. Vilevile Wizara yangu inaandaa mkakati maalum wa uendeshaji wa michezo kuanzia ngazi ya vijiji, kwa kushirikiana na jamii katika kupanga na kutekeleza mipango inayohusu maendeleo ya michezo. Mkakati huo utashirikisha watoto, vijana, watu wazima na wazee.

Utaratibu huo utaiwezesha jamii na Serikali kwa ujumla kuweza kuratibu kusimamia na kutekeleza mipango na shughuli mbalimbali. Pia jamii itakuwa na wajibu

wa kusimamia na kulinda maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo katika shule, vijiji na ngazi nyingine.

Chini ya mkakati huo, Wizara yangu itaendelea kuhimiza mamlaka mbalimbali kupitia bajeti zao, kuTenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya michezo, pamoja na kuweka mikakati ya upatikanaji wa fedha hizo.

Vilevile Wizara itaendelea kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali kwa Watalaam na Viongozi wa michezo ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji michezo katika mazingira ya sasa.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

- (a) Kwa kuwa nchi kama Kenya na Ethiopia zinatambulika na kuheshimika kwa umahiri wao wa riadha hasa mbio ndefu; je, Serikali ina mikakati gani hasa ya ziada ya kuangalia namna ya kuwekeza katika michezo ya aina hii?
- (b) Kwa kuwa wapo wanamichezo hapa Tanzania waliowahi kupeperusha Bendera yetu na kuipatia sifa nyingi nchi hii lakini hali zao za maisha ni duni na ni mbaya sana; je, Serikali inasema nini juu ya suala hili kwa kuwatelekeza wanamichezo kama hawa?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Masoud, amezungumzia kuhusu uwezekano wa kutayarisha wanariadha mashuhuri kama vile Kenya; nininapenda nichukue nafasi hii kusema kwamba, Serikali ina mpango madhubuti kabisa, tunao makocha kutoka nje tumewatayarisha, kuna vyama vya riadha ambavyo vinatayarisha wanariadha, ambapo mpaka sasa hivi tunapata tatizo kidogo, lakini tunaye kocha kutoka Nje. Kwa mfano, kuna kocha moja anayetoka Ujerumani, Bwana Thum na amejitayarisha kabisa kuweza kutayarisha makocha mbalimbali wa kuweza kufundisha wacheza riadha, lakini pia wacheza riadha mbalimbali ambao wanafundishwa kuhakikisha kwamba, walikuja kutuletea sifa nchi yetu. Bado tuna nafasi kubwa ya kuweza kujifunza, lakini pia kuchukua hii nafasi kuweza kujitayarisha ili tuweze kuchukua ushindi siku zijazo kama Kenya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna chuo chetu cha mafunzo ambacho kinawafundisha wanariadha mbalimbali na tumetenga nafasi Singida, kuhakikisha kwamba, huko tunaangalia tupate wanariadha wa kutuletea ushindi katika nchi yetu

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwengine, swal lake la pili ameuliza kuhusu wanamichezo wetu wengi wanaishi katika maisha duni. Mimi ninadhani ni suala ambalo mpaka hivi sasa nchi yetu haijatilia maanani au Wananchi wenyewe hatujachukulia michezo kama ajira rasmi, ambayo inaweza kutuletea maendeleo. Kwa hiyo, kwa hivi sasa Serikali yetu inatoa mpango maalum wa kuhakikisha kwamba, kuanzia sasa na siku

zilizopita, Wananchi wetu tunataka tuwaangalie na kuwahimiza kuhakikisha kwamba, wanachukulia michezo kama ajira; pia kujitayarisha kwamba, shughuli za michezo ni wajibu wa jamii; na Serikali imepanga kuanzisha kama nilivyosema, jukumu la kuhakikisha kwamba, tuna michezo kwa jamii ambayo itahakikisha kuwa, michezo inachukuliwa katika ngazi ya jamii kama jambo muhimu pamoja na Halmashauri yetu pia kuhakikisha kwamba, wanaweka viwanja rasmi na kuhakikisha wale amba wanashika nafasi za michezo tunawaangalia kwa karibu. Ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha. Nina matangazo ya kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, aninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa, leo watakuwa na kikao, saa saba mchana katika Chumba Namba 227. Amenambia saa tano, lakini Kamati zote sasa zitakuwa zinakaa saa saba mchana, kama kuna maelezo itabidi nipewe mimi mwenyewe na nikubali. Tumejifunza kwamba, tunapoweka Vikao vya Kamati wakati Kikao cha Bunge kinaendelea, Bunge linakuwa wazi. Kwa hiyo, maelezo niliyopewa sijaridhika nayo, Kamati hii itakutana saa saba mchana. Hivyo hivyo Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Juma Nkamia, aninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo kutakuwa na kikao kwenye Jengo la Utawala, ghorofa ya pili, Chumba Namba 219, wao pia watakutana saa saba mchana.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Diana Chilolo, aninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa C. Kikao hicho kitafanyika saa saba mchana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, aninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa B, saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge, ninasema saa saba mchana, kwa sababu kazi wanazokwenda kufanya zilianzia Dar es Salaam, kwa hiyo, hatuwezi kuendelea kutumia muda wa hapa, watumie muda wao wenyewe na kama kuna mabadiliko kamili mtanieleza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1), imenibidi nirekebishe muda wa kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Jumamosi niliitisha Kikao cha Kamati ya Uongozi ili tushauriane juu ya mwenendo wa uchangiaji wa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kutokana na kuwa na idadi kubwa ya Wabunge waliojiorodhesha kuchangia na ili kutoa nafasi kwa Wabunge wengi zaidi, ambao wameomba kuchangia Hotuba hii na hawajachangia kabisa katika Hotuba zilizopita. Kamati ya Uongozi, imeazimia kuwa, mjadala wa Hotuba ya Waziri Mkuu uongezewe siku mbili. Hivyo basi, badala ya kufunga mjadala Siku ya Jumatano, Tarehe 29, tutaendelea mpaka Siku ya Ijumaa, tarehe 1 Julai. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, idadi ya Wabunge ambao hawajachangia katika Hotuba hiyo na wameshajiorodhesha tayari ni Wabunge 107 na wote watapata nafasi hadi Ijumaa saa sita. Kwa hiyo, nininapenda kuwafahamisha kuwa ili tuweze kutekeleza hilo kikamilifu, tumefunga kupokea maombi mapya ya kuchangia na ninaomba tujitahidi kutumia muda vizuri, kwa kupunguza hongera, pole, miongozo na taarifa, kwa sababu haya yote mtu anapewa nafasi yake kuchangia wewe unamtolea Mwongozo au taarifa; unahuusika nini na hotuba yake? Mwache atoe hotuba yake, kama amekuudhi sana basi kuna utaratibu mwininge wa kumweleza baadaye siyo katikati ya maelezo yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na uamuzi huo, Kamati iliazimia kusogezza mbele shughuli za Serikali kuhusiana na Miswada kwenye Mkutano huu. Kwa hiyo, Miswada ambayo ilikuwepo katika orodha yetu ya mwanzo itaingia mwezi wa Oktoba.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sana maana ninaona watu wanaendelea kuandika, hapa hatutapokea maombi ya kuomba kuchangia Hotuba na orodha yetu mtaiona wakati wote katika *pigeon hall* yetu, kila wakati tutaonesha wale waliochangia angalau mara moja. Hii haina maana kwamba, wewe hautaweza kuchangia; kama ninyi ni wachangiaji wazuri, kuna Wizara zinakuja, sasa jipange Wizara yako unayopenda kuchangia. Ukifanya kosa basi hutapata muda.

Waheshimiwa Wabunge, kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, tumefunga kupokea maombi ya ziada. Tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(*Majadiliano yanaendelea*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, alikuwa aanze kuchangia, lakini imebidi aondoke asubuhi hii kwenda kushiriki kwenye mazishi nyumbani kwake Kondoaa, kwa hiyo, atapata nafasi kesho. Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa atachangia, Mheshimiwa Mariam Kisangi atakuwepo, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Fakharia Shomari Hamis.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili Tukufu, ninaomba nichukue fursa hii, kuwashukuru sana Wananchi wangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, kwa heshima ya kipekee waliyonipa mwaka 2010 ya kupita bila kupingwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii, kuwashukuru kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza kazi zetu na majukumu ya Kibunge katika maeneo yetu.

Mhehsimiwa Spika, ninaomba nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi, kwa kuniteua kugombea Ubunge katika Jimbo la Mufindi Kaskazini. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, kwa ushindi mkubwa aliouputa usiokuwa na shaka ndani yake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa ya kipekee, kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, kwa Hotuba yake nzuri na yenye mwelekeo ya kuwasaidia Watanzania wengi kujikwamua na matatizo.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwangu nininapenda nijielekeze kwenye *allocation of resources*. Wilaya yetu ya Mufindi ni moja ya Wilaya ambayo ina viwanda vingi katika nchi hii ya Tanzania, ina viwanda vikubwa vinane na ina viwanda vidogo 367. Kuna jambo moja linanisikitisha sana, pamoja na kuwa tunalipa kodi nyingi kwa Serikali kwenye hivi viwanda vikubwa vinane, lakin *allocation* ya pesa za matumizi zinazokwenda kwenye Mikoa ya Iringa na hasa katika Wilaya ya Mufundi hazilingani na hali halisi ya pato tunalochangia kwenye Taifa. Ninaomba Waziri Mkuu atuangalie sana, ajitahidi kutusaidia na kururudishia sehemu ya pesa ambazo tunazitoa katika mchango wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie Ahadi za Rais. Ninaomba kumpongeza Rais, kwa kutuahidi kutupatia kilomita tatu za lami na ninaomba niishukuru sana Serikali kwa sababu ahadi hiyo imeshaanza kutekelezwa. Jana nilikuwa Mufindi na nimeona wanamalizia kuweka lami katika lile eneo ambalo aliahidi Rais; ninaomba niishukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, nininapenda nichukue fursa hii, kumkumbusha Waziri Mkuu, Rais na Makamu wa Rais, mwaka 2010 wakati wa kuomba kura aliahidi ndani ya miezi mitatu atatuletea benki nyingine katika Wilaya ya Mufindi zaidi ya *NMB*. Nimejitahidi kukutana na Waziri wa Fedha na wakati mwingine nimekutana na Waziri Mkuu mwenyewe, jambo hili limekuwa ni kero na adha kubwa kwa Watu wa Mufindi. Wanatembea zaidi ya kilomita 70 au 80 kwenda kutafuta huduma za Kibenki katika maeneo mengine. Ninaomba sana, Waziri Mkuu, aliangalie jambo hili, linawezekutuletea athari kubwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Mufindi Kaskazini lina Kata 15, lakini cha kusikitisha, kuna zaidi ya Kata kumi hazina maji na zaidi ya vijiji 68 havina maji. Hili ni jambo bayo, Wananchi wanatumia muda wao mwingi kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za maendeleo. Ninamwomba Waziri Mkuu, wakati anagawa *resources* hizi aliangalie sana suala la maji katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii vilevile, niishukuru sana Serikali, kwa jitihada zake ilizozifanya za kuhakikisha tunapata Shule za Sekondari za Kata katika nchi nzima. Hilo ni fanikio kubwa na ndani ya mafanikio ni lazima matatizo yawepo na kero ziwepo, hizi kero tusizichukulie kama ni matatizo, tuzichukulie kama ni changamoto, kuna matatizo ya Walimu, vitabu na maabara. Ninaomba Waziri Mkuu,

jambo hili ambalo Rais aliahidi, litekelezwe haraka iwezekanavyo ili wanafunzi wetu waweze kupata huduma za msingi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii, kuzungumzia suala la misitu. Wilaya ya Mufindi, ina msitu amba ni mkubwa katika misitu yote katika Bara la Afrika, lakini cha kusikitisha, msitu ule umekuwa kero kubwa sana kwa wenyeji hauwasaidii kabisa. Wenyeji wanakuwa siyo sehemu ya mgawo katika msitu ule; hii ni kero. Wanahehimika na kutambulika yanapotokea matatizo kama ya moto. Ninaomba Waziri Mkuu, aliangalie jambo hili, kwa sababu Wananchi wa Wilaya ya Mufindi walipokuwa wanatoa ardhi kwa Serikali, walikuwa wanaamini kabisa itawasaidia kupata ajira na kupata kuni katika maeneo ya msitu. Jambo la kusikitisha ni kwamba, vibali vimegawiwa kinyemela huko Makao Makuu ya Wizara ya Maliasili na jambo hili limekuwa kero kubwa sana katika Wilaya yetu. Ninamwomba sana Waziri Mkuu aliangalie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile jambo la kusikitisha sana, unakuta sisi ndiyo tuna msitu mkubwa, lakini baadhi ya vijana wetu wanaosoma katika Shule za Msingi na Sekondari, wanakaa chini au wanakalia madawati ya udongo kule kwetu tunaita “*Madobe*.”

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii, kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atusaidie katika miundombinu. Pamoja na uchumi wetu mkubwa, amba tunachangia katika Pato la Taifa, lakini tumekuwa tuna kero kubwa sana katika Wilaya ya Mufindi hasa kwa barabara inayotoka Kinyanambo C mpaka Kisusa. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa hili, kwa sababu ndiyo kwenye vyanzo vya umeme kama Bwawa la Kihansi, lakini cha kusikitika ni kwamba, linapitika kwa vipindi tofauti, lilitakiwa lipitike mwaka mzima. Wananchi wanatembea zaidi ya kilomita 50 kwenda kutafuta huduma za usafiri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu, pamoja na maelezo mengi mazuri, lakini hakuzungumza kwa kina juu ya ajira. Ajira ni bomu ambalo linaweza likalipuka wakati wowote. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Serikali yetu, ijipange ili kuhakikisha Wananchi wanapata ajira za uhakika kupitia vyanzo tulivyokuwa navyo na rasilimali tulizokuwa nazo. Rasilimali nyingi zimeelekezwa kwa watu wa kuja badala ya wazawa. Ninaomba tuliangalie jambo hili kwa kina. Unakuta katika Wilaya yetu ya Mufundi, rasilimali nyingi za uhakika zinamilikiwa na wageni. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutengeneze mazingira ya kina kuhakikisha tunawasaidia Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba nizungumzie kidogo kuhusu suala la kilimo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo na asilimia 75 ya Wananchi wa Tanzania wanategemea kilimo. Nimeridhika sana safari hii niliposikia kwamba, Serikali imeelekeza zaidi ya bilioni 100 katika kuisaidia *TIB* iweze kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Spika, hizi hela ninaomba zisiihie mjini ziende kwa walengwa. Sisi tuna Benki kama Mkoba, ambayo mwaka jana tulipewa milioni 500 kupitia *TIB* kwa ajili ya kuwasaidia Wananchi, lakini bado hazikuwatoshna na hazikuwasaidia chochote.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, safari hii angalieni hasa hasa maeneo hususan itakuwa busara kama mtaongeza hela kwenye maeneo ambayo ndiyo uti na kitega uchumi katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii, kuzungumzia kidogo kuhusu habari ya umeme. Umeme ni tatizo katika nchi hii na tumekuwa tunazungumzia kutatua matatizo ya umeme kwa njia ambazo ninaziona siyo mwafaka kabisa. Tuna makaa ya mawe ya Liganga, lakini Serikali haijaonesha *concentration* ya kina kwamba, ina nia ya dhati ya kuyatumia makaa ya mawe Liganga na makaa ya mawe yaliyoko Ngaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama kweli tuna nia ya kutaka kutatua tatizo la umeme, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Serikali yake, waelekeze nguvu zao zote Liganga na Ngaka, kule ndiko kutakakopatikana *solution* ya kweli ya umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo la kusitikisha katika Wilaya yetu na Jimbo letu la Mufindi Kaskazini, vyanzo vya umeme kama Bwana la Kihansi lipo pale, lakini cha kusikitisha, vijiji vyote vinavyozunguka Bwana hili havipati umeme. Umeme unavuka tu kwenye vyanzo vya umeme unakwenda kwenye maeneo mengine. Ninaomba mliangalie sana hilo hasa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Itakuwa ni fedheha na aibu, watu ambaao wanalinda mabwawa wasipate umeme waende kupata umeme katika maeneo mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nininapenda kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu. Ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, ninapenda nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote waliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Ninawapongeza sana; hongereni sana. Ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama muda utaniruhusu nitachangia katika maeneo yafuatayo: Ujenzi wa Barabara, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maendeleo na Sekta ya Uwekezaji na Ubinafsishaji, Elimu na Afya.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaishukuru Serikali kwa kuweka mkazo katika ujenzi wa barabara. Kusema kweli maendeleo ya barabara tunayaona na hasa Mkoa wa Dar es Salaam, lakini bado msongamano wa magari ni mkubwa sana, kutokana na idadi ya magari ambayo yanaingia kila siku Mkoani Dar es Salaam. Pamoja na Serikali kujitahidi sana katika ujenzi wa barabara, kila palipo na jambo zuri hapakosi kuwa na kasoro, lakini hatusemi ni kasoro ni changamoto; Mkoa wa Dar es Salaam na hata sehemu nyingine, katika ujenzi wa barabara kumezuka heka heka ya watu kuvunjiwa majumba yao yaliyo pembezoni mwa barabara. Hili ni tatizo. Wananchi walijenga

nyumba zao wengine miaka 70 iliyopita, miaka 60, leo wanaambiwa wasogeze nyumba zao kwa ajili ya barabara. Hili ni tatizo, ni maendeleo, maendeleo hayawezi kufika bila barabara kujengwa. Maendeleo hayo ndani yake yanakuwa na msiba mkubwa. Kuna watu ambao ninawatambua, nimewaona kabisa katika zoezi la ujenzi wa barabara wakianguka na kuzimia, wengine wamekufa, kwa kukosa makazi. Nimeona kwa macho yangu, mfanyabiashara mmoja anaitwa Sinde, alikuwa anauza soda za jumla Mbagala Rangi Tatu, alivunjiwa nyumba yake haikubaki hata tone. Huu ni mtihani, Mtoni kwa Aziz Ally, kuna baba mmoja alikuwa anauza vifaa vya ujenzi, anaitwa Mzee Khamis, alivunjiwa nyumba yote, yaani akabaki hana kitu na akapata *pressure* na *stroke* juu.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba, maendeleo yanakuja na ujenzi wa barabara na makazi bora. Pale tunapowaua watu kiuchumi; hii barabara atatumia nani? Anayetakiwa kutumia ndiyo huyu mwekezaji au mfanyabiashara; leo tumemaliza nyang'anyang'a kabisa tunamwekea nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, Wakazi waliopo kwenye eneo la *Kilwa Road*, wawaangalie kwa jicho la huruma. Kibaya zaidi ni pale panapotangazwa kwamba, Wananchi wa barabara kutoka sehemu fulani kwenda sehemu fulani walioko pembezoni wanalipwa fedha zao. Eneo fulani hapa na hapa wanalipwa kwa kuvunjiwa. Hii hali inawafanya Wananchi wengine waonekane kama wao hawatakiwi na Serikali yao. Wananchi wanakuwa wanyonge na hawailewi Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iwe na maamuzi magumu katika hili, wawaangalie hawa Wananchi. Viongozi tunajitahidi kuongea na Wananchi, Wananchi wetu ni watii wanasikiliza, sasa hivi ni miaka mitano imepita huu ni wa sita, hakuna maelezo yanayolelewka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu, uwaangalie hawa Wananchi kwa jicho la huruma wapewe haki zao. Kibaya zaidi, hao hao watu wa *Kilwa Road*, kuna waliokwenda mahakamani walilipwa fedha zao, lakini yule raia mwema ambaye haendi mahakamani, haitii hasara Serikali yake, kwa sababu unapokwenda Mahakamani Mwanasheria wa Serikali, anakwenda kushiriki mahakamani. Kama hatashiriki Mwanasheria wa Serikali, basi attachukuliwa hata Mwanasheria binafsi akaiwakilishe Serikali kwenye kesi hiyo. Hiyo ni hasara tayari wanaitengeneza. Yule raia mwema ambaye ye ye hakwenda mahakamani bali anahitaji Serikali yake imwangalie, anaonekana ye ye hafai kulipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba tuangalie, wapo watu wazuri wanaipenda Serikali yao na nchi yao, kila siku wanakaa wakisubiri leo Serikali yetu itatuona; basi ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awaone Wananchi wa *Kilwa Road* na maeneo mengine. (*Makofi*)

Nije kwenye eneo hilo hilo la ujenzi wa barabara; ninaomba uweke mkazo wa dhati, barabara ambayo inatoka Kibambe – Segerea - Kinyerezi na kufika *Airport* au

Majumba Sita ni muhimu sana ili kupunguza msongamano wa magari uliopo katika Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninamwomba tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara ambayo inatoka Mbezi kufika Tangibovu itawasaidia sana Wananchi wa Dar es Salaam kupunguza msongamano wa magari katikati ya Mji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia tuangalie uwezekano wa kujenga daraja kutoka Kilungule Buza kwenda Jeti; njia hiyo ni nyepesi sana. Dakika tatu mtu anatoka Mbagala anafika Uwanja wa Ndege, lakini tatizo lililopo ni daraja dogo tu kwenye ule mto; matatizo yanayotokana na *TAZAMA Pipeline*. Ninaomba Serikali yangu ikae na Watu wa *TAZAMA Pipeline* iangalie tatizo hili nasi tupate wepesi. Barabara hii ni fupi mno kufika *airport*; kwa kweli itatusaidia sana. (*Makofi*)

Nije kwenye eneo la Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Serikali yetu inajitahidi, Halmashauri zetu zinajitahidi sana kutafuta fedha kuwatafutia Wananchi viwanja ili waweze kupata makazi bora. Kinachoshangaza, viwanja hivi vinapopatikana watu hawaviedelezi, matokeo yake kuna watu wanatafuta maeneo ya kuishi, viwanja vimekaa mpaka leo havieleweki vya nani. Je, kwa *style* hiyo tutapata maendeleo kama viwanja vinalimbikizwa mtu anakwenda achukua viwanja 50, 60 sasa vitaendelea vipi? Mimi ninaomba Serikali iweke mkakati madhubuti kwamba, iwapo mtu anachukua kiwanja kwa miaka mingapi anatakiwa awe amekiendeleza; vinginevyo, tunakwenda mbele. Sisi Kigamboni tunachukua viwanja, lakini Viwanja vya Twangoma, Viwanja vya Kizota 20,000, Viwanja vya Mbezi, Viwanja vya Chanika, sijaviona kama vyote vimekwisha na sasa hivi ni zaidi ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iweke maamuzi, mtu akipewa kiwanja leo baada ya miaka mitano ajenge, hana uwezo wa kujenga au hana shida ya kiwanga, apewe mwengine ambaye anaonekana ana tatizo la kweli. (*Makofi*)

Nije katika Sekta ya Ubinafsishaji na Uwekezaji. Kwa kweli ubinafsishaji ni muhimu, lakini bado una athari zake. Sisi katika Wilaya ya Temeke, eneo la Kijiji Pembamnazi tumewekewa maeneo ekari na ekari hatumjui hata mwenyewe nani. Mwingine ameweke ekari 400, mwingine ameweke ekari 200, yale maeno ni ya akina nani tunaambiwa ni wawekezaji na wameweke wana sheria gani mpaka leo hii zaidi ya miaka kumi hayana uendelezwaji wanatuwekea mapori, wanatujazia wanyama waharibifu na nyoka tu. Mimi ninaomba Serikali yako kuititia Wizara ya Miundombinu, wakakague maeneo hayo na kama wao hawana shida na hayo maeneo, basi Serikali iyataifishe iwave Wananchi, Wananchi wana shida ya mahali pa kukaa. Dar es Salaam hakuna mashamba kuna miji sasa igawiwe viwanja watu wapate makazi bora. Walimu wetu, manesi wetu na madaktari, wanahitaji makazi bora. Kwa hiyo, haya maeneo yakikatwa kuwa viwanja yatatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la elimu na afya; elimu nimekuta wenzangu wengi wanazungumzia juu ya walimu wa vijijini waongezewe posho. Ndugu zangu, walimu wote matatizo yao ni sawa, aliye mjini anakumbana na changamoto ya

kodi ya nyumba, *rent* za nyumba mijini ni gharama. Tunaona hapa Dodoma, ukichukua *apartment* ndogo shilingi 250,000 mpaka 300,000. Sasa huyu mwalimu anayefundisha pale Dodoma Mjini anaishije? Tukiangalia kijijini naye ana unafuu wa nyumba na chakula, lakini ana ugumu wa maeneo fulani fulani. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iwaangalie walimu wote kwa pamoja, kwa huruma kwamba, hawa wanapata matatizo pamoja na madaktari wetu na manesi wana hali ngumu, ikiwezekana hata posho za mazingira magumu wapewe. (*Makofi*)

Ninaiomba Serikali yangu iangalie upande wa kupunguza muda wa kazi kwa walimu walioko vijijini. Mjini walimu wanamaliza kazi saa nane mchana, lakini vijijini wanamaliza saa kumi; wanakatisha masomo mchana watoto waende kula kutokana na kipindi nilichokiona cha *TBC International* huko Mkoa wa Pwani wanasesma, watoto hawaendi kula kwa sababu wanakaa mbali na bibi zao watakuwa hawapo wamekwenda shambani. Kwa hiyo, wanakaa pale pale shulenii wanacheza mpira mpaka wanaunganisha saa kumi. Ninaiomba Serikali iangalie tena na hawa walimu wa vijijini nao waweze kuishia saa nane watoto wakapate chakula na walimu wakapate chakula. Pia walimu wafanye shughuli nyingine za kujitegemea kama hapa mjini, kama tunavyoona kwamba, changamoto zao wote ni za aina moja.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii ya kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Bajeti ya Mwaka 2011/2012. Ninataka pia niwashukuru Wananchi wangu wa Jimbo la Uchaguzi la Ngorongoro, kwa kunichagua kwa kura nyngi. (*Makofi*)

Ninataka niwaambie tu kwamba, utaraguzi umekwisha, tuenze sasa kushughulikia maendeleo ya Wilaya yetu, ambayo ni kubwa na ina changamoto nyngi za kimaendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakwenda kwenye maendeleo. Katika Hotuba ya Waziri wa Fedha, umeme umepewa kipaumbele namba moja katika Bajeti ambayo tunaanza hivi punde. Utaratibu wa *TANESCO* kuipa Wilaya ya Ngorongoro umeme ilikuwa ni mwaka 2015. Ninapenda niishukuru Serikali kuitia kwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, utaratibu huu umekuja mapema zaidi, miaka mitatu au minne, kuliko utaratibu uliokuwa umewekwa awali. Ninaishukuru sana Serikali kwa hatua hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni tutawasha jenereta ambazo tumezipata, labda matumizi ni kuwasha jenereta hizo hizo katika mwezi *August* au mapema *Septemba* na hii pia ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, alipotembelea Ngorongoro kule Samunge na Loliondo mwaka 2007. Ninashukuru sana kwamba, ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais sasa imetimia. Ninataka niseme huu ni mradi mkubwa kabisa kwa Wilaya ya Ngorongoro tangu Uhuru. Tunaelekea miaka 50, mimi ndiyo kwanza ninapata umeme. Ninaishukuru sana Serikali ya CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ninataka niwaambie Wananchi wa Ngorongoro, sasa wachangamkie fursa hii waanzishe miradi midogo midogo inayotumia umeme. Vilevile Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, inaweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo na mazao ya mifugo ili kupelekea Wilaya ya Ngorongoro kukua kwa kasi zaidi. Kwa sababu nimeambiwa umeme huu ni mwangi kiasi kwamba, kwa kweli tunahitaji tuanzishe viwanda. Mji Mdogo wa Waso na Loliondo na vijiji vya jirani na hoteli za kitalii zilizoko jirani, wanaweza kutumia huu umeme ambao ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka nimwombe pia Waziri wa Nishati na Madini, waendelee kutafiti maji ya Mto Pinyinyi, kwa sababu yale maji ni mengi na utafiti ukikamilika, unaweza ikawa pia ni chanzo kingine cha kupata umeme katika maeneo ya *Lake Natron* na Wilaya ya Ngorongoro kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, miundombinu na hasa barabara, imepewa kipaumbele namba tatu katika bajeti. Mambo ambayo yanaendeleza miji ili kwenda kwa haraka zaidi ni masuala ya barabara, masuala ya umeme, mambo ya maji kama yanapatikana kwa wingi, viwanda na hata utalii. Wilaya yangu ya Ngorongoro ina karibu vyote hivyo sasa tumepata umeme ila barabara bado ni mbovu sana. Barabara ya kutoka Lodware Geti inakoishia lami, ukipita Karatu ukafika Lodwale Geti kabla ya kuingia Hifadhi ya Ngorongoro na kwenda mpaka Golini, ukitoka Golini ukielekea Loliondo, hakuna barabara kabisa. Ile mbuga ni hifadhi, imeharibika kwa kila gari kutafuta njia yake. Unafiga pale unaambiwa uelekeo wa kwenda Loliondo, mbele kilomita kama nane kuna milima matiti pita kulia au kushoto. Sasa magari yameharibu sana sehemu ile na ndiyo maana nilikuwa ninaomba barabara ya kutoka Olbalbal kwenda Nasirarok kupita Piaya, Ormanyie kwenda Loliondo, itengenezwe japo kwa kiwango cha moramu, inaweza ikasaidia kupunguza magari ya kupita Mbugani na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mto wa Mbu – Loliondo, ni barabara ambayo imekuwa na kelele sana na ninadhani barabara hii kwa kuwa Serikali ilikuwa imeshadhamiria kuijenga, ilishaweka katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010/2015 kwamba; itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Kwa sababu inapata upinzani mkali, lakini ninaamini bado itatengenezwa kwa sababu imeshaingia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na katika Bajeti ya mwaka huu ambauto tutaanza hivi punde, imetengewa shilingi bilioni moja na milioni mia sita. Hata hivyo, wamepunguza kwa kiasi kidogo, lakini barabara hii ni ukombozi mkubwa sana kwa Wananchi wa Ngorongoro na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais pia mwaka 2007 na yeze mwenyewe alijaribu kukabiliana sana na upinzani wa barabara hii, ametetea kwa nguvu zake zote na sisi Wananchi wa Ngorongoro tunamuunga mkono, barabra hii itengenezwe kwa kiwango cha lami. (*Makofit*)

Jirani zetu Kenya nao wanatupiga vita sana kuhusu hii barabara, lakini na wale wote ambaeo wanaweka masuala ya wanyamapori mbele kuliko maendeleo ya watu, ndiyo watu ambaeo wanaipiga vita hii barabara. Hoja yao wanasesma barabara hiyo itaharibu mfumo wa ikolojia ya hifadhi ya Serengeti, ambayo wanasesma ni uruthi wa ulimwengu. Hivi kufanya Serengeti urithi wa ulimwengu wamemshirikisha nani na urithi wa

ulimwengu katika maeneo mengine ya Mataifa yaliyoendelea; hivi sisi tumeshakwenda huko tukaona tunafaidika vipi na huko wanakosema?

Wanyamapori hawa, ninaomba wasije wakawa ni kizingiti au tabu sasa kwa maendeleo ya watu. Mbona ukienda Afrika ya Kusini, jirani tu hapa, unakwenda *Kurga National Park*, njia yote ni lami ndani ya hifadhi; lakini mbona tumeweka lami Mikumi? Maana hata kama ni kugongwa kwa wanyama ni sawa na wewe ukipakia mifuko ya simenti kwenye lori, kule kupakia na kusafirisha na kwenda kupakua, lazima mifuko fulani itapasuka tu. (*Makofi*)

Upasukaji ule ni *reasonable*, lakini ninasema hata kama hii barabara itajengwa, itawekwa *mitigation measure*, wataweka matuta, watafanya nini, hakuna mtu atakayeendesha kwa *speed* kiasi cha kugonga wanyama. Jamani ninasema Watu wa Ngorongoro wanaihitaji hii barabara, tuwaangalie kwa jicho la huruma zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la njaa; Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuona juu ya jambo hili na umekuwa *sympathetic*, umelewa sana hali yetu ya Ngorongoro, Watu wa Ngorongoro wamo katika zile Wilaya 48 ambazo umeainisha katika Hotuba yako ya Bajeti. Wilaya ya Ngorongo ina hali mbaya sana ya chakula na imekuwa mbaya zaidi kwa sababu mmoja uliopita, Serikali ilipiga marufuku kilimo cha bustani katika Tarafa ya Ngorongoro.

Kilimo ambacho Wamasai wale wanalima katika mahame, unababilisha boma limechakaa sana unaweka pale viazi, unaweka kitu kingine kidogo, hii imewasaidia sana muda wote. Sisi hatujawahi kupata tabu ya njaa kama ambavyo tunakabiliana nayo sasa na hii ni kwa sababu ya kupigwa marufuku hizo bustani. Sasa ninaomba Serikali ibebe jukumu la kulisha wale watu, msituambie tuna mifugo, mifugo imekufa kwa wingi kutokana na mambo manne makubwa: Moja, *volcano* ya Mlima Lengai, ile *eruption* ilipotua kwenye nyasi imeunguza majani yote, imeunguza kila kitu na vyanzo vya maji vimekauka. Kupigwa marufuku kwa kilimo kumetuletea njaa kubwa zaidi. Vilevile mifugo imekufa na mvua haikunyesha kabisa kwa miaka mitatu mfululizo, imenyesha kwa mtawanyo amba siyo mzuri. Kwa hiyo, ninaomba Serikali itusaidie chakula, kwa sababu Wananchi wale wana njaa kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niliseme ni kwamba, tulipata mlipuko wa Ugonjwa wa Surua hivi karibuni na ninashukuru jitihada zilizochukuliwa na Wilaya na Mkoa, pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, wamejaribu kuidhibiti hali hiyo. Ninaomba sasa Wizara ipeleke waganga na madawa ya chanjo ili kuendelea kukabiliana na hali hiyo na ninakushukuru Waziri Mkuu vilevile, nilikueleza hili na ulipiga simu kwa Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Babu wa Loliondo; ninataka nimseme kidogo huyu Babu. Ninawashukuru wote waliokwenda Loliondo kupata Kikombe cha Babu na waliopata wanajua wenyewe, ndiyo wanaweza kutoa ushuhuda kama wamepona au namna gani. Ninasema kwamba, Serikali kama inavyohimiza, waendelee kupima afya zao hata baada ya kupata Kikombe cha Babu na ninashukuru Serikali yetu ilisema

kwamba, dawa ile haina madhara, sasa anayepata kikombe akapime baada ya hapo ili atoe ushuhuda. Kuna mtu mmoja wa Blantire, Malawi, amepona kabisa ugonjwa wake, mimi sitaki kuwaambia ni ugonjwa gani, amemletea Babu gari aina ya Toyota Pick Up, yenye *Registration Number BL 9238* na lipo pale Samunge, Babu anatumia na Vijana wake kwenda kuchukua dawa, kwa sababu dawa ile sasa inapatikana mbali kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Babu huyu ameisaidia Wilaya ya Ngorongoro, sasa ipo juu kama mkungu wa ndizi, imefahamika ndani na nje ya nchi. Niwaambie ndugu zetu Kenya hawa siyo majirani wazuri sana; kila siku likitokea jambo zuri Tanzania wanasesma lipo kwao; Serengeti wanasesma ipo kwao, Kilimanjaro ipo kwao; na sasa Saminge wanasesma ipo Kusini mwa Jamhuri ya Kenya! Wanasesma hivyo ili kuwakatisha watu tamaa, wanasesma kutoka *Kilimanjaro International Airport* kwenda Samunge ni kilomita mia nane na hawasemi kama ni kwenda na kurudi, lakini kutoka Nairobi au *Wilson Airport* kuja Samunge ni kilomita arobaini na tano, ambapo ukweli ni kwamba, ni zaidi ya kilomita mia tatu ukipitia Narok kuja Loliondo kwenda Samunge. Sasa mimi ninashangaa, hivi kwa nini sisi hatukanushi hivi vitu? Sasa hivi watu wanokwenda Samunge kwa wingi kabisa wanatoka Kenya na siyo Wakenya wenyewe ni watu amba wanatoka sehemu mbalimbali, lakini wanatua Nairobi, Jomo Kenyatta, Wilson, wanachukuliwa na magari yao.

Sisi ingekuwa huyu Babu kaoteshwa kutoka Kenya, leo magari yetu yangepeleka watu mpaka mpakani mwa Kenya, magari ya Kenya yamesimama upande wa pili yanawapeleka, lakini wao wanatoka Nairobi, wanatoka kila mahali Kenya, wanakwenda moja kwa moja Samunge; kwa nini jambo hili linakuwa namna hiyo? Ninaomba Wizara inayohusika, nchi kama inasema uongo wa mchana, hivi hakuna namna ya kuwaambia mnachosema ni uongo?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis na Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, ajiandae.

MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia leo kusimama mbele ya Bunge hili na kuweza kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sina budi ya kumshukuru mama yangu mpendwa, Mama Asha Binti Ramadhani, kwa kuniombea Dua na leo nipo katika Ukumbi huu. Vilevile sina budi kuwashukuru Umoja wa Akina Mama (UWT), Mkoa wa Mjini Magharibi, kwa kunipa kura za kutosha na kuniwezesha leo kuwa katika Ukumbi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na kumpungeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba nzuri, inayotekelzeza na ndiyo maana watu wengi wana hamu ya kutaka kuichangia kwa jinsi alivyoikita Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwenye Hotuba yake na leo watu wote wakawa na hamu nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia mambo madogo madogo ya kuboresha maana ninajua *speech* ni nzuri, haina matatizo, uzuri wake ni kuiboresha ili kuiongezea heba. Nitaingia katika Tume ya Kuratibu Madawa ya Kulevy. Kitengo hiki kinahitaji msaada wa Serikali, madawa ya kulevy ni tatizo la jamii, la vijana wetu, maana tukisema vijana hata na watu wazima, maana wengine wanaona kama wanafanya uraibu kumbe ni tatizo kuu na janga la nchi. (*Makofi*)

Kitengo hiki kinahitaji usaidizi mkubwa kwa sababu wahusika wake walikuwa na haki ya kuwa na ulinzi, magari ya kutosha na mkemia wao wa kuchunguza madawa yao, lakini ukiangalia vitu vyote hivyo kwao ni tatizo. Ukiangalia magari hawana, wakati unajua wanaowafuatalilia ni watu amba wana uwezo, kwa sababu mtu anatengeneza maisha yake ya uchumi kwa kutumia madawa wakati ni kitu haramu, lakini ye ye anaona kwake ndiyo uchumi wake. Yupo tayari hata kumdhuru atakayekuwa anamfuatalilia, sasa yule atakayekuwa anafuatalilia anatakiwa awekewe ulizi wa kumsaidia. (*Makofi*)

Mkurungenzi hana ulinzi wala bima; hivi leo mimi nikamate madawa ya kulevy, muhusika mkuu nimemkamata yuko ndani, lakini ye ye anaao mtandao wake; ule mtandao unaweza ukamdhuru au wakati mwagine tunataka kusema watu wafuatalie, unakuta kuna gari moja la Mkurungenzi; hao wanaotaka kufuatalilia watafuatalilia kwa kitu gani? Tunataka kwenda bandarini, *airport* na vijijini; tutakwenda na kitu gani; na huo ulinzi utakuwaje? Umeshaletewa taarifa huko kwamba, tayari madawa ya kulevy yako pahali fulani na gari lililokuwepo ni la Mkurungenzi, pengine kaondoka kaenda sehemu fulani; kazi hiyo ipo? Kusema unachukua taxi, siyo utaratibu maana Gari la Serikali lina utaratibu wake na tai ina utaratibu. Sasa ningeliomba Mheshimiwa suala hili uliangalie linasababisha rushwa. Wakati nimeshakamata unga na unga ule inabidi lazima uende kwa Mkemia wa Serikali, Kitengo hakina Mkemia, hapa katikati mwanya uliokuwepo tayari rushwa inacheza na itakapocheza rushwa katikati, utaambiwa kwamba ule uliokamatwa siyo unga ni saruji, unga wa ngano; sasa kazi hiyo itakuwa imefikia wapi? Itakuwa tunafanya kazi ya zeze, hatufiki tulikokusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu Wafanya biashara wa Zanzibar. Unajua Wafanyabiashara wa Zanzibar wana tatizo kubwa la unyanyasaji; kwa mfano, anatoka na biashara yake Zanzibar, ameshailipia kodi anakuja nayo Dar es Salaam, ikiwa anatumia bandari au *airport*, akifika pale anadaiwa kodi nyingine mara ya pili. Akisema mimi risiti ninazo na nimeshalipa, anaambiwa hapana ile tunaichukulia kama ni karatasi tu, tunataka ulipe tena hapa ndiyo tutajua kama umelipa.

Hata Waheshimiwa Wabunge, wanakuja na magari yao, wakipita pale wanajua mimi nilishapata mkopo wangu, nilishanunua gari langu, litanisaidia kuendea Dodoma; analipitisha bandarini, anaambiwa hili gari haliwezi kupita halijalipiwa, inabidi alipie tena. Ukiuliza tatizo nini? Unaambiwa *harmonisation* ambayo katika miaka tisini tulifanya utaratibu kuzuia bandari za vichochoroni. Zanzibar ni bandari ya uchochoroni siyo *official*? Sasa vitu kama hivyo ni tatizo, itabidi tuviangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninajua mazungumzo haya yamekuwa ya muda mrefu, lakini kutoka 1990 mpaka leo, hakuna kilichofanikiwa. Ninajua Waheshimiwa mnalijua na mtaliangalia kwa jicho la huruma ili suala hili liweze kutekelezeka muweze kuisaidia Zanzibar katika *tax base* yake isibomoke inyanyuke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni Masuala ya Manunuzi. Unajua pesa za Serikali nyingi zinapotea katika manunuzi na watu wanatajirika kwa sababu asilimia 70 ya pesa za Serikali zinaingia kwa wajanja. Wanapokuwa wanakwenda kununua vitu vya Serikali, ambavyo kwa kutumia pesa za matumizi ya kawaida au kutumia fedha za maendeleo, zile za maendeleo ndiyo zinachakachuliwa kabisa, kwa sababu mtu anayefanya lile jambo anatumia taratibu na sheria; na utakuta sheria na taratibu hazimbani. Hii ni kwa sababu Muswada wa Manunuzi ni mwepesi, kwa sasa unahitaji marekebisho, tungeomba Muswada uje tena Bungeni hapa tusaidie hawa wenzetu kama wao wanapita huku, Serikali ina uwezo wa kubana. Sasa ningewomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, afanye mpango Muswada wa Manunuzi uje Bungeni tuujadili ili tuweze kunusuru fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile hizi Halmashauri zetu, maana pesa zinapenya sana huko; wao pia wataalamu wao wapatiwe ujuzi wa fani ya manunuzi angalau na wao wawe na mwanga wa suala hili, wajue jinsi ya kudhibiti manunuzi katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuzungumzia juu ya Manispaa ya Dodoma. Manispaa ya Dodoma inakua, hata ukiangalia wakazi wake, wapo kati ya 324,347, kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2002. Usiku kucha Mji huu utazidi kukua kwa sababu vyuo vinaongezeka na wakati hapa ndiyo Makao Makuu ya Nchi, sasa kila mmoja atapenda kuja kufanya kazi, kuja kukaa na kuja kusoma. Hivi karibuni kuna vyuo vingine vinataka kuingizwa, sasa ningeomba tuangalie miundombinu chakavu, barabara ukitembea humo mitaani haziridhishi, maji matatizo, umeme mgogoro, asubuhi unawahi kuamka umeme usije kukatika kabla hujapiga pasi kwa kukimbilia Bungeni. Sasa ningetaka suala hili pia mliangalie, wakati tumeshasema huku ndiyo Makao Makuu ya Nchi yetu; kwa nini kusing'are mtu akitoka nje anajua ninakwenda Tanzania, ninakwenda Dodoma na anajua kwamba hii Dodoma ndiyo Makao Makuu ya Tanzania? Unakuta miundombinu yote imejipanga vizuri; maji, umeme, kila kilichokuwepo pale kinavutia, Bunge letu linavutia, basi kama zinavyovutia Ofisi zetu za Bunge na huko mitaani pia kuvutie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia suala la UKIMWI. Ninashukuru Kitengo kinachohusika na masuala ya UKIMWI, kinafanya kazi nzuri na inakubalika. Sisi wenyewe tunaona hatua nzuri wanazozifanya, lakini kuna suala moja kwa wao wanalionia ni zuri na mtu ye yeyote atalionia ni zuri, lakini kidogo lina matatizo, kwa sababu kuna kitengo wanashirikiana nacho, wanakuwa wanapita kwenye vijiwe na *kit bags* hizi ambazo ndani kunakuwa na zana na kujisaidia kama bomba, kondomu na vinginevyo. Wanapita vijiweni kuwaambia vijana wetu waache kujidunga sindano kwa kutumia bomba moja ili kuzuia UKIMWI. Kwa upande wa pili, utaona kama wanaofanya kazi hii wanafanya kazi ya kusambaza UKIMWI, kwa sababu kijana ukishampa hizo zana si ndiyo unamwambia hilo jambo lifanye?

Wao kwa nia njema wanataka wapunguze, lakini vijana wetu badala ya kupunguza wao wataongeza. Sasa ningeliwaomba wapite vijiweni, wawaelimishe vijana kama watapenda vijana hawa wawasaidie, wawatafutie vifaa vya michezo kama jezi wakati wanawapa elimu, wawaletee na vifaa vya michezo ili wawaunganishe angalau waingie kwenye michezo na akili zao ziwe kwenye michezo, wapunguze makali ya lile suala wanadolifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningetaka kuzungumzia suala la Msajili wa Vyama vya Siasa. Gharama ya uchaguzi ambayo ilipitishwa mwaka 2010 ni nzuri, inasaidia, lakini ilikuwa inahitaji elimu; tena siyo elimu kwa Viongozi tu, iende mpaka chini, kwa sababu sisi tunatafuta unafuu.

Lakini utakuta rushwa inacheza humo humo. Kwa sababu nia ni njema, lakini ile nia haijapata elimu ya kutosha, utakuta ndani yake mianya ya rushwa inaangalia, na inatazama na watu wanaikodolea macho. Sasa ningeomba semina, mikutano, elimu zingeweza kutolewa kuanzia chini mpaka juu hadi tukaelewa, tukafahamu na kuelimika kwa ujumla.

Vile vile kulikuwa na suala lingine kwa Msajili wa Vyama ilikuwa siyo zuri ambalo wanatumia jengo la nyumba ya kukodi. Jengo la nyumba ya kukodi kwa Ofisi za kiserikali kwa kazi nzito kama ile tena kubwa, haipendezi. Sasa angalau Serikali ingefanya mpango ikawapa uwezo na kuwapatia jengo lao. Wapewe Ofisi ya Serikali ya kufanyia kazi na vile vile kuchukua vifaa vya uchaguzi tukaviweka kwenye maghala ya kukodi, pia siyo vizuri. Wasaidiwe wajenge Ofisi yao ya kazi, wapate na maghala yao ya kuwekea vitendea kazi vyao kwa sababu wakati mwingine mtu utaogopa. Kutumia nyumba ya kodi kama Ofisi.

SPIKA: Ahsante.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri pamoja na Mawaziri katika Ofisi yake, hotuba ambayo imeonyesha ni mambo gani Serikali yetu imetekeleza kwa mwaka wa fedha uliopita, namna gani Serikali imejipanga kutekeleza kwa mwaka wa fedha huu ambao tunaujadili sasa.

Mheshimiwa Spika, mchang'o wangu naomba ujielekeze kwanza katika ugawaji wa raslimali za nchi yetu. Natambua Ilani ya Uchaguzi ya chama chetu kilichoko madarakani ilielekeza kuona kwamba Mikoa ambayo ipo nyuma kimaendeleo Serikali itafanya kila njia ili kuweza kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikoa ambayo wetu wa Pwani ni mmojawapo katika Mikoa ambayo

iko nyuma kimaendeleo. Lakini kwa bajeti hii ambayo tunaijadili hapa, imetengewa shilingi bilioni 22 tu. Ni Mkoa ambao ni wa pili kutoka mwisho, tukiwafuatia Lindi na Singida. Sasa kwa mazingira haya kwa kweli ni ngumu sana kuona kwamba dhamira ya Serikali kama itaweza kutekelezwa. Hii inajidhihirisha kwenye sekta ambazo nitazijadili. Kwa mfano sekta ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa matokeo ya mwaka jana ya mtihani wa Kidato cha Nne, Mkoa wetu wa Pwani zaidi ya asilimia 60 ya wanafunzi waliofanya mtihani huo walifeli. Walipata *Division zero*. Lakini matokeo mabaya ya wanafunzi hao yalisababishwa na changamoto zinazotukabili, uhaba wa nyumba za walimu, changamoto ya kutokuwepo kwa maabara na pia miundombinu na uhaba mkubwa wa walimu wa sekondari zaidi ya walimu elfu moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha, tumetengewa shilingi bilioni mbili tu ambazo ni sawa sawa na tulizotengenewa mwaka jana. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba asilimia 60 ya wanafunzi hawa waliofeli na kwa kuwa Mkoa wa Pwani mpaka sasa hatuna Chuo cha VETA, ndiyo kwanza kinajengwa, hatuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Vyuo tulivyokuwa navyo vya wananchi vina hali mbaya. Sasa tunajiuliza, wanafunzi hawa asilimia 60 tunawapeleka wapi.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati tunatafakari namna gani wanafunzi hawa waliofeli tutawawezesha vipi kiajira, ukiangalia Sekta ya Kilimo, kwa mwaka huu wa fedha imetengewa shilingi bilioni 1.2 ukilinganisha na mwaka jana ambapo ilitengewa shilingi bilioni 2.3. Ndiyo hapo tunapojiuliza, hivi ni kweli Mkoa wetu umepiga hatua za kimaendeleo kufanya bajeti ya mwaka huu kupungua kwenye Sekta ya Kilimo, ambayo sekta hiyo inatoa ajira kwa vijana, kwa watu wazima na akinamama?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atazame sekta hii imekuwaje. Lakini pia ukiangalia Sekta ya Uvuvi kwa ujumla wake mwaka jana ilitengewa bajeti ya shilingi bilioni nane. Mwaka huu imetengewa shilingi bilioni nne na Mkoa wetu wa Pwani ni mmoja wa wadau wa Sekta hii ya Uvuvi. (*Makofi*)

Mzee wangu hapa, Mheshimiwa Hamad Rashid alieleza kabisa ni namna gani Sekta ya Uvuvi inaweza ikachangia maendeleo kwa Taifa kuititia pato linalopatikana kwenye sekta hiyo. Sasa unaangalia kabisa kama ni shilingi bilioni nne tu kutoka kwenye shilingi bilioni nane za mwaka jana kwa nchi nzima: Je, vijana hawa ambao kwa kweli wamefeli, kuajiriwa kwenye Sekta ya Kilimo itashindikana, uvuvi nao utashindikana.

Mheshimiwa Spika, tungeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie, lakini sambamba na hilo, kwenye upande wa afya, pia kiwango tulichotengewa ni kama mwaka jana. Lakini kwa Mkoa wetu mzima una hospitali nane. Tuna Vituo vya Afya 20 na tuna sera, kila Kata kitajengwa Kituo cha Afya. Kila Kijiji kitajengwa Zahanati. Tuna zahanati 235 kati ya zaidi ya vijiji 500. Tuna Vituo vya Afya 20 kati ya Kata zaidi ya 100 na kwa bajeti hii ambayo imepitishwa kama ile ya mwaka jana, tuna mashaka namna gani Mkoa wetu utapiga hatua katika kuona afya ya akina mama, watoto na kwa wananchi kwa

ujumla inaboreshwani. Ni kwa namna gani mwaka huu wa fedha Serikali imejipanga ili kuweza kuboresha afya za Wanapwani.

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia pia katika sekta hiyo ya afya kwenye Halmashauri katika kifungu cha *Health Sector Development Grant* hakuna pesa yoyote iliyotengwa. Labda tutapata majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini sambamba na hilo, kuna kifungu cha *Child Survival and Development* hakikupangiwa pesa yoyote. Sasa unajiliza: Je, afya ya mtoto wa Pwani katika bajeti hii imeangaliwa kwa mazingira gani? Kwa kuzingatia changamoto tulizokuwa nazo, kuna uhaba zaidi ya watumishi wa afya 1,000. Tuna miundombinu chakavu, tuna Kata ambazo zipo kwenye Visiwa na siyo rahisi kufikika na madhara yake ni kwamba Vituo vingi vya Afya, Zahanati nyingi Mkoa wetu wa Pwani zinahudumiwa na wahudumu wa afya badala ya wataalam wa Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba tunaomba Mikoa iliyoko pembezoni na tuliokuwa nyuma kimaendeleo tuangaliwe. Mimi siamini kama mithali ya wazee wa zamani inavyosema mwenye nacho huongezwa. Anaongezwa, lakini na sisi pia tusionacho tufikiriwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Halmashauri zetu za Mitaa. Yanasemwa mengi sana juu ya ubadhirusi mkubwa, lakini mimi ninaamini kupotea njia ndiyo kujua njia. Ninaamini matatizo ya Halmashauri katika matumizi ya pesa yanaweza yakatatuliwa tukijua tatizo la msingi ni nini na tukijua ni namna gani mifumo iliyopo inavyochangia Halmashauri zetu kufanya matumizi mabaya ya pesa za Serikali ndio hapo tutakapoweza kutatua au kupunguza matatizo ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, basi naomba niipongeze Serikali. Nitofautiane na wenzangu niseme kwamba Serikali imeliona. Kwa mfano, matatizo ya mishahara hewa. Mwaka jana tu shilingi bilioni 1.8 zimelipwa kwa watumishi waliokufa au watumishi hewa. Lakini Serikali imejipanga, imeanzisha mifumo mpya wa uingizaji wa kumbukumbu za watumishi. Kwa sasa Halmashauri husika itaingiza kumbukumbu hizo za watumishi walioajiriwa, tarehe gani wameajiriwa.

Kwa hiyo, naamini Serikali imeliona. Sasa tukiendelea kuilaumu Serikali wakatiimeona hilo na kwamba imejipanga, nadhani siyo sawasawa. Tuipe moyo, kulaumu tulaumu na tuipe moyo Serikali. Lakini pia Serikali imeona kwamba tatizo kubwa kwenye Halmashauri zetu ni wingi wa *accounts*. Kukiwa na akaunti nyingi sana, hela zinahamishwa zinakwenda huku, zinakwenda huku, Serikali imeamua kwa makusudi kuzipunguza kuanzia tarehe 1 Julai, akaunti kwenye Halmashauri zinabaki sita tu. Kwa hiyo, ni hatua mojawapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali kwa kuona kuna matatizo makubwa ya Halmashauri yanayochangiwa na uwezo mdogo wa Wakaguzi wa Ndani ambavyo kwa vyovyote vile, kwa kuwa wapo pale mwaka mzima siku 365 wanaangalia zile hesabu, wanapaswa kupunguza matatizo na kwa kuwa walikuwa wanaripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi ikaonekana kuna *conflict of interest*. Serikali imeanzisha

Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na imeshamteua. Nachukua fursa hii kumpongeza Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Ndani na kumtakia kheri katika mafanikio yake. Lakini siyo hilo tu, Serikali imejipanga katika uboreshaji wa mapato ya Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, nadhani tuiunge mkono Serikali, tukemee Halmashaueri zinazofanya ubadhirifu, wachukue hatua, au walioiba mishahara, ni jambo rahisi mno, wala halihitaji Tume. Mtu ambaye ana wajibu wa kuona kwamba mtumishi huyu amekufa, ni lazima nimtoe kwenye *pay roll*, asisubiri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, asisubiri Wizara ya Fedha, yupo pale Afisa Utumishi anayehusika na Mhasibu pia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia upande wa mapato, tunaamini Serikali Kuu inapeleka pesa za maendeleo. Lakini Serikali za Mitaa nazo zina wajibu wa kukusanya mapato. Tumeona kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lengo la kukusanya mapato halifikiwi. Lakini hata yale yanayokusanywa kuititia utaratibu wa mawakala hayawasilishwi kwenye Halmashauri husika. Lakini niiombe Serikali izisaidie Serikali za Mitaa juu ya namna gani ya kubinafsisha vyanzo vya mapato. Tatizo kubwa linalojitokeza ni namna mikataba inavyoingiwa ya ukusanyaji mapato ambayo kwa upande mmoja inasababisha Halmashauri nyingi mapato yanayokusanywa kubaki kwa mawakala. Kwa hiyo, Serikali kuititia tafiti mbalimbali ilizofanya kuititia Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hasa Kituo cha Ubungo na Halmashauri ambazo zimefanyiwa ukaguzi maalum watumie ripoti zile na mapendekezo kuona ni namna gani wanaweza wakazisaidia hizi Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa suala la miundombinu. Nimalizie pia kwa kuishuru Serikali kwamba yapo mambo mengi yamefanywa. Haya niliyozungumza ni changamoto na ninaamini kabisa kwamba Serikali hii ni sikivu, lakini kwa suala la miundombinu nichangie kilomita 60 zilizobaki ya barabara ya Ndunu-Somanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo maneno mengi yanazungumzwa na sisi tulipita hizi siku za karibuni tunaona mkandarasi ameweka madaraja. Barabara kwa kweli karibu inakamilika, bado tu uwekaji wa lami. Lakini tunasikia na wananchi wanasesma kwamba mkandarasi yule anakwamishwa, halipwi kwa wakati. Sasa namna muda unavyokwenda, barabara ilikuwa ikabidhiwe mwaka jana. Namna muda unavyokwenda, ni wazi inaweza ikatokea hata *variation order*, Mkandarasi akaomba *variation* tukalipa pesa nyingi. Kwa hiyo, niiombe Serikali kuititia bajeti ya mwaka huu kama kweli mkandarasi yule ambaye anamalizia kilometra 60 amefanya kazi. Anastahili kulipwa kwa wakati, alipwe ili amalize ili na sisi watumiaji wa barabara ile na ile ndoto ya Serikali ya kutaka mtu aweze kutoka na *taxi* kutoka Mtwara mpaka Mwanza itimie ndani ya mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, naiomba Serikali kwenye pesa za maendeleo ipeleke kwenye Halmashauri kwa wakati. Tatizo lingine linalosababishwa na kutokukamilika kwa miradi kwa wakati ni pesa hizi za maendeleo kwenda karibu na mwisho wa mwaka. Kwa mfano, ripoti ya mwaka 2009/2011 ya Mdhibiti inasema shilingi bilioni 175 hazijatumika. Lakini sababu kubwa, pesa zile zinafika mwisho wa

mwaka na zinapofika mwisho wa mwaka, ipo hatari pia ya kutotumiwa vizuri. Kwa hiyo, niiombe Serikali yetu kwa kweli ilitazame hilo, na endapo inatoka kwamba wale wafadhili wetu wanaotaka kutusaidia watachelewesha hizo pesa, basi taarifa ifike mapema ili mipango ile iweze kuhuishwa na kipindi kingine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini naiomba sana Serikali itusaidie, Mkoa wa Pwani tuna changamoto nyingi. Naomba viwanda vidogo vidogo. Kuna maeneo tunalima matunda mfano, Kiwangwa na maeneo ya Rufiji, Mkuranga, tupatiwe hivyo viwanda na nishati, na naunga mkono vipaumbele vyote vya bajeti vya mwaka huu. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Huyu kabla hajakuwa Mbunge, alikuwa Mkaguzi kwenye Ofisi ya CAG. Kwa hiyo, anasema siyo kwa kubabaisha. Kwa uhakika kabisa! Hongera sana.

Sasa namwita anayefuata Mheshimiwa Kheri Ameir, na atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mheshimiwa James Lembeli ajiandae.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, naanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mmoja katika wachangiaji katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini nianzie kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Matemwe Unguja, kwa kunichagua na kuniamini kwa kipindi cha tatu sasa hivi kuingia Bungeni. Nawashukuru kwa hilo. Lakini niwashukuru vile vile timu iliyonifanya kazi ya kampeni, na kuishukuru Kamati ya Ufundı tuliyokwenda nayo pamoja katika uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naanza moja kwa moja kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini nianzie kwa kuwanasihi ndugu zangu tuliomo humu ndani kama viongozi nasaha za jambo la mwanzo katika nchi yetu kufikiria suala la usalama na amani katika nchi yetu. Hii najiunga na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na naomba kunakili aliyyoyasema katika ukurasa wa 64.

Anasema: “Ukumbuke kwamba sisi sote ni Watanzania. Nawasihi Watanzania wenzangu tuendelee na utaifa wetu na tuishi na kufanya kazi kwa amani, tuweke maslahi ya Taifa mbele, mengine tuweke nyuma.”

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka kutaja mambo mawili, matatu. Wakati fulani ulipotembelea Kamati zetu, ulikuja na salaam ukasema ulipokuwa umetoka Liberia pamoja na Sierra Leone ulipewa salamu na vijana wetu wanaofanya kazi kule, ukaambiwa tupelekee salamu zetu kwa Watanzania. Katika yote wanayoyafanya wasichezee suala la amani na ukatuambia ulisikitishwa sana na hali uliyoikuta kule. Kuna wale waliokuwa wanaambiwa wakati fulani wa machafuko: unataka shati mikono mirefu? Kabla hujasema ndiyo au siyo, unakatwa kiganja, maana yake mirefu hiyo. Lakini ukisema mirefu hujakaa vizuri ukasema mifupi, unakatwa kiganja hapa cha mkono. Haya tulikusikia Mheshimiwa Spika, ulipokuwa unatembelea Kamati mbalimbali ukatuasa.

SPIKA: Kweli kabisa. (*Makofi*)

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jamani yote twendeni. Lakini jambo la muhimu katika nchi hii tusichezee amani. Mipango mingi tumepanga, tuna *vision 2020 - 2025*. Tuna mipango ya *vision* mwaka 2012/2015. Hakuna kitakachotendeka hata kimoja kama amani haipo. Sisi katika hali hii tuliyonayo kama ni viongozi, tukumbuke jambo moja, kwamba tunabeba jukumu kubwa la nchi hii na watu waliokuwa nyuma yetu. Kuna viziwi, kuna viwete, kuna wazee kwa maana vikongwe, kuna watoto wadogo. Kuchezea kwetu kwa amani sisi tunabeba jukumu la wale wote ukiacha wanyama na viumbe vingine hai katika dunia hii. Sisi sote ni mashahidi na tunaelewa kilichotokea Burundi, Somalia na nchi jirani Uganda na nchi nyingine katika Afrika.

Mheshimiwa Spika, naungana na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kauli yako ulipokuwa umetembelea nchi za wenzetu, kwamba amani ni kitu cha kwanza kabisa katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, narejea tena kusema kwamba sisi sote ni Watanzania, amani haichagui Chama, amani haichagui dini, amani haichagui kabisa! Hapa hatungekuwepo kama amani haipo. Hakuna kilimo, hakuna elimu, hakuna biashara na hata nyumbani bibi na bwana watakuwa hawajuan kama hakuna amani. (*Makofi*)

Nakubaliana na usemi wa wale wanaosema tugombane, lakini tusupigane, tukae kusuluuhisha mambo yetu kwa kutumia vikao na sio kutumia rungu, maandamano na mengine njiani. Naona rafiki yangu pale ananiangalia. Muda mrefu tulikuwa pamoja mimi na yeye Mheshimiwa Mwenyekiti wa *CHADEMA*, muda mrefu amekuwepo na mimi, *ideology* yake mimi namkumbuka siku za nyuma, ni mtu mzuri, sijui kitu gani kilichombadilisha. Mheshimiwa naomba tuendelee na mkakati wako ule ule wa nyuma, nchi hii inakutegemea sana, nchi hii inatutegemea sote kama viongozi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna vipaumbele vitano vilivyowekwa. Mimi ningeomba Bunge hili liwe na kipaumbele kingine cha sita na hicho cha sita kiwe ndio cha mwanzo. Cha mwanzo kisiwe Kilimo Kwanza au Nishati, nasema tuazimie sote kuwa na kipaumbele cha kwanza, amani Tanzania. Tatalima tukiwa tuna amani, tutasoma tukiwa tuna amani, tutafuga tukiwa tuna amani. Kilimo ni uti wa mgongo katika nchi hii. Mawasiliano ni jambo ambalo linatulazimu tulishikie bango.

Mheshimiwa Spika, sijui kama Wabunge wanayo taarifa kwamba Zanzibar wanaagiza mchele kutoka India! Ni rahisi zaidi mchele kuagiza kutoka India kuliko kuagiza kutoka Shinyanga. Ni rahisi zaidi mchele kutoka Pakistani kuliko kutoka Mbeya. Haya ni kwa sababu ya mawasiliano ya barabara, mawasiliano ya treni, na ananikumbusha hapa ndugu yangu, inaitwa miundombinu. Kwa hiyo, tukimudu hilo, basi tutakuwa tumesaidia sana Tanzania na kuna uwezekano mkubwa sana wa chakula kuwa rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikwenda Kyela - Mbeya wakati fulani, tumekuta mkungu wa ndizi unauzwa Sh. 1,000/=, una chane 12. Lakini ukienda Dar es Salaam hapa au Dodoma unakuta ndizi moja Sh. 250=/. Tumekwenda Kilwa, unakuta samaki mtungo mmoja, mtungo kama ile kamba nyingi inayofungwa inauzwa 2,500=/. Ukienda Dar es Salaam samaki yule yule anauzwa Sh. 20,000/= ama Sh. 30,000=/. Ili twende na kusaidia ndugu zetu au kusaidia Tanzania, basi suala la miundombinu nalo liwe katika daraja la kwanza la kusaidiwa, yaliyobakia, chakula kitajiingiza ndani ya masoko chenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sana, nilitaka kusisitiza sana katika suala la amani kuliko mengine yote. Naunga hoja mkono, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini napaswa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Vijijini kwa kuniwezesha kunipa kura za ushindi zilizonifikisha katika Bunge hili Tukufu. Lakini nitakuwa sio mwingi wa shukrani kama sitawashukuru kwa dhati viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi, kuanzia ngazi ya Matawi, Wilaya, Mkoa hadi Taifa, kwa kusimamia Chama cha Mapinduzi kiweze kuongoza Serikali ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia Serikali kwa uadilifu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kuunga mkono hoja ya hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu ambayo kaiwasilisha. Naamini bajeti iliyowasilishwa imegusa kila aina na karibu kwa maisha yote ya Mtanzania wa Tanzania hii. Tuna changamoto mbalimbali katika maeneo yetu, hasa Mmikoa iliyosahaulika ya Rukwa, Kigoma na Tabora. Mikoa hii ilisahaulika kwa muda mrefu sana. Nianze tu kwa kuishukuru Serikali kwa kutupa au kutuwezesha kuandaa miundombinu hasa ya barabara, reli na usafiri wa anga kwa maana ya kutujengea uwanja pale mjini Mpanda na reli, kutuhakikisha katika kipindi chote ambacho reli zilifungwa, maeneo mengine kama sisi Mpanda, tulikuwa tunapata huduma ya reli. Hivyo, napaswa kuishukuru Serikali katika hayo walijotufanyia wananchi wa Mpanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini bado tuna changamoto kubwa sana hasa ya miundombinu. Serikali imefanya jitihada za dhati kuanza kujenga barabara ya Tunduma mpaka Sumbawanga kwa kiwango cha lami. Lakini bado kuna barabara inajengwa kutoka Sumbawanga kuja mpanda. Barabara hii ujenzi wake unakwenda kwa kusuasua. Naiomba Serikali ielekeze nguvu sana katika kuhakikisha barabara hii inaimarishwa na kukamilika kwa wakati. Kukamilika kwa barabara hizi kutafungua milango hasa kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Katavi, wanaotegemea shughuli kuu za kilimo.

Mheshimiwa Spika, lakini bado tuna barabara ambazo hazijaingizwa katika mpango maalum, hasa barabara ya kutoka Mpanda kwenda Kasulu, mpaka Mkoa wa Kigoma. Barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Mpanda na wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Barabara hii ikifunguliwa, ikajengwa kwa kiwango cha lami, itawasaidia wananchi wa Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Rukwa au Mkoa wa Katavi. Wataendelea kimaendeleo kwa sababu Mikoa hii inazalisha mazao, lakini tatizo kubwa ni

miundombinu michafu. Niihimize Serikali kuhakikisha barabara hii inapewa kipaumbele cha aina yake inavyopaswa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunayo barabara nyingine ya kutoka Mpanda kupitia Sikonge, kwenda Mkoa wa Tabora, barabara hii kwa sasa inapitika, lakini tulikuwa tunaiomba Serikali nayo iwekwe katika mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii itakapokuwa imekamilika, itawafanya wananchi wa Mpanda wawe na mawasiliano ya karibu na Mkoa wa Tabora. Niihimize sasa Serikali katika hili liweze kutekelezwa kwa muda unaotakiwa. Lakini bado tuna changamoto ya reli. Reli hii ni ya muda mrefu, ina uchakavu na bado mabehewa wanayotumia wananchi hayaridhishi.

Nitoe tu shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi - Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba, kwa kufanya jitihada za dhati kuzitembelea reli za Mkoa wa Kigoma, Mpanda na kufika katika maeneo ya eneo la bandari inapojengwa kule Kalema na kushuhudia uwanja wa ndege wa mpanda unavyojengwa. Lakini jitihada hizi tunaomba zizidishwe ili kuhakikisha uwanja ule unakamilika kwa muda muafaka na kuhakikisha maeneo ya bandari ile ya Kalema inakamilika na kuhakikisha wananchi wanaofanya kazi katika ile bandari, hasa vibarua, wanalipwa malipo yao kwa muda na wakati sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa ili uendelee unahitaji nishati ya umeme na umeme huo tunaomba uelekezwe vijijini. Tuna maeneo ambayo ni ya muhimu sana katika shughuli za uzalishaji. Maeneo hayo yako kule katika ukanda wa Ziwa Tanganyika. Kunahitajika umeme ambaio utawasaidia wananchi katika eneo hilo. Umeme ukifika eneo la Ziwa Tanganyika utawavuta wawekezaji. Kuna wawekezaji walipatikana kutoka nchi ya Norway, wanahitaji kuja kuwekeza katika Ziwa Tanganyika, kwa maana ya shughuli za uvuvi, lakini kikwazo kikubwa ni huduma ya umeme. Naiomba Serikali, ifanye jitihada za kuhakikisha inaandaa miundombinu ya umeme, uletwe katika maeneo hayo ili uweze kuwasaidia wananchi wa eneo hilo. Wananchi wa Ziwa Tanganyika ni wananchi masikini, lakini wana eneo na vyanzo vizuri vya mapato, wakitumia rasilimali ya Ziwa Tanganyika, ambalo lina samaki wengi, wakubwa, wazuri na dagaa wazuri ambaio wana thamani kubwa na wanaopendwa katika nchi hii, dagaa wanaotoka Ziwa Tanganyika. Tukiwawezesha hawa wavuvi wadogo wadogo, wataweza kujikwamua katika shughuli zao za kuendeleza Taifa hili na kuongeza kipato chao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na uboreshaji huu, tunahitaji barabara ya Mpanda kwenda Ziwa Tanganyika nayo iwe imekamilishwa vizuri kwa maana ya Mpanda – Ikora – Kalema. Barabara hii ikikamilika na tukapelekewa umeme katika maeneo haya, nina imani wananchi wa eneo hili watabadili maisha yao na watakuwa na uchumi mzuri sana. Lakini tuna barabara nyingine ambayo inahitajika ipewe huduma nzuri na ya kutosha ni barabara ya Mpanda – Mwese. Barabara hii ni muhimu sana, lakini nasikitika barabara hii hata kupishana magari mawili ni taabu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iipanue barabara ya Mpanda – Mwese na isiishie pale Mwese tu, tunaomba barabara hii ishuke mpaka kule Ziwani, ikutane na barabara inayotoka Kigoma ili wananchi hawa wawe na mawasiliano mazuri

yatakayoendesa shughuli zao. Kuna mazao muhimu kama kahawa na mazao ya migomba ambayo yapo pale ambayo yakipata miundombinu mizuri tutakuwa tumeimarisha na kuwasaidia Watanzania ambao uchumi wao ni mdogo sana katika eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto kubwa sana katika Mkoa wa Rukwa hasa vijiji. Vijiji vingi havina maji, wanaishi katika maisha ya kusuasua na kwa kudra ya Mwenyezi Mungu tu. Kuna baadhi ya vijiji toka uhuru hawajapata huduma ya maji yanayotokana na huduma ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Serikali kuptitia Ofisi ya Waziri Mkuu, hasa Mawaziri wanaofanya shughuli chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, wamsadie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu ni vigumu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa maombi, lakini wao wana nafasi sana. Pindi watakapofanya ziara katika maeneo ya eneo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, mengine mtakwenda kuyaona ninyi wenyewe, na mkiyaona mtakuwa na nafasi ya kumsaidia. Sio lazima aombe! Kuna maeneo ambayo yana matatizo makubwa sana katika Tarafa. Tarafa ya Mpimbwe, Inyonga, Mwese, Kabungu na maeneo mengine, yana matatizo ya maji. Tunaomba sana mpeleke huduma katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwaongezee mishahara walimu. Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, sambamba na majengo wanayoishi na wanayofanya kazi. Zipo shule nyingine hazijapata hata huduma zile za *MMEM*, tukichukulia mfano wa shule ya Mwese, yaani ukifika maeneo yale utasikitika watoto wanasoma katika mazingira haya na mwalimu anafanya kazi hapa. Naiomba sana Serikali ichukue uzito wa aina yake kuhakikisha inawasaidia wananchi katika maeneo ambayo yalisaulika kama ya Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali itusaidie sana kuimarisha huduma za afya katika Wilaya ya Mpanda. Wilaya ya Mpanda ina hospitali moja na ina Vituo vya Afya nane, jumla viro tisa pamoja na cha binafsi. Lakini tuna zahanati zisizopungua 31. Zahanati hizi hazina waganga, hospitali ya Wilaya haina waganga na mbaya zaidi ni hata wale ambao Halmashauri ya Wilaya iliwaombea kuongezewa Mkataba wa muda hawajapewa nafasi ili waweze kutusaidia wananchi wa Wilaya ya Mpanda. Nawaomba sana, angalau katika hatua za mwanzo, muwape mikataba wale watumishi waliokuwa wamemaliza muda wao ili waweze kusaidia kutoa huduma katika maeneo ya Mpanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la kilimo. Kilimo kila siku kinahubiriwa hapa kwamba ni Kilimo Kwanza. Lakini bahati mbaya hakijapewa msukumo mzuri na Serikali. Naishukuru Serikali kwa namna moja au nyingine kwa kuelekeza nguvu hapo, lakini bado tuna changamoto. Kwanza, Serikali inapotoa ruzuku, pembejeo zile haziwafikii wakulima waliolengwa, badala yake zinaishia mikononi mwa watendaji. Karibu mbolea zote zinazotolewa na ruzuku ya Serikali asilimia 60 inakwenda nje ya nchi na karibu asilimia kubwa ya mbolea zinazotoka Mkoa wa Rukwa zinaishia katika

nchi jirani ya Burundi. Wale wanaokutwa na matatizo, wakikamatwa, Serikali haiwachukulii hatua za dhati. Naomba mwadhibiti au tubadilishe mfumo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iviangalie vyama vyaya ushirika, vипитие huko na ninaamini zitawafikia walengwa kuliko ilivyo sasa tunatunisha mifuko ya watendaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii adimu nami nitoe mchango kuhusiana na hoja iliyopo mbele yetu. Napenda pia kuanza na kuwapongeza wote waliota hotuba. Vile vile nmpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo iko wazi, pamoja na kwamba sikubaliani na baadhi ya mambo ambayo yamesemwa, lakini ni hotuba nzito na nampongeza.

Nampongeza pia mtoa hotuba ya pili, Waziri wa Nchi, TAMISEMI - Mheshimiwa Mkuchika. Nampongeza kipekee Mheshimiwa Freeman Mbwe - Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake ambayo inatoa mwelekeo wa kuchangia kwa yale ambayo Serikali labda haikuyaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia katika maeneo matatu, labda kama nitakuwa na muda zaidi nitaongezea. Eneo la kwanza ni elimu, na ninaposema elimu nina maana ya Elimu ya Shule Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ufundu, Vyuo vingine ambavyo viko chini ya *NACTE* na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamechangia kuhusu changamoto ambazo zinakabili mfumo wetu wa elimu. Mimi binafsi kwa kweli najua kwamba nchi yetu imepata mafanikio mbalimbali katika uwanja huu, hata baadhi yetu hapa ni matokeo ya hayo mafanikio. Baada ya kusema hilo, natambua pia kwamba tunakabiliwa na changamoto kubwa sana na Wabunge hapa wamethibitisha hilo kwa kuonyesha upungufu mbalimbali uliopo katika Sekta yetu ya Elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi yoyote ambayo imeendelea na sijaiona nchi ambayo imeendelea bila kutoa kipaumbele namba moja kwa elimu. Katika bajeti yetu, tumeorodhesha vipaumbele vyetu, tumeviona, kwa kweli vyote ni muhimu na uteuzi wa vipaumbele hivyo ulikuwa sahihi kwa kiasi kikubwa. Lakini nilishangaa kuona elimu katika ule mfuatano wa vipaumbele, imepewa nafasi nadhani ya mwisho. Mimi nimeangalia bajeti za nchi mbalimbali hata huko Marekani, kuhusu elimu wana bajeti ya Serikali Kuu na Serikali za Majimbo (*state*), ukijumlisha bajeti zote hizo utakuta kwamba elimu kwa kweli inapata nafasi ya kwanza, namba moja.

Ukiangalia China ambayo imetolewa mfano wa mafanikio mbalimbali hapa Bungeni elimu ni kipaumbele namba moja, Cuba ambao wamekuwa marafiki zetu kwa muda mrefu na ambao baadhi ya mambo yao tumeyaiga kwao, walikuwa hapa wakisaidia katika Sekta ya Afya, toka mwanzo mpaka leo wao elimu ni kipaumbele namba moja. Sisi hapa Tanzania kwa kuzingatia changamoto zinazotukabili, ukiangalia Shule za

Msingi, majengo, ukubwa wa madarasa, nyumba za walimu, maabara, majengo ya maktaba, maslahi duni ya walimu changamoto hizo kwenye sekondari matatizo ni kama hayo hayo, kwenye vyuo viko chini ya *NACTE*, matatizo ni kama hayo hayo.

Kwenye Vyuo Vikuu mimi nimekuwa nikifundisha Vyuo Vikuu kwa muda mrefu na najua changamoto zilizopo madarasa, ni makubwa ajabu! Vile kwamba hakuna darasa ambalo linatosheleza kwa wanafunzi wa somo lolote labda kwa yale madarasa madogo madogo tu, lakini kwa yale madarasa ya kawaida hakuna jengo linalotosheleza. Hizo zote ni changamoto na nimetaja chache tu ambazo zinatukabili. Lakini sisi hatujatambua kwamba tunapaswa kuipa elimu kipaumbele namba moja. Kwa hiyo, napendekeza kupitia Bunge letu hili Tukufu, tuanze kufikiria upya mfumo wetu wa elimu, tulifanye hili suala zito ambalo linapaswa kuangaliwa upya. Naomba Waziri Mkuu alichukue hilo, alifikirie. Siyo lazima waanze mwaka huu, lakini waanze taratibu kujipanga upya ili elimu ipate uzito unaostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulivyoanza mwanzoni, Baba yetu wa Taifa alitambua hilo ndiyo maana bajeti za zamani elimu ilikuwa inapata kipaumbele namba moja, bila hivyo haya maendeleo ambayo tumeyapata, hawa akina Prof. Kahigi, kina Mheshimiwa Mizengo Pinda hapa Waziri Mkuu na wengine hata huyu Mwanasheria Mkuu wa Serikali wasingesoma, hawa watu wa vijijini hawa, wazazi wao hawakuwa na uwezo wa kuwasomesha. Kwa hiyo, naomba tujipange upya, tuanze kufikiria upya hii sekta nzima ya elimu, tunaweza kuanza labda kwa kuunda jopo la wataalam au Tume kama tulivyofanya kuhusiana na masuala ya ardhi, kwa mfano; au masuala ya madini kwa sababu tusipofanya hivyo na kujipanga upya, tutapitwa na kila nchi hapa Afrika Mashariki. Kenya wameshaanza kutoa Elimu ya Sekondari bure. Naomba tujipange upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo kwa hilo, lakini ni kwamba naomba tu hiyo iwe chachu ili suala hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la maslahi kwa watumishi. Maslahi ya watumishi ni duni sana siyo tu kwa walimu wala kwa manesi, bali kwa jumla watumishi karibu wote isipokuwa wale ambao wanafanya maamuzi ya kila mmoja wetu. Wengine wote maslahi yao ni duni isipokuwa wale wa juu ambao wanajipangia marupurupu yao na posho zao na kadhalika, lakini wengine wote maslahi yao ni duni. Naomba suala hilo liangaliwe. Naomba utaratibu wa mishahara na posho na kila kitu ambacho kinahusiana na maslahi kwa watumishi kiangaliwe upya, kifumuliwe kabisa kama ilivyopendekezwa katika mpango wa miaka mitano. Mishahara ipangwe upya, walimu wapate mishahara mizuri, Madiwani na wao wapate mishahara, waingizwe katika utumishi. Mafao ya uzeeni ambayo yanapangwa na hizi *PPF*, *NSSF* na *PSPF* yote yawekwe pamoja katika mfuko mmoja ili kila mtu apate kitu ambacho hakitofautiani na mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la kusikitisha ambalo limekuwa likitokea hapa nchini ambayo inabidi nilisemee hapa. Kuna mfumo unaitwa *SSSS* ambao uliwhusu watumishi waliokuwa kwenye mfumo wa Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki. Naomba

nitangaze maslahi, mimi nilikuwa mmojawao hao watu. Hao watumishi kwa kweli hawakutendewa haki. Wanapata tu malipo ya mkupuo, baada ya kupata hayo malipo ambayo ni madogo, ni chini ya hata malipo ya nesi, wakishapata hayo, ile pensheni ya kila mwezi hawapati. Maprofesa wa Vyuo Vikuu, Muhibili wengine walikuwa kwenye utaratibu huo, Serikali imekuwa ikiambiwa juu ya hili, lakini inavuta miguu. Juzi juzi tu ndiyo tunesikia kwamba eti wamesema wale ambao hawajastaafu kuanzia Machi ndiyo watawekwa kwenye utaratibu wa *PPF*.

Mimi nasema kwamba hiyo ni dhuluma. Kuna watumishi ambao wametumikia nchi hii kwa muda mrefu sana, miaka 30 na kitu, wanalipwa tu kiasi kidogo. Kuna maprofesa, Prof. Kibambo, Prof. Mkude, Prof. Kanywanyi na watu wengi tu ambao walikuwa kwenye utaratibu huo ambao walipata tu kile kiasi kidogo tu, fedha ndogo tu na hawapati ile pensheni za kila mwezi. Naomba Waziri aliangalie hili. Najua kwamba mwaka jana alikaa na Viongozi wa Vyama vya Vyuo Vikuu, lakini hakulisuluhiha, baadaye uamuzi uliofikiwa na Serikali ukamshangaza kila mtu. Watu wamefanya kazi hapa kwa uzalendo, kwa miaka zaidi ya 30 halafu wanapata tu malipo kidogo ya mkupuo halafu wananyimwa *pension* kila mwezi. Hii haikubaliki! Hamwezi kuwa na ubaguzi wa namna hiyo halafu mnakuja hapa mnasema Serikali hii inatenda haki na kadhalika. Watu hawatawaamini kwa sababu matendo yenu ndiyo yanayoamua misimamo yenu ni nini. Naomba hili suala liangaliwe upya, watu kule kwenye Vyuo Vikuu wanashubiri jibu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee maeneo ambayo yamesahaulika. Mara nyingi wanazungumzia Rukwa, Kigoma na Tabora, lakini hawazungumzii Bukombe. Bukombe hakuna umeme, hakuna maji, hakuna malambo, hakuna majosho, miundombinu ni mibovu. Kuna vijiji ambavyo havifikiki, wakati mwingine mimi nilikuwa natembea kwa miguu au baiskeli kuvifikia hivyo vijiji, mimi mwenyewe ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kufika huko kwenye hivyo vijiji ambavyo havifikiki. Naomba changamoto hizi Serikali ione namna ya kuzishughulikia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Prof. Kahigi, sasa namwita Mheshimiwa Diana Chilolo, halafu Mheshimiwa Haji Khatib Kai, halafu Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na TAMISEMI. Kabla sijaanza kutoa mchango wangu, nashindwa kujizua kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa uteuzi wako kwa kuwa Spika na siyo hivyo tu, kwa uwezo wa juu uliouonyesha kwa kuongoza Bunge hili. Nataka nikuthibitishie kwamba wanawake wenzio tunajivuna kwa uwezo mkubwa uliouonyesha wa kushika mhimili mmojawapo katika mihimili mitatu ya Serikali yetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya ponezi hizo, namshukuru Mwenyezi Mungu na nawapongeza wanawake wa Singida kwa jinsi ambavyo wanadirudisha siku zote

Bungeni. Kwa heshima kubwa, nataka niwaahidi kwamba sitawaangusha, mwendo wangu ni ule ule kuhakikisha Singida inapaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwashukuru wanawake walionileta hapa, sasa nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi vizuri. Mko wa Singida umefunguka, zamani safari ya Dar es Salaam, Singida ilikuwa ni wiki, Mheshimiwa Majaliwa ni shahidi, kulikuwa na vikwazo vingi njiani, lakini leo tunatembea Dar es Salaam - Singida masaa manane. Haya ni mambo ya kujivunia katika Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake yote, mpiganaji Mkuchika, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Nangu, Mheshimiwa William Lukuvi - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, pamoja na Manaibu Mawaziri machachari – Mheshimiwa Mwanri na Mheshimiwa Majaliwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba amepewa timu nzuri na siyo kwa viongozi hao tu, hata Watendaji. Tunamwamini kabisa ndugu Lyimo - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na kijana Hussein Katanga - Katibu Mkuu TAMISEMI. Kwa wapiganaji hawa, nina hakika kabisa Ofisi ya Waziri Mkuu inatembea, haijasimama. Namtakia kila kheri Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoto wa mkulima kwa uwezo wake wa juu anaouonyesha katika kuendesha shughuli za Serikali ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi nawashukuru Wabunge wote waliochangia. Ninaamini michango ya Wabunge wote kwamba ni mizuri na kweli kama Serikali inataka kufanya kazi ikitumia mawazo ya Wabunge, tutakimbia na siyo kutembea tena. Baada ya pongezi hizi, sasa nataka nijikite kuchangia maeneo machache ambayo yananisibu sana.

Mheshimiwa Spika, la kwanza wewe ni shahidi, nimeshauliza swalii la walimu wastaifu walioajiriwa kwa mkatiba, wanaodai mishahara yao ya miezi 16 mara nne ndani ya Bunge hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi, Mawaziri wenye dhamana ni mashahidi, wengine hawamo Bungeni humu. Mheshimiwa Mwantumu alikuwa anajibu vizuri, kila niliposimama nilipewa maneno matamu yenye faraja ajabu, kwamba ni kweli wale walimu wanadai na wanastahili kulipwa, lakini mpaka hivi ninavyozungumza walimu hao wastaifu nane, ambao wawili wameshatangulia mbele ya haki mpaka leo bado hawajapata haki zao. Mishahara ya miezi 16! Kulikoni? Walimu hao wana matatizo gani? Nimeongea Kiswahili chote cha Singida nimekimaliza, sijui nitumie lugha gani leo!

WABUNGE FULANI: Kibena.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, leo hii kilio changu nakipeleka kwa Msemaji Mkuu wa Serikali. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hatima ya walimu hawa ifike, tunataka wafe wote? Ilikuwa upembuzi umekamilika, wakasema, waliofariki wanahitaji watu wa kusimamia mirathi wakaletewa. Tatizo liko wapi ndugu zangu watendaji? Wahurumieni hao wazee.

Mheshimiwa Majaliwa amepewa hicho kitengo, ametoka Singida na hao wazee anawafahamu wote na adha wanayoipata anaifahamu. Ndugu yangu Majaliwa wahurumie hao wazee! Uliniambia mwezi wa nne sitauliza tena, lakini haikutekelezeka mpaka tumefika kwenye bajeti. Naomba basi kilio hiki kiwe cha mwisho, nisiongee tena hili. Walimu hawa wana haki zao za msingi ndugu zangu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hicho kilio change, naomba nizungumzie juu ya maendeleo ya Mkoa wa Singida. Singida chini ya Uongozi wa Dkt. Nkone, tunajenga hospitali ya Rufaa ambayo inajengwa kwa kiwango cha juu kweli kweli. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi, kashafika. Mheshimiwa Mkuchika juzi alikuwa huko, tumemtembeza, hospitali nzuri na ninahakika hospitali ya rufaa itasaidia Mikoa mingi ya jirani pamoja na wananchi wa Mkoa wa Singida.

Vilevile naishukukuru Serikali kwa sababu mwaka jana tulipewa shilingi bilioni mbili na mwaka huu tumetengewa shilingi bilioni mbili, lakini hospitali hiyo ina vitengo vingi, *unit 37*. Kama tutaendelea na utaratibu wa kutenga shilingi bilioni mbili ina maana hospitali hiyo itajengwa siyo chini ya miaka thelathini na zaidi. Sasa itakamilika leo?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uongozi wa Mkoa umeonyesha juhudhi na vifaa tumevitafuta na tumevipata, Mkuu wa Mkoa ameshaleta na wananchi wanachangia juhudhi zao. Naiomba Serikali yenye kuwapenda Watanzania wake iongeze hela kidogo tu. Kiwango kikiongezeka miaka ya ukamilishaji kujenga hospitali ya rufaa itapungua, lakini kama tutakwenda kwa mwendo huo, kweli hospitali itatumia miaka mingi kujengwa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, namfahamu huruma yake na aliona jitihada za wana Singida. Nina hakika ombi hili ambalo nimelitoa kwa niaba ya wana Singida atalisikiliza na atalifanyia kazi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu ujenzi wa *rest house* Singida ambayo itatumika kwa ajili ya viongozi wakuu wanapokuwa Singida. Imeshajengwa tayari na imefikia hatua nzuri, lakini bado haijakamilika. Tunajisikia vibaya sana wageni wa kitaifa wanapokuja, Mkuu wa Mkoa anahama. Hii hamahama, atahama mpaka lini? Madhali ujenzi huu unakwenda vizuri, mwaka huu hamjatutengea hata senti tano! Hiyo mimi nasamehe. Lakini mwaka jana kuna hela zetu ambazo zilikuwa ndani ya bajeti itakayokwisha tarehe 30 Juni, 2011, shilingi milioni 87, tunaomba basi kwani ahadi ni deni, tupewe hizo shilingi milioni 87 ili tuweze kukamilisha nyumba ya wageni wa kitaifa ambayo ina kiwango cha juu mpaka *gym* ipo humo ndani. Wageni wetu wakifanya ziara jioni watafanya mazoezi. Nawaomba sana, kwani ahadi ni deni, kwa sababu ilishaingia kwenye hesabu za mwaka jana kwamba ni mgawo wetu, tupewe kwa sababu ni stahili yetu. Naomba sana.

Mheshimiwa Spika, naiongelea habari ya Wabunge wa Viti Maalum na Madiwani. Nakushukuru sana hapa Bungeni Wabunge wa Viti Maalum tuna haki sawa na Wabunge wa Majimbo au Wabunge wanaume. Lakini nashangaa huko Mikoani na kwenye Halmashauri mbona kuna matabaka? Ukiulizauliza unaambiwa matabaka hayo yanatoka Wizarani, ni maelekezo. Mbunge wa Viti Maalum kwenye *RCC* anaambiwa kwenye *Road Board* wanaotakiwa ni wawili. Katika Mkoa unakuta Wabunge wa Viti

Maalum labda ni wanne. Kwa Madiwani kwenye Halmashauri hawaruhusiwi kuingia kwenye Kamati ya Fedha. Hayo matabaka huko yanatoka wapi?

Mimi naiomba Serikali na namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atuondolee haya matabaka. Wabunge wote ni sawa na Madiwani wote ni sawa, tena Wabunge wa Viti Maalum wana uwezo mzuri wa kutoa mawazo na siyo kutoa mawazo tu, pia ni wahudhuriaji wazuri wa vikao. Mnapoteza wachangiaji wazuri ambao wangeweza kusaidia kutoa mawazo ya maendeleo. Naomba sana hizo sheria ndogo ndogo Waziri Mkuu aziondoe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hilo na mimi niongelee kuhusu posho za Madiwani. Hili limezungumzwa sana humu ndani. Ukiona linaongelewa sana maana yake lina adha kubwa. Waheshimiwa Madiwani hawa, licha ya kutowatendea haki na kuwafanya washindwe kuchangia miradi ya maendeleo, pia tunawapa vishawishi. Tukumbuke wanasmamia mabilioni ya pesa kwenye Halmashauri zetu, watasimamiae wakati wao wana njaa? Hivi kweli unampa mtu mamilioni ya pesa kuzisimamia wakati ye ye hana kitu mfukoni? Hivi akishawishiwa na mtendaji pale wanapoangalia *value for money* kuangalia mradi wa maendeleo wakipindisha na wakipitisha mradi ambao kiwango chake siyo kizuri, mtamlamu vipi? Si anaweza akapewa hata bahasha jamani! Kwa nini tunawapeleka Madiwani kubaya? Naomba tuwaangalie, wanawenza wakashawishika vitu ambavyo siyo stahili yao kwa sababu ya umaskini. Ninawaomba sana mtakapopitisha bajeti hii, mtamke lolote kuhusu Madiwani, mtakuwa mmewakonga nafsi zao na watafanya kazi kwa moyo mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo, naomba nizungumzie kuhusu habari ya wajasiriamali akina mama. Mkoa wa Singida, wanawake wanajitahidi sana kuondokana na umaskini kama wanawake wa Mikoa mingine. Lakini kinachowakwaza ni fedha. Ukienda benki ni matatizo, ukienda Halmashauri 10% ni matatizo, sasa kapatikana mwanamke mkombozi Singida, Meneja wa *SIDO* wa Mkoa wa Singida ni Mama mahiri kweli kweli, anafanya kazi yake vizuri. Anawawezesha akina mama, anafanya semina mbalimbali za kuwakomboa akina mama, lakini Meneja huyu anakabiliwa na ufinyu wa bajeti.

Kama mwanamke kaonyesha uwezo wa juu, kwa nini msimpe vitendea kazi? Mpeni huyu Meneja vitendea kazi ili aweze kuwakwamua wanawake wa Mkoa wa Singida. Nina hakika mwanamke huyu tukimwezesha kwa fedha, akinamama wajasiriamali wa Singida watafanya kazi zao vizuri, wataachana na habari hii ya kuombaomba kwa akina baba. Unajua akina baba tunawazidishia mizigo mingine ambayo tunaweza tukaibeba wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu takwimu. Bajeti nzuri ni ile ambayo ina takwimu nzuri. Ninapata wasiwasi, watendaji wetu takwimu wanazotoa za uzalishaji wanakisia tu hawaendi vijijini kukusanya. Sasa watendaji watoke ofisini.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, nashukuru. Mheshimiwa Haji Khatib Kai.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru. Kipekee, naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Micheweni kwa kuniwezesha kunipa kura kwa wingi kabisa na kuweza kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Nawaambia wananchi wa Jimbo la Micheweni kwamba niko pamoja nao na ninawaahidi kwamba yote niliyoahidi katika kampeni, basi wawe na moyo wa subira, nitakuwa mwenye kuyatekeleza yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kutoa shukurani kwa familia yangu, na ninamwomba mke wangu naamini sasa hivi ananisikiliza na ananiona kwenye TV, basi nakuomba uwe mwenye subira, kwani niko kwenye majukumu. Endelea kukaa na familia vizuri na mimi baada ya mwezi mmoja, tutakuwa pamoja. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi sana kwa ndugu zetu na majirani zetu wa CHADEMA kwa kitendo kizuri walichokionyesha kule Mjini Arusha kukubali kufanya muafaka na CCM na kuunda Serikali ya mseto, na hii naamini kwamba wamekopi kutoka kule Zanzibar. Hii haina maana kwamba wao CHADEMA ni CCM 'C'. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye maeneo matatu, lakini nitaanza na kilimo. Serikali ya awamu ya nne imetangaza Sera ya Kilimo kama ni sekta iliyopewa kipaumbele kupitia kaulimbiu yake ya Kilimo Kwanza. Lakini bado bajeti ya Wizara hii haionyeshi umuhimu kwa vitendo kutokana na fedha zilizotengwa ili kukabili mapinduzi ya kijani.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Sekta ya Kilimo ultarajija kufikia 5.5%, Watanzania wengi walipata matumani makubwa baada ya kutangazwa kwa sera ya kilimo kuwa sasa wataondokana na matatizo mengi ambayo yamewakabili katika kujiandolea umaskini kupitia Sekta ya Kilimo. Pamoja na umuhimu ambao Sekta ya Kilimo imepewa lakini mchango wa Sekta ya Kilimo katika pato la Taifa linatarajija kupungua kutoka 21% mwaka 2010 hadi kufikia 18.7% mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapotangaza mipango mbalimbali yenyе kuleta matumaini kwa wananchi, ni lazima tuwe makini kuisimamia ili wananchi waone kweli Serikali ipo kuwasaidia na kuwaondolea kero na siyo kufanya siasa.

Mheshimiwa Spika, kama nchi iliyodhamiria kilimo kuwa ndiyo sekta ya kuongeza pato la Taifa na hivyo kupunguza umaskini kwa wananchi walio wengi, tulitegemea mipango na mikakati ya Serikali hii itaonekana kwa ukuaji mkubwa wa sekta hii, lakini matokeo yake tunaambiwa tatarajie kushuka kwa mchango wa Sekta ya Kilimo katika pato la Taifa. Hii ni dhihaka kubwa.

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 17 Juni, 2011 kwenye taarifa ya habari ilielezwa kuwa Wizara ya Kilimo na Chakula imetenga shilingi bilioni 40 za kufanya ufafiti wa kilimo, wakati tunashindwa kuwa na mipango madhubuti ya kuwawezesha wakulima wanufaika na kilimo ili kuondokana na umaskini. Sisi tunaelekeza nguvu zetu katika masuala mengine ambayo hayana lengo la moja kwa moja kumkomboa, bado wakulima wanatumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye elimu. Sekta ya Elimu kama vile ilivyo kilimo, ni sekta iliyotarajiwa kutimiza matarajio mengi ya Watanzania. Serikali imetangaza kutoa vitabu vya Kiada na Ziada kwa wanafunzi wa Shule za Msingi ili kuwapunguzia wananchi wanyonge wa Taifa hili mzigo wa kununua vitabu hivyo.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010 inaonyesha kuwa hadi kufikia Desemba, 2010 Shule nyingi za Msingi zimepokea fedha zisizozidi Sh. 60,000/= hadi Sh. 30,000/= kazi hiyo kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu wananchi wetu hawana uwezo wa kununua vitabu, lakini jambo la kushangaza 40% ya ruzuku maalum inayotolewa na Serikali kwa lengo hili na kuboresha elimu ni lazima tujiulize kiasi hiki kingine cha fedha zinazotolewa zinakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, kama fedha hizi za umma zinatengwa kwa ajili ya shughuli hizi, lakini bado tunazungumzia tatizo kwa ukubwa ule ule kila siku. Hii siyo ya kuipuuzia, ni lazima tufikirie upya ili kuwajengea imani wananchi kuwa kweli tupo Serikalini kuwapunguzia kero na siyo vinginevyo. Ni vyema tukawa na usimamizi mzuri wa raslimali za umma.

Mheshimiwa Spika, wakati tunafikiria nini cha kufanya kwa ajili ya watu wetu, siku zote ni muhimu sana kuelewa mpango huu unamlenga nani na atanufaika vipi. Watanzania walio wengi ni maskini na walio wengi wako vijijini karibu 80%, wengi wao tunashindwa kuwapatia elimu inayostahili ili kuwawezesha kuzikabili changamoto za dunia ya sasa.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, viongozi wetu wa vijiji, vitongoji na Kata nao ni wenye taaluma duni, watu amba tulitarajia ndiyo watakaowaonyesha njia...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, usisome. Sisi tunakuona unasoma.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Muungano. Tanzania ni Jamhuri ya Muungano ambayo iliundwa na mataifa mawili yaliyopata uhuru mwaka 1964 yakiwa na lengo la kuunda Taifa moja ambalo litasimamia maendeleo mbalimbali ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, tukishindwa kutekeleza hilo, tutafikia mahali ambapo tutashindwa na kuwaambia wananchi wa Taifa hili. Baya zaidi, endapo hatutaona

umuhimu wa kutatua kero hizi za Muungano, basi tutashindwa cha kuwaambia wananchi wetu na baya zaidi ni kwamba kila siku Watanzania au Wazanzibar ndio ambao tunanung'unika zaidi kwa kero hizi.

Mheshimiwa Spika, kila wakati wa Bunge zinazungumzwa kero za Muungano, lakini Serikali hakuna hata siku moja ambayo imetuambia ni kero ngapi ambazo mpaka sasa zimetatuliwa.

Mheshimiwa Spika, wakati mwagine Wazanzibar wanانung'unika zaidi kuliko Watanzania Bara. Wazanzibar imefika mahali ambapo hawana imani na Muungano huu kwa sababu wao ndiyo walio nyuma katika maendeleo, lakini ikiangalia Tanzania inasonga mbele. Kwa hiyo, tunachokisema na tunachokiomba ikiwa Serikali hii imeona kwamba Zanzibar imekuwa kikwazo ama imekuwa kero, basi ni vyema kama Zanzibar imekuwa mzigo, basi mtuache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa na ninajiuliza kila siku, kila siku tunazungumzia kero na kila siku tunaambiwa kwamba Kamati imeundwa, lakini hatujui Kamati hii imeundwa wapi? Kwa hiyo, narudia tena kusema kwamba ikiwa Zanzibar imekuwa mzigo na imekuwa kero, basi teremsheni kichwani ili muwe huru, la sivyo, basi afadhali Muungano huu uvunjwe halafu uundwe tena endapo itawezekana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Katiba si inakuja? Mtaiongea vizuri. Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo karibu. Halafu kufuatana na tulivyobana orodha sasa hivi ya kuzungumza kwamba hataingia mtu ambaye hayupo kwenye orodha hii, na kama kuna mtu anataka kuingia itabidi abadilishane na mwenzake.

Sasa kwa misingi hiyo, Mheshimiwa James D. Lembeli nafasi yake itakuja kuzungumzwa tarehe 29 Juni, 2011, Mheshimiwa Sussan Lyimo anachukua nafasi ya Lembeli kwa sababu wanakwenda kufanya semina ile ya miaka 10 ya Bunge la Afrika Mashariki. Nimewateua mwenyewe. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo nitamwomba Mheshimiwa Sussan A. J. Lyimo afuate halafu na Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli ajiandae.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kupata nafasi hii ya kuzungumza katika Bunge lako hili Tukufu. Lakini vile vile nina wajibu wa kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Mgogoni kwa kunipa ridhaa yao ya kuweza kuwawakilisha katika Bunge hili. La pili, nakishukuru Chama changu kwa kuweza kunituea kuja kuwawakilisha Watanzania wenzangu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vilevile nina wajibu wa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba, pamoja na Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar – Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa juhudi kubwa walizozichukua

juu ya kuweza kukaa kwenye meza wakaweza kufanya mazungumzo na leo wakaifikisha Zanzibar katika mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile sina budi kumpongeza Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman Mbewe kwa kuona kwamba maamuzi waliyoyafanya viongozi wa *CUF* juu ya kukaa meza moja na CCM mpaka ukawea kupatikana mwafaka wa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Zanzibar na wao leo wamefikia hatua hiyo kwa kuunda Serikali ya umoja pale katika Mkoa wa Arusha. Mimi nathubutu kusema kwamba bado CHADEMA ni wapinzani, siyo CCM ‘C’. Kama ambavyo *CUF* ni wapinzani katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano na CHADEMA vilevile ni wapinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niangalie sehemu moja hii ya fedha za maendeleo ambazo zimeletwa majimboni. Sheria hii mimi sijaipata kuhusiana na namna fedha zile zinavyotumika. Lakini nimepata taarifa kwamba fedha zile baada ya mwezi mmoja zinarudi Hazina. Sasa ikiwa hivi ndivyo na Wabunge ndio wahusika wakuu wa kwenda kutoa mipango juu ya matumizi ya fedha zile, na leo wako katika Bunge lako hili na watakuwepo hapa kwa karibu miezi miwili, sasa tunataka utaratibu gani utumike juu ya fedha zile zilizopelekwa majimboni? (*Makofi*)

Kwa sababu Wabunge ni wahusika kwa fedha zile na ni Wenyeviti katika matumizi ya fedha zile. Naomba kutengwe kanuni ili fedha zile Wabunge wafike waone ni namna gani zitawenza kutumika. Vinginevyo, baadhi ya Halmashauri watazitumia vibaya fedha zile.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la Muungano. Napenda ninukuu kifungu cha 16 ukurasa wa tisa Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema: “Muungano wetu umetimiza miaka 47 yenye maendeleo katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Maendeleo haya yananufaisha wananchi kwa kuwapa fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli zao katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vikao vya Makatibu Wakuu na Mawaziri wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vilifanyika ili kujadili masuala mbalimbali ya Muungano.

Katika mwaka 2011/2012 Serikali itaendelea kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano. Aidha, Serikali itatoa elimu kwa umma na kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kwa kuhakikisha kwamba Sekta, Wizara na Asasi zisizo za Muungano zinakutana mara kwa mara.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ina Wizara 26. Hivi karibuni nilipata jibu la swali langu kuambiwa kuwa Wizara za Muungano ni sita. Ina maana mambo yote ambayo siyo ya Muungano yanapangiwa bajeti ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuangalie, kutakuwa na usawa gani katika Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar? Licha ya kwamba haya ambayo siyo ya Muungano yamesemwa katika Katiba, kutakuwa na usawa gani katika Muungano wa Tanganyika na

Zanzibar kama Wizara za Muungano ni sita, zile zisizokuwa za Muungano ni 20 na bajeti ni moja?

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano kweli ina nia ya dhati ya kutatua kero ambazo zimo ndani ya Muungano, basi ninaamini mapendekezo ya *JFC* yangelifuatwa kama yalivyo, lakini hayakufuatwa. Kwa hiyo, siamini kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*SMT*) ina nia ya dhati ya kutatua matatizo au kero zilizomo kwenye Muungano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kujenga imani ya dhati kwa Wazanzibari, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulisimamie hili ili liweze kutatuliwa na kupatiwa ufumbuzi. Tunaamini kwamba vikao vinakaliwa, Waziri wa Mambo ya Muungano anatoka Zanzibar, ni kweli kwamba Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano anatoka Zanzibar, ni kweli kwamba Mtendaji Mkuu, Makamu wa Pili wa Rais anatoka Zanzibar na hawa ni wanakamati, lakini tujiulize: Hivi, mawazo yao na mapendekezo yao yamezingatiwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, nina amini kwamba hakuna ukweli wa dhati wa kutatuliwa masuala haya. Mimi niseme kwamba, mmewafikisha mahali Wazanzibari wanaona kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano inawadhalilisha. Kuna Wanajeshi, Polisi na wafanyakazi wengine Zanzibar ambao wanatumia huduma Zanzibar, lakini hawalipi kodi kwa SMZ, kodi zao zote zinaelekezwa SMT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano imekuwa ni Juja Majuja kwa Wazanzibari. Imefanya kwamba Zanzibar haina haki wala uwezo wa kuweza kupewa nafasi ya kuitumikia Tanzania nje. Tuangalie mabalozi waliopo, Zanzibar ina mabalozi wanne (4) tu na hawa wote hupangwa katika nchi za Kiarabu, nchi za Kiislam isipokuwa Mheshimiwa Mapuri, labda kapelekwa China. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwamba Wazanzibari na wao wana haki katika Muungano huu, wana uwezo katika Muungano huu na wana haki ya kupewa baadhi ya wafanyakazi kufanya kazi katika ofisi za Kibalozi.

Mheshimiwa Spika, kuna Kamati ambazo huundwa mara kwa mara, eti kuangalia kero za Muungano. Kuna Kamati ya Nyalali imepita, ikaja na mapendekezo yake, lakini mpaka leo hatujui wapi yamekwenda. Kuna Kamati ya Shellukindo, ripoti yake mpaka leo haijatolewa. Kuna ripoti ya Amina Salum Ali, mpaka leo haijatolewa. Tuamini kama kuna Kamati ambayo itaweza kukaa kutatua kero za Muungano?

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba katika hili...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji kwisha*)

SPIKA: Haya, tunashukuru, ahsante.

MHE. KOMBO HAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, ya kwanza hiyo.

SPIKA: Ya pili hiyo. Tunashukuru. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe taarifa kidogo juu ya hoja hii ya fedha hizi za *CDF*. Waheshimiwa Wabunge wengi wamemfuata Waziri wa Fedha, wamenifuata na mimi na ni kweli kwamba baadhi ya Wakurugenzi wanawaita huko, waache Bunge waende kusimamia hizo fedha! Lakini taarifa zilizopo ni kwamba fedha hizi ni za maendeleo, hazitarudi Hazina. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tumekubaliana na Waziri wa Fedha na wenzetu wa TAMISEMI kuhakikisha kwamba wale Wenyeviti wenyewe uwezo wa kuzitumia sasa hivi kwa maelekezo yaliyopo wazitumie, maana fedha hizi zinasimamiwa chini ya Sheria Maalum iliyotungwa na Bunge lako na Wenyeviti ni Wabunge wa Majimbo. Kwa hiyo, kama mna maelekezo, zitumieni kwa sababu fedha zote za bajeti ya mwaka huu zimeshakamilika na zimeshatumwa majimboni, kote Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, nilitaka nitoe taarifa kuhusu hilo kwamba fedha hizi hazitarudi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha atasimamia hilo. (*Makofi*)

SPIKA: Nimemruhusu atoe taarifa sasa hivi kwa sababu Wabunge wengi walikuwa wanaomba ruhusa kwenda majimboni wakashughulikie hizo hela, tena ingekuwa ni *rush* kwa sababu ukitoka hapa unakwenda kushughulikiae hiyo siku ya kesho? Kwa hiyo, ndiyo maana nimemruhusu aseme kwa sababu wengi walikuwa wanaomba ruhusa kwenda huko. Ni fedha za maendeleo, hazirejeshwi hazina *by tarehe 30 Juni*, mztumie kwa mpango mzuri kwa sababu zitakaguliwa fedha zile. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napongeza hotuba zote zilizotolewa hususan ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ambayo imetoa mwanga na uhalisia wa hali halisi ya nchi .(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba siungi hoja mkono kwa sababu kuu tatu. Moja, ni ukubwa wa Baraza la Mawaziri ambao unaonyesha dhahiri matumizi mabaya ya fedha, lakini pili, uonevu wa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu, na tatu, Serikali kutokuwa na dhamira ya kweli ya kuhamia Dodoma pamoja na mambo mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la ukubwa wa Baraza la Mawaziri. Suala hili tumekuwa tukilizungumza muda mrefu ndani ya Bunge, lakini mpaka leo Baraza letu la Mawaziri ni kubwa sana, baraza lenye Mawaziri 54 hii ikijumuisha

Mheshimiwa Rais ambaye ni sehemu ya Baraza, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu na Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha dhahiri na hili niliwahi kulisema na ninakumbuka hata kiongozi wa Kambi ya Upinzani katika Bunge la Tisa alisema, ukiangalia nchi za wenzetu, ninaomba ninukuu: "Shirika la Fedha Duniani, takwimu za mwaka 2010 zinaonyesha dhahiri kwamba Tanzania ni nchi ya 97 yenye *GDP* ya dola bilioni 21, lakini ina Baraza la Mawaziri 54 ukilinganisha na nchi ya Marekani ambayo ni nchi ya kwanza kwa utajiri duniani ikiwa na *GDP* ya dola trilioni 14 zaidi ya mara 1,000 ya *GDP* ya Tanzania, lakini baraza lake la Mawaziri ni 15 tu."

Mheshimiwa Spika, lakini nchi ya Japan ambayo ni ya tatu kwa utajiri yenye *GDP* ya dola trilioni tano bado ina Baraza la Mawaziri 17, wakati nchi ya Ujerumani ambayo ni ya nne kwa *GDP* ina Baraza la Mawaziri la 15 tu. Tanzania nchi ambayo ni maskini kiasi hicho, bado ina Baraza la Mawaziri kubwa sana zaidi ya mara tatu ya Marekani. Kwa hiyo, bado nasimama nikisema kwamba ni lazima Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iangalie kwa makini ukubwa huu wa Baraza la Mawaziri kwa sababu kwa kweli fedha nyingi zinaishia huko.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la pili ambalo nimezungumzia kwamba ni suala la kuhamia Dodoma. Kama ambavyo Kiongozi wa Upinzani alizungumza, ni wazi kwamba suala la kuhamia Dodoma limekuwepo toka mwaka 1976 mpaka leo ni miaka 35 sawa na miezi 420, bado hatujahamia Dodoma.

Kuna nchi nyingi ambazo zimeweza kuhamia katika Makao Makuu mengine tukichukulia mfano wa nchi kama ya Nigeria ambayo imechukua miaka michache sana na tunatambua nchi hiyo imekuwa na utawala tofauti, utawala wa kijeshi, lakini bado imeweza kutimiza azma yake. Lakini nchi kama ya Brazil, Makao yake Makuu yalikuwa *Rio De Janeiro*, ilichukua miaka mitatu na nusu tu kuweza kuhamia Brazili. Kwa hiyo, bado naona Serikali haina dhamira ya kweli na haina pia utashi wa kisiasa wa kuhamia Dodoma. Ndiyo sababu sisi tunasema kama imeshindwa iseme wazi ili kama ambavyo CHADEMA au Kambi ya Upinzani tunataka, Dodoma ibakie kuwa mji wa Elimu ili wananchi waweze kuelewa kwa sababu kusema kwamba umeshindwa wala siyo kosa. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nategemea kwamba Serikali kwa sababu imeshachukua miaka mingi na hatuoni dhamira yoyote ya kuhamia Dodoma na nalisema hili kwa sababu tuna takwimu. Kwa mfano toka mwaka 2001 mpaka leo hii ukarabati wa *State House-Ikulu Dar es Salaam* umeshagharimu shilingi bilioni 56. Kuanzia mwaka 2001 kila mwaka kuna ukarabati wa Ikulu wa zaidi ya shilingi bilioni mbili. Mwaka jana ilitengewa shilingi bilioni 7.2 na mwaka huu wameomba shilingi bilioni 10.2 ya ukarabati wa Ikulu ya Rais.

Mheshimiwa Spika, lazima tujiulize, hivi kweli ni nyumba gani ambayo inakarabatiwa kila mwaka? Kuanzia mwaka 2001, 2002, 2003 mpaka leo hii Ikulu ya Rais inaendelea kukarabatiwa na kwa fedha nyingi. Fedha hizi zisingewenza kutosha kukarabati au kuendeleza Ikulu iliyoko Chamwino ili Rais aweze kuhamia Dodoma? Ninaamini kabisa Rais akihamia Dodoma, hakuna Waziri atakayebaki Dar es Salaam. Kuna Mbunge mmoja alisema Spika ahamie Dodoma, lakini haiwezi kuwa na *impact*, Spika hata akihamia Dodoma kama Rais hayuko Dodoma haitakuwa na *impact* kwa sababu Rais na Waziri Mkuu ndio Watendaji Wakuu wa Serikali. Vilevile ukiangalia bado Waziri Mkuu anaomba aidhinishiwe fedha kwa ajili ya makazi ya Dodoma na Ofisi ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, suala la kuhamia Dodoma mimi naona bado halijapewa msukumo wa kutosha. Ifike mahali Serikali iseme tumeshindwa kuhamia Dodoma, Dodoma ibakie kuwa Mji wa Elimu au mji wa kitu kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo nielekee kwenye suala la migomo ya wanafunzi Vyuo vya Elimu ya Juu. Kumekuwa na mazungumzo mengi hapa Bungeni na tuhuma mbalimbali kwamba Viongozi na Wanasiasa wamekuwa wakisaidia sana migomo ya Vyuo vya Elimu ya Juu na tuhuma hizi mara nyingi zilikuwa zinatolewa na upande wa CCM zikielekezwa upande wa Upinzani. Naomba nieleze Bunge hili kwamba migomo katika Vyuo vya Elimu ya Juu haijaanza leo. Nitoe takwimu tu kwamba kumekuwa na migomo katika Vyuo Vikuu pamoja na maandamano kuanzia mwaka 1965 na wakati huo CHADEMA haikuwepo, CUF haikuwepo wala TLP haikuwepo.

Mheshimiwa Spika, mgomo wa pili ulikuwa mwaka 1966, wanafunzi wakipinga kuhusu kwenda Jeshi la Kujenga Taifa, CHADEMA haikuwepo wala CUF haikuwepo. Maandamano na migomo imeendelea mpaka mwaka 1990 wakati wanafunzi wakidai suala zima la uchangiaji wa gharama za elimu na mnakumbuka kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1991 kilifungwa kwa takriban mwaka mzima wakati Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi akiwa Mkuu wa Chuo kile na tutakumbuka sana alipokuwa akisema wanafunzi wamemtukana matusi ya nguoni wakati huo CHADEMA haikuwepo wala CUF haikuwepo. Kwa hiyo, hivi vijembe kwamba Vyama vya Upinzani ndio wanasaidia maandamano na migomo Vyuo Vikuu si ya kweli, ni ya uongo na mimi niseme kwamba ...

SPIKA: Mheshimiwa Susan, ukisema si ya kweli inatosha.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Ndio nataka niendelee Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Neno uongo humu Bungeni halitakiwi.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Sawa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba maandamano yalikuwepo toka enzi hizo na yataendelea kuwepo kama Serikali haitatimiza wajibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua kwamba kuna Bodi ya Mikopo na wanafunzi wenye stahili ya kupewa mikopo hiyo wanapaswa kupewa kwa wakati kwa

sababu wanafunzi hawa hawategemei fedha nyingine zozote zaidi ya mikopo wanayopewa. Sasa kama wanafunzi hao hawajapewa mikopo hiyo kwa wakati tunategemea wanafunzi hawa wale wapi, walale wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi inapotokea kwamba Kiongozi Mkuu wa Serikali amewapa wanafunzi wale ahadi, halafu ahadi hiyo haikutimizwa na anakuja mtu mwagine wa chini anatoa barua kwamba hakuna fedha, sisi tutegemee nini, wanafunzi hao wategemee kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba katika suala zima la wanafunzi, kuna sheria ambayo inaruhusu maandamano, inaruhusu migomo na inaruhusu pia uhuru wa wanafunzi kuongea. Kama Serikali inaridhia sheria hiyo, ni kwa nini wanafunzi wanapofanya maandamano ya haki kabisa wananyimwa haki yao?

Mheshimiwa Spika, niendelee na suala zima la maandamano ya CHADEMA. Kumekuwa na maneno mengi ndani ya Bunge hili kuhusu maandamano. Napenda ninukuu alichosema Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge wa Mchinga ndani ya Bunge lako la Tisa, alisema:- “*Ukiona mwanamume mtu mzima analia, jua ameshikwa pabaya.*” (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mbwe nakwambia endelea, sisi tumewashika pabaya, tutaendelea na maandamano mpaka kieleweke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi wakati Mheshimiwa John Komba Mbunge wa Mbinga alipokuwa anachangia alimwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu; “*Ukiona unasifiwa sana, jua hujafanya kitu, lakini ukiona unalalamikiwa umefanya vizuri, kamatia hapo hapo*”.

Kwa hiyo, nasema CHADEMA, Mheshimiwa Mbwe, Mheshimiwa Dr. Slaa, kamatia hapo hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie suala zima la maji. Wote tunajua maji ni uhai na bila maji hatuwezi kuishi na takwimu zinaonesha kwamba watu wengi wanaouguia magonjwa mengi hasa watoto wanakufa kutokana na maradhi yanayotokana na maji yaani *water born diseases*. Nazungumza hili kutokana na hali halisi ya maji hususan katika Wilaya ya Moshi Vijijini ninakotokea.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Tisa nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji aende akaone tatizo la maji katika Wilaya ya Moshi Vijijini na kwa kweli namshukuru sana Naibu Waziri wakati ule Mheshimiwa Chiza alikubali ombi hilo na akaenda. Jambo linalosikitisha ni kwamba alipofika, baada ya siku moja maji yalitoka katika maeneo ya Korini Kusini, maeneo ya Rau, maeneo ya Kiwaraa pamoja na Mbokomu kwa ujumla wake lakini jambo la kusikitisha baada tu ya kuondoka na mpaka hivi ninapozungumza hakuna maji kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana haya masuala ya maji ni masuala ya msingi na kimsingi katika maeneo hayo unakuta wazee ni wengi, dumu la maji linauzwa

shilingi 1,000/= na kama tunavyojuu watu wengi wanaotoka maeneo hayo wanafuga pamoja na matumizi yao ya ndani, kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, naomba sana wakati Waziri wa Maji atakapokuwa analeta hotuba yake aangalie maeneo hususan ya vijijini, suala ni kwamba kama maji yaliweza kutoka alipokuja Waziri kwa nini baadaye maji hayatoki? Kwa hiyo, inaonekana huu ulikuwa tu ni usanii na ndiyo maana maji hayakutoka tena. Kwa hiyo, tunaomba sana sehemu zenyenye matatizo ya maji yashughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nalotaka kulizungumzia ni suala la elimu. Wote tunajua elimu ni msingi, elimu ni kila kitu na hakuna nchi yoyote duniani ambayo imeendelea bila ya kuwa na elimu. Ni jambo la kusikitisha sana kuona katika vipaumbele vyetu elimu bado haijapewa kipaumbele na sisi tunaamini kabisa bila elimu hatuwezi kusonga mbele. Tunaomba Serikali pamoja na kwamba imeweke vipaumbele ambavyo vinaeleweka lakini mimi binafsi nadhani bado elimu ingepaswa kupewa kipaumbele zaidi ili vijana wetu waweze kuelimika kwa sababu mimi naamini hatuwezi kupata Wahandisi wa Maji, hatuwezi kupata Madaktari kama hatujawekeza katika elimu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nataka kuzungumzia ni suala zima la miundombinu ya barabara hususan Dar es Salaam. Wote tunatambua kwamba Jiji la Dar es Salaam au Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 70, lakini kwa hali inavyoendelea ya msongamano wa magari ni wazi kwamba hatutaweza kufikisha lengo hilo. Kwa hiyo, naomba kama ambavyo Waziri wa Ujenzi aliwahi kusema jiji lolote linavyofika zaidi ya watu 2,000,000 basi inapaswa kuwa na *flyovers* lakini hatuna...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Muda nilionao Mheshimiwa Kuruthum ni dakika 10, kama hazikutoshi basi tunasitisha shughuli. Yuko wapi Mheshimiwa Kuruthum? Zinatosha au tukuongezee?

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Hazitoshi.

SPIKA: Haya. Waheshimiwa Wabunge kutokana na hilo basi nina matangazo mawili. Kama nilivyosema, orodha yetu sasa haitakuwa inaingiliwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge unapoleta barua ya kutaka ubadilishiwe namba basi uchukue na jina la mwenzako huyo mnayebadilishana. Sababu sisi hatupendi kuambiwa kwamba Meza inachakachua majina. Kwa hiyo, ukitaka kubadilisha uzungumze na huyo mwenzako ulete majina yote, sisi tutabdalisha kama ukitaka kuzungumza kesho, kesho kutwa badilishana na mwingine kwa majina msilete barua zisizokuwa na majina.

La pili, napenda kusema pia tumeimarisha ile Idara yetu ya Habari, kwa hiyo Waandishi wa Habari, hawa Maafisa wangu watakuwa wanapita kwenu asubuhi kuuliza kama kuna swali lolote mnalotaka lishughulikiwe. Watapita saa hizi, mchana baada ya

kusitisha shughuli na watapita jioni. Kwa sababu wengi wananiandikia vibarua hapa tunaomba Muswada, tunaomba maelezo, sasa mimi nikikupa wewe nitabakia na nini hapa Mezani? Kama mnataka kuongea na mimi wenyewe mnawaambia basi nitaongea nanyi. Kwa sababu inaonekana kama nazungumza na nyie huko nje mnaandika vingine na mimi napaswa kuingia humu ndani naanza sasa kujitetea, sipendi hivyo. Kwa hiyo, watakuja mara zote, kama kuna nia ya kuongea na mimi wenyewe watanipangia na mimi nitakuja kuongea na nyie.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kueleza hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.52 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii ni Mheshimiwa Gosbert Blandes atafuatiwa na Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee sana kukushukuru kwa kunipa nafasi.

Nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa kuniamini na kunipa kura nyingi za kishindo. Wananchi wa Karagwe wanajua kutofautisha ipi ni mbivu na ipi mbichi na napenda kuwahakikishia kwamba Mbunge wao niko makini na nitachapa kazi kuliko kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikushukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunipendekeza mimi na kunateua kugombea Jimbo la Karagwe. Yapo mengi yalismwa, Karagwe maandamano yanaendelea, mimi nimesema binafsi sitishiki na maandamano ya Chama chochote. Karagwe tuko mpakani mwa Tanzania, Rwanda na Uganda. Nimeambiwa wanataka kuandamana waanzie Karagwe waende mpaka Mji wa Kigali amba o uko Rwanda lakini wananchi wa Karagwe wanajua ni nani anafaa kuwa Mbunge wa Karagwe, nani anafaa kuwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia maslahi ya Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Waheshimiwa Madiwani nchi nzima wanapokea posho ambayo haizidi shilingi 120,000/- kwa mwezi. Kusema kweli posho hii ni ndogo sana, haikidhi mahitaji hasa ukilinganisha na kazi nzuri ambayo Waheshimiwa Madiwani wanaifanya. Pia Wenyeviti wetu wa Vijiji wanapokea posho ndogo sana ambayo haitoshi kununua hata mche wa sabuni. Mimi nasema Serikali iangalie kwa makini kuwaongezea posho na mshahara Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigosie kidogo kuhusiana na kiinua mgongo wanachopokea Waheshimiwa Madiwani. Waheshimiwa Madiwani wanapokea kiinua mgongo ambacho nadhani hakifiki hata shilingi milioni nne. Ukizingatia kazi ambayo anaifanya Mheshimiwa Diwani ya miaka mitano ya kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, baada ya miaka mitano ukasema aondoke na kiinua mgongo cha shilingi milioni nne, kwa kweli ni ndogo. Napendekeza kwamba, kwa kuwa mwisho wa miaka mitano Serikali inajua Mheshimiwa Diwani atapokea shilingi ngapi, naomba na kupendekeza kwamba Serikali ianze ku-*compute* kila mwezi, fedha hizi ambazo Mheshimiwa Diwani atapokea baada ya miaka mitano ziwe zinapelekwa kwenye Taasisi zetu za fedha ikiwemo NSSF na LAPF, ziwekezwe kule ili baada ya miaka mitano Mheshimiwa Diwani aondoke na fedha yake ile ya msingi pamoja na riba ambayo itakuwa imepatikana kwenye mfuko wa LAPF au NSSF, badala ya kupokea shilingi labda milioni nne anaweza akaondoka na kitita cha shilingi milioni saba hata nane au zaidi. Hiyo nadhani itasaidia sio kwa Madiwani tu hata Waheshimiwa Wabunge, ile fedha ambayo tunapokea baada ya mwisho wa miaka mitano, ikianza kuchangisha kupelekwa kule LAPF itasaidia sana kuongeza kipato cha Waheshimiwa Wabunge na Madiwani, riba itasaidia kupandisha kiwango hicho lakini pia Serikali itaondokana na ile adha ya kutoa fedha nyingi kwa mkupuo na kuyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Karagwe, jambo nalotaka kulizungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba unipe *attention* kubwa sana. Mkoa wa Kagera uko mpakani mwa Tanzania, Rwanda na Burundi, pamoja na Uganda. Mkoa huu kwa Bahati mbaya umekuwa ukivamiwa na wahamiaji haramu ambao wanakuwa na mifugo yao na suala hili limekuwa kama tabia. Mkoa wa Kagera umekuwa kama shamba la bibi, mtu yejote anayependa kuingia, anaingia na kutoka anavyotaka, kisingizio Serikali inasema kwamba eti mpaka ule ni mkubwa sana kwa hiyo Serikali inashindwa kuulinda vizuri, kwa hiyo mtu yejote anaingia na kutoka. Sasa mimi nauliza tufanyeje sisi watu wa Kagera? Kama Serikali inashindwa kulinda mipaka vizuri mtu anaingia na kutoka anavyotaka, watu wa Kagera wafanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukiingia Mkoa wa Kagera, ukienda Karagwe, Biharamulo Muleba utakuta kuna wahamiaji chungu nzima kutoka Rwanda na Uganda mifugo imejaa kule, wale watu ni wakatili sana, wanapiga watu wetu, juzi wameua watu sita katika Wilaya ya Ngara, kijiji cha Msagamba, hao ni watu kutoka Rwanda. Naomba sana Serikali sasa ichukue hatua za makusudi tena za haraka sana kunusuru wananchi wetu wa Mkoa wa Kagera kutokana na Wahamiaji haramu kutoka hizi nchi jirani. Inasikitisha sana unapoona mtu anatokana nchi jirani anaingia, kwanza ni haramu lakini anakuwa na nguvu ya kumpiga mtu mpaka kuua na Serikali hili jambo inalifahamu kwa sababu ni la muda mrefu sana. Kinachonisikitisha, tunao viongozi hata wa Serikali pale Karagwe, kuna viongozi upande wa TAKUKURU wanawakingia kifua sana hawa wahamiaji haramu kwa kisingizio kwamba pengine ni watu wanaofanana na wenyeji wa Mkoa wa Kagera kwa sababu Wanyarwanda na watu wa Ngara wanaofanana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu uliangalie sana jambo hili linatutesa sana sisi watu wa Karagwe na Kagera kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la Pori la Akiba la Kimisi. Sisi hatuna tatizo na pori hilo, sio kwamba tunalikataa. Pori hilo limefanywa kuwa Pori la Akiba la Wanyamapori lakini napenda kusema kwamba pori hilo limekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Wilaya ya Karagwe, hasa Kata za Nyakakika, Rugu, Nyakasimbi pamoja na Kata ya Bweranya. Pori limemega maeneo ya wananchi kwa maana kwamba wananchi hawana mahali tena pa kufugia, hawana mahali pa kulima na mifugo yao sasa hivi ikifanya makosa ikaingia kwenye Pori la Akiba la Kimisi, mwananchi atazalilishwa kupita kiasi. Mifugo inakamatwa, atatozwa faini ya shilingi milioni mbili na wakati mwengine wakitozwa faini hiyo ya milioni mbili ataandikiwa risiti au stakabadhi ya shilingi laki tatu, nne au laki tano. Serikali yetu najua inajali watu wake sana na hilo sina wasiwasi nalo, naomba iangalie haraka sana uwezekano wa kusogeza mipaka hiyo. Wananchi wangu wa Karagwe wanateseka sana kutokana na pori hili. Mapendekezo yangu na tumeshaleta maombi kwa Waziri wa Maliasili angalau mipaka isogee kwa kilomita kuanzia ishirini kuingia ndani kwa sababu eneo lile ni kubwa sana ili wananchi wangu wapate makazi na sehemu ya kufugia mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusiana na Kampuni za *Ranch* za *NARCO*. Kampuni ya *Ranch* ya Taifa ambayo ilimilikisha wananchi kufugia mifugo yao katika *ranch* za Misenyi, Kagoma pamoja na Kitengule katika Mkoa wa Kagera, jambo hili lilikuwa ni zuri wala hatupingani nalo, isipokuwa nataka kusema *ranch* hizi walipewa watu bila kuzingatia mipaka ya vijiji, kuna wananchi ambao *ranch* zimetolewa zikawa zimechukua hata shule. Sasa wananchi wamekosa huduma za jamii kwa sababu wale ambao wamegawiwa *ranch* wamekuwa wakali sana, hawataki wananchi wafanye shughuli zao za kijamii ndani ya eneo hilo. Tumeshalizingumza sana humu ndani suala hili liko Muleba, liko Karagwe na liko Misenyi. Ni kero kubwa sana na jambo hili linaweza likaleta matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kule kwangu Karagwe kuna vijiji ambavyo vimemegwa, wananchi hawana mahali hata pa kufanya shughuli zao za kawaida. Kuna kijiji cha Katanda, Kihanga, Kibwera, Mshabaiguru, Mlamba na sehemu zingine, ukienda Muleba huko ndiyo usiseme, ukienda Misenyi huko ni balaa. Tunaomba sana wafugaji hawa wabaki na maeneo ya kutosha lakini pia na wananchi wamegewe maeneo ili na wenyewe waweze kufanya shughuli zao za maendeleo katika maeneo yao. Tulishaleta pendeleko hili, tumeshamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie, tunaomba sana kwa sababu wananchi wameshaanza kupandwa munkari, muda wowote lolote linaweza likatokea, niiombe Serikali isisubiri matatizo haya yakajitokeza, itusaidie kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya kutoka Kyaka mpaka Bugene. Inaendelea vizuri, naomba mkandarasi asimamie ili iweze kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme vijijini. Rais aliahidi umeme kwenda maeneo yote ya Bushangaro, Nyaishozi, Rwambaizi katika Jimbo la Karagwe lakini pia tumeahidiwa umeme wa Mrongo, kule kwenye Jimbo la Kyerwa kwa Mheshimiwa Katagira. Tunaomba Serikali iharakishe sana ili wananchi wetu waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mafuta ya taa, nashauri lile ongezeko la ushuru kutoka shilingi 52/= mpaka shilingi 400.30 kwa lita, ule ushuru ambaa utatozwa, napendekeza ziende kwenye Mfuko wa Umeme wa Vijijini ili umeme uweze kufika kwenye vijijini vyetu kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa afya, nasikitika kusema kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema matibabu kwa wazee yawe bure. Sasa hivi wazee wetu wanaadhirika, wakienda hospitali na kwenye zahanati hawapati tiba bure, wakati Ilani inasema watapewa tiba bure. Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wazee ili wapate tiba bure. Pia na wale wanaochangia shilingi 5,000/- hawapati dawa. Anaingia hospitali, anaambiwa dawa akanunue, akitoka nje anakuta dawa ziko za kutosha. Sasa kwa nini dawa hizi hazipatikani hospitalini? Tunataka dawa ziwepo hata Muhimbili na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa maji. Mkoa wa Kagera umejaliwa kuwa kandokando ya Ziwa Victoria, tuna Mto Kagera, tuna Maziwa mengine madogomadogo lakini la kushangaza kwenye Jimbo langu maji yanayopatikana ni chini ya asilimia 90 asimilia kumi ndiyo wanapata maji. Niombe sana Wizara ya Maji, Mheshimiwa Waziri Mkuu asikie kilio chetu, maji yatoke Ziwa Victoria, Mto Kagera tupate maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Karagwe inajumuisha Majimbo mawili, Kyerwa pamoja na Karagwe. Nasikitika kusema kwamba mpaka sasa hivi navyozungumza, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe haina Mkurugenzi Mtendaji, haina Afisa Utumishi, haina Mganga wa Wilaya, haina Mweka Hazina, haina Afisa Elimu. Hii itatugharimu sana katika kupata fedha za *Local Government Development Grant*. Naomba watu hawa wawepo, kuna ambaa wamekuwa waki-act kwa muda mrefu sana. Karibu mwaka mzima, sasa naomba kama watakuwa wamekidhi vigezo basi wawe-confirmed au waletwe kutoka sehemu zingine na sisi tupate watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Karagwe tunalima mahindi, maharage, karanga, njegere na kadhalika lakini mazao yetu yananunuliwa kwa debe na kwa gunia kwa kukadiria tu. Wananchi wetu wanapata matatizo, wanapunjwa sana. Tunaomba Serikali liangalie hili, mazao yanunuliwe kwa vipimo halisi ambavyo ni kilo ili waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Askari Polisi Karagwe, tunao WALIMU na watumishi wengine, mishahara yao inachelewa, kila siku wanamilalamikia. Maaskari Polisi wamehamishwa kwenda Karagwe hawajalipwa mafao yao ya uhamisho, Walimu hawajalipwa, kwa hiyo, tunawavunja moyo katika kufanya shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo barabara kutoka Chanyamisa kuja Nyaishozi mpaka Nyakange hospitali, barabara nyingine ni kutoka Gakorongo mpaka Mrongo. Barabara hizi tumeahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Kabla Serikali haijafikia huko kwa kiwango cha lami, basi angalau izibe mashimo haya ambayo yamejitokeza, yamekuwa mahandaki yanasurya sana wananchi wangu wa Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikishangaa bei ya kahawa Karagwe. Kahawa ya Karagwe ni nzuri, haitwi mbolea za chumvichumvi, bei ya kilo moja ni shilingi 1000/- lakini ukienda Kilimanjaro, Mbeya, Mbanga kilo hiyo hiyo moja ni shilingi 3,500/- mpaka shilingi 7000/-. Sijajua kwa nini wananchi wangu wa Karagwe wanaendelea kupunjwa kiasi hicho. Naomba sana bei ya kahawa iangaliwe, matokeo yake wananchi wamekasirika sana wanapeleka kahawa hiyo nchi jirani ya Uganda na sehemu nyingine ili angalau wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Benki ya Wakulima na Wafugaji ambayo imefunguliwa Dar es Salaam, dirisha dogo, sijajua ni lini itawafikia wananchi wa Jimbo la Karagwe. Naomba sana hata kama halitajengwa tawi basi angalau pale kwenye *branch* yetu ya *NMB* ya *CRDB* liwepo dirisha dogo kwa ajili ya wananchi wangu kutoka Kata mbalimbali, Kata ya Ihembe, Kata ya Rugu, Nyakasimbi na sehemu zingine ili na wao waweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama hapa nikiwa na nguvu tele jioni hii ya leo lakini pia napenda kuwashukuru au kuendelea kuwapa moyo wadau wote wa Chama cha Wananchi (*CUF*) waendelee kutuunga mkono na sisi wawakilishi wao hatujachoka, tutaendelea kuwapigania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitaanza TAMISEMI. Katika Hotuba ya Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mkuchika, ukurasa wa tisa, kipengele cha kumi na sita, ameongelea juhudzi zinazochukuliwa kwa makusudi na TAMISEMI kuhakikisha kwamba wanawachukulia hatua za kinidhamu watumishi wote ambao wanakwenda kinyume na Kanuni za Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na juhudi za Mheshimiwa Mkuchika tumeziona lakini mimi nasema kwamba katika sehemu hii TAMISEMI inatakiwa iongeze uthubutu wa hali ya juu. Waziri ametuelezea hapa kwamba kuna Wakurugenzi 16 ambao wameachishwa kazi na kupata adhabu tofautitofauti lakini tatizo la watumishi wetu katika Halmashauri zetu kuendelea kukandamiza kile kinachopelekwa kwa ajili ya wananchi wetu bado kubwa sana, mimi bado nasikitika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata bahati ya kutembelea katika Halmashauri chache katika mwaka huu lakini nilichokiona kwa kiasi kikubwa ni kwamba watumishi wengi katika Halmashauri zetu wanaendelea kuharibu lakini TAMISEMI wamekuwa wepesi sana wa kuhamisha mtumishi ambaye anaharibu Rombo kumpeleka Siha,

mtumishi anayeharibu Kilosa wanatuletea Mkuranga, Pwani, mtumishi anayeharibu Morogoro wananilettea Rufiji Wilayani kwangu. Mimi nasikitika sana kwa sababu naamini watumishi hawa ambao bado wanaendelea kuharibu na wanaendelea kutafuna pesa ambayo ilitakiwa imsaide Mtanzania mnyonge kwa kumhamisha kituo cha kazi sio kwamba umemsaidia Mtanzania mnyonge bali unaendelea kumkandamiza kwa sababu wataendelea kuwapa mafunzo wale ambao wanawakuta kwa ajili ya kuwaibia na kwa ajili ya kuendelea kufanya matumizi mabaya katika fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kidogo katika kuangalia Mkoa wetu wa Pwani. Mimi bado naenda palepale kwenye Bajeti ya mwaka 2011/2012, bado hajjalenga kabisa kumkomboa mwananchi wa Mkoa wa Pwani hasa yule mwenye hali ngumu. Kumekuwa na usemi wa kebehi, watu wengi sana wanapenda kuutumia kwamba watu wa Pwani hawapendi kusoma wanachopenda wao ni kucheza ngoma, Watu wa Pwani hawapendi kujituma ni wavivu, lakini hawaangalii watu wa Pwani hawa ni kiasi gani wamevezeshwa sasa ili waweze kusoma na kupata hiyo elimu bora? Au watu wa Pwani hawa ni kwa kiasi gani sasa wamevezeshwa ili waweze kujikwamua kiuchumi ili watu wa Pwani waonekane si wavivu. Watu wa Pwani wanapenda kusoma kama wanavyopenda kusoma watu wa Kaskazini. Mimi nasikitika sana, kwa kweli mimi nikisikia mtu anasema mtu wa Pwani hapendi kusoma, anapenda kucheza ngoma, natamani nimtie makonde, kwa kweli ananitia uchungu sana. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi nimezaliwa Pwani, nimekulia Pwani, nimesoma Pwani, Elimu ya Msingi mpaka ya Sekondari, nafahamu vizuri mazingira ya Pwani, kwa hiyo, nikimsikia mtu wa Pwani hapendi kusoma kwa kweli hii inaniuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado bajeti imeendelea kuwa ndogo kwa Mkoa wa Pwani. Mkoa ambao una changamoto nydingi za elimu, afya, kilimo na mambo yote lakini bado bajeti imeendelea kumkandamiza mtu wa Mkoa wa Pwani. Kwa kweli hii inasikitisha sana. Kwa nini nasema hivi? Mkoa wa Pwani sisi tumebarikiwa, tumepata Shule ya Sekondari ya Kibaha, shule ambayo inaongoza kwa kutoa wanafunzi wenye vipaji, lakini pia tumepata shule za watu binafsi kama Marian Girls ya Bagamoyo ambayo pia inaongoza kwa kufaulisha katika Tanzania, lakini hivi Wanarufiji ukiangalia Shule ya Kibaha ni Wandengereko wangapi ambao wametoka Kibaha wamepata fursa ya kujiunga na shule hiyo ya vipaji? Ni Wazaramo wangapi wametoka Bagamoyo ambayo wamepata fursa ya kujiunga na shule ya vipaj? Ni Wazaramo wangapi kutoka Kisarawe na Mkuranga wamepata fursa ya kujiunga na shule ya vipaji Kibaha? Hakuna! Mimi naona ni sawa na asilimia 0.0000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sasa hawaonekani mpaka leo hii? Ukienda Pwani Mheshimiwa Majaliwa anajua kuna Shule ya Msingi mpaka leo hii bado ina Mwalimu mmoja na sasa hivi ameongezeka wa pili. Wakienda kuchukua mshahara hakuna Mwalimu, hivi unategemea mtoto wa Pwani huyu anayetoka Tapita kule Rufiji atakuwa *geneus* kiasi gani kuweza kufaulu vizuri mtihani wa Darasa la Saba ili akajiunge Kibaha kwenye shule ya wenye vipaji? Kuna shule iko Kikobo Waziri anaifahamu, mpaka sasa bado ni ya tope, hivi unategemea mtoto wa Pwani anayetoka Kikobo atafanya

juhudu gani za makusudi ambazo zitamwezesha yeye kufaulu ili naye aingie kwenye shule za vipaji? Halafu unasema mtoto wa Pwani hapendi kusoma! Mtoto wa Pwani bado hajaandalisha mazingira mazuri ambayo sasa yatamwezesha na yeye kuweza kusoma aweze kufikia watu wa Kaskazini ambao wanaongelewa kwamba wanapenda kusoma na watu wa Pwani ni wavivu. Mimi nasikitika sana, Pwani tunaachwa nyuma kwa kila kitu, lakini hili bado hawaliangalii tunaendelea kukandamizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende kidogo kwenye suala la kilimo, nashukuru sana katika hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 23 wakati anaongelea *SAGCOT*, Mpango wa kukuza kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania ameigusa na Pwani, nimeshukuru kidogo. Sasa je, Pwani hii ambayo inazungumziwa hapa ni kweli ipo nia ya dhati ya kuigusa Pwani hii itoke kule tunapodhamiria kwenye kilimo cha mkono na kwenda kwenye kilimo hicho ambacho kitamwezesha mwana Pwani huyu kuzalisha mara tatu kama Hotuba ya Waziri Mkuu inavyosema? Nataka nizungumze kidogo hapa kwa sababu pamenigusa kidogo, kule Rufiji kabla ya Mkakati wa *SAGCOT* ambao sasa ninauona hapa mwaka 2011/12 na kuendelea kuna kitu kilikuwa kinaitwa RUBADA, Rufiji *Basin Development Authority*, imeundwa toka mwaka 1975 kwa tangazo la gazeti la Serikali, mimi bado sijazaliwa hata sijui kama nitazaliwa. Kazi kubwa ya RUBADA ilikuwa ni kuendeleza kilimo katika Bonde la Mto Rufiji, ukiacha na hii ya kuangalia vyanzo vya umeme na kutunza mazingira. Mwaka 1990 RUBADA ilijenga Ofisi Ikwiriri, mpaka leo nasimama hapa hata ekari kumi tu za mfano kule kwenye bonde la mto Rufiji *especially* mto Rufiji ambazo zinaonyesha RUBADA imefanya kazi kweli ya kumuinua Mwana Rufiji kutoka kwenye kilimo cha jembe la mkono kwenda kwenye kilimo cha kisasa, hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo inapoongelewa *SAGCOT* tunaambiwa kwamba RUBADA ndiyo atakuwa mtu wa kwanza kusimamia ili amtoe mkulima wa Pwani, Rufiji kutoka kwenye kilimo cha jembe la mkono na kumpeleka kwenye kilimo cha umwagiliaji. RUBADA imekuja na maneno mazuri sana kwamba mpango huu sasa hivi umetokana na ziara ya Waziri Mkuu kule Korea mwaka 2009 na kuhakikisha kwamba Rufiji nao wananaufaika na kutoka kwenye umaskini kwa kutumia sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kumtaja Waziri Mkuu lakini pia haitoshi RUBADA imetuulia na wawekezaji, kuna hawa Wakorea, kuna Marekani, kuna Waingereza, Wasingapore na wengine, tunaishukuru sana kwa majina mengi ya wawekezaji. Wamekwenda mbali zaidi kutuambia kwamba kuna viwanda ambavyo sasa vitakuwa vya usindikaji mpunga wetu ambao utalimwa katika Bonde la Mto Rufiji kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji, kwenye muhogo wetu utakaolimwa Rufiji sehemu za Magongo na kuna Mtama, tunashukuru sana lakini Rufiji tunajiuliza kwamba RUBADA hawa ambao sasa wanatakrabani miaka 35 na wameweka ofisi Rufiji takribani miaka 20 wameshindwa kuweka japo ekari kumi za mfano za kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Rufiji, leo hii ndiyo kweli ataweza kumtoa mtu wa Rufiji katika umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia haitoshi RUBADA hao wanatuambia kwamba kuna wawekezaji wa aina tatu watakaokuja kwa mpango huu wa kilimo, kuna wawekezaji

wakubwa ambao watachukua ekari elfu tano mpaka ekari elfu 25, kuna wawekezaji ambao watachukua ekari 20 mpaka ekari 500, kuna wawekezaji ambao watachukua ekari moja mpaka 10, sasa hao ndiyo wenzangu wa Rufiji. Rufiji leo wanaambiwa katika mpango ambao Waziri Mkuu ameuleta kuwatoa watu wa Rufiji katika umaskini, akachukue ekari moja hivi kweli tuna mkakati wa kumtoa mtu wa Rufiji katika umaskini kwa ekari moja? Mimi naona lengo la mpango huu siyo MKUKUTA hapa kuna MKUKUBI, tuna lengo la kumkandamiza mtu wa Rufiji zaidi atoe ardhi yake lakini bado asinufaik.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri Mkuu kwa kuwa RUBADA imemgusa moja kwa moja Waziri Mkuu kwamba ye ye ndiye hasa, kwa kutumia Wakorea amepata hiso pesa zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya mradi wa Rufiji basi afike Rufiji kuwaridhisha Wanarufiji kwamba kweli mpango huu utakuwa endelevu na siyo hadithi ya mama kuku kila siku anamwambia mtoto wake kwamba utanyonya kesho, mtanyonya kesho kutwa, mtanyonya mtondogoo kumbe hana hata nyonyo, anafanya kazi ya kuwaongopea vifaranga wake. Halafu anakuja kurithisha mpaka kizazi chake, kifaranga nacho kinakua kinaanza kuja kumwongopea kifaranga mwenzie, kwamba utanyonya kesho, kesho kutwa kumbe nyonyo hakuna. Sasa Wanarufiji wanataka kujua mkakati huu kweli utakuwa wa kuwakomboa wana Rufiji au hadithi ya mama kuku? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kwenye sekta ya afya, sekta ya afya ni sekta muhimu sana kwa sisi Watanzania, lakini Waziri Mkuu hivi inakuwaje hawa wafadhili ambao wanatuletea pesa katika sekta muhimu kama sekta ya afya, wanakuwa na masharti mengi ambayo sasa hayamkomboi Mtanzania mnyonge kupata matibabu bali yanawanufaisha watu wachache. Kwa mfano, katika sekta ya afya kuna mfuko unaoitwa *Basket Fund*, utakuta Halmashauri inapata mpaka milioni mia tano, milioni mia nne kuititia mfuko huu, lakini fedha za mfuko ule asilimia 80 mpaka 70 zinakwenda kwenye posho, kwenye matengenezo ya magari, kwenye mafuta ya magari na siyo kwenye dawa ambazo zitamnufaisha Mtanzania mnyonge ambaye yupo chini, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli hatuwezi kuongea na Wafadhili japo watufikirie sisi maskini, tunawapenda sana wafadhili, ndugu zetu, wanatusaidia katika bajeti zetu, ndugu zetu wanatusaidia kujengea zahanati zetu, lakini sasa inakuwaje hizi pesa zao wao wanazielekeza zaidi katika mambo haya? Leo unakwenda kwenye Halmashauri unakuta watumishi wapo kwenye mafunzo ya uchanjaji mbwa, kesho unakwenda wapo kwenye mafunzo ya UKIMWI, kesho kutwa unakwenda wapo kwenye mafunzo ya uzazi salama, mtondogoo unakwenda unaambiwa wanajifunza mambo ya *outreach*, watu wanaingiza posho tu lakini ukiwaliza madawa mliweka shilingi ngapi kutoka kwenye hii milioni mia tano, hakuna! Utaambiwa ooh ni mwongozo wa wahisani kwenye pesa hizi kwamba ziende kwenye mafunzo. Sasa je, tunawafundisha nini Wakuu wa Idara ambao kila siku wanapigiwa kelele kuhusu UKIMWI na wanaufahamu UKIMWI? Utashangaa mpaka *Technician* anakwenda kwenye mafunzo ya kukusanya takwimu za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, *Technician* wa barabara! Ukiniambia ni miongozo ya Wafadhili, hivi kweli hawa Wafadhili hawawezi kutusaidia sisi wanyonge tupate japo huduma muhimu kama dawa? Mtu anaenda hospitali anaenda kununua Panado lakini milioni mia tano imeingia, watu wamechukua posho tena ma-

technician wanaenda kujifunza kukusanya takwimu za watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi, inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapenda sana wafadhili lakini basi tujaribu kuwaomba na sisi ni wanyonge hizi pesa mnazotupatia ziende sehemu muhimu. Tupate dawa, tupate *delivery kits* za akina mama, ukienda Zahanati zingine hata vitanda vya kuzalia akina mama hakuna au viro vichache lakini hizi pesa zingetusaidia katika zahanati zetu tutapata *delivery kits*, kina mama wangepata vifaa vya vizuri kwa ajili ya uzazi. Leo hii akina mama wanaambiwa wakanunue *gloves*, lakini pesa ya namna hii kama ipo kwa nini akina mama wasipatiwe *gloves* hospitalini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wahisani wetu watusaidie, watuonee huruma, hizo posho zinanufaisha wachache...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli. Anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali na Mheshimiwa Moza Abedi Saidy ajiandae na baadaye Hamad Ali Hamad.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyetuwezesha kuwepo hapa tukiwa wazima wa afya. Vilevile nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba iliyowasilishwa hapa Bungeni na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alioitoa katika Bunge hili Tukufu tarehe 21 Agosti, 2008 pamoja na mambo mengine alieleza mambo kumi ambayo yana utata katika Muungano wetu. Masuala ya Muungano yanazungumzwa na yanafanyiwa utafiti. Naomba niyataje kwa mtiririko mambo ambayo Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliyazungumzia. Jambo la kwanza, mgawo wa mapato yanayotokana na misaada ya nje, misamaha na mikopo kutoka *IMF* na fadia zinazopatikana na mapato ya Benki Kuu. Pili, malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kuhusu masuala ya kodi. Tatu, utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu Zanzibar, Nne, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asili. Tano, uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu. Sita, utekezaji wa Sheria ya *Merchant shipping* katika Jamhuri ya Muungano, masuala ya uanachama wa *International Maritime Organisation*. Saba, ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za nje. Nane, ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tisa, ni suala la ajira ya watumishi kutoka Zanzibar katika taasisi za Muungano na mwisho ni utafutaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia mpango wa umwagiliaji Zanzibar kupitia mpango wa *ASDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hiyo ilifuatana na kikao cha kusaini Hati ya Makubaliano kuhusu kero za Muungano kilichofanyika Zanzibar tarehe 2 Juni, 2010

ambacho utiaji saini huo ulishuhudiwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kero za Muungano, Mheshimiwa Ali Mohammed Shein ambaye sasa ni Rais wa Zanzibar na Waziri Mkuu pia alishuhudia pamoja na aliyekuwa Waziri Kiongozi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na Mheshimiwa Ali Juma Shamhuna ambaye alikuwa ni Makamu wa Waziri Kiongozi. Hati ya Makubaliano ya utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu Zanzibar ulitiwa saini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera na Uratibu wa Bunge wakati huo Mheshimiwa Philip Marmo na Waziri Ofisi ya Rais wa Zanzibar, Katiba na Utawala Bora, Mheshimiwa Ramadhani Abdallah Shaban. Aidha, Hati ya Makubaliano ya utekelezaji wa *Merchant Shipping Act* ilitiwa saini na Mheshimiwa William Ngeleja na Waziri wa Ofisi ya Waziri Kiongozi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Machano Said. Waziri Marmo alitia saini kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria wakati huo Waziri Mathias Chikawe na Waziri Ngeleja kwa niaba ya aliyekuwa Waziri wa Miundombinu wakati huo Dkt. Shukuru Kawambwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo kumi ambayo aliyataja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ndiyo kero na utata wa Muungano, ni mambo mawili tu ambayo yalitiwa saini na kila mmoja wetu anajua, nane yako *pending*. Katika ripoti hiyo ilisema kwamba kuna mambo mbalimbali ya Muungano ambayo yameripotiwa na yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha hivi karibuni katika Baraza la Wawakilishi, Makamu wa Pili wa Rais ambaye ni Balozi Seif Idd aliliambia Baraza kwamba suala la wafanyabiashara wa Zanzibar limepatiwa ufumbuzi. Wasiwasi wangu na wasiwasi wa Watanzania ni kikao gani ambacho kilikaa au ni Kamati gani au kama kuna Kamati nyingine mpya imeundwa baada ya ile ya aliyekuwa Makamu wa Rais ya Dkt. Shein, tuambiwe au kama imefanya kazi yake usiku pia tunaweza kuambiwa. Mimi sioni kama kuna Kamati nyingine mpya iliyoundwa kushughulikia kero za Muungano kwa sababu katika ile Kamati ni mambo mawili tu ndiyo yaliyotiwa saini mbele ya Waziri Mkuu. Nakaribia kusema kwamba Makamu wa Pili wa Rais, amelipotosha Baraza la Wawakilishi kwa sababu hakulambia ukweli. Kama aliwaambia ukweli basi atuambie ni lini na mahali gani na huo utiaji wa saini ulishuhudiwa na nani kama yalivyofanyika haya mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niingie katika hoja ya pili. Rais katika mambo kumi aliyoyazungumzia moja katika kero za Muungano ni kuhusu Wafanyakazi wa kutoka Zanzibar katika taasisi za Muungano. Baadhi ya Taasisi za Muungano hazina sura ya kimuungano katika muundo wa utawala na utumishi wake. Jambo hili linasababisha kutokuwepo kwa uwiano baina ya pande zote mbili, Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama kitabu hiki cha *BOT Annual Report* ya mwaka 2009/2010, naomba nitoe ushahidi pevu wa hoja yangu, katika ukurasa wa 281, *Part Six, list of Management*, ukitazama *Executive Office*, kuna watu wanenye na Mzanzibar hapa ni mmoja na yuko pale kama *political figure. Directorate of Governance Office*, kuna watu saba, hapana Mzanzibar hata mmoja na hawa ni Mameneja na *Managing Directors*. Ukija namba mbili, *Directorate of Strategic Planning and Performance*

Review, kuna watu wane, hakuna Mzanzibar hata mmoja. Ukija namba tatu katika *Deposit Insurance Board*, pana watu watatu, hakuna Mzanzibar hata mmoja. Ukija namba nne katika *Risk Management*, kuna watu wanen hakuna Mzanzibar hata mmoja. Ukija namba tano, *Directorate of Human Resource and Management*, pana watu watano, hakuna Mzanzibar hata mmoja. Ukija namba sita, *Directorate of Banking*, pana watu watatu, hakuna Mzanzibar hata mmoja. Ukija namba saba, *Directorate of Banking and Supervision*, pana watu watano, hapana Mzanzibar hata mmoja. Ukija namba nane, *Directorate of Economic Research and Policy*, pana watu nane, hapana Mzanzibar hata mmoja. Ukija namba tisa, *Directorate of Finance*, pana watu watatu, hakuna Mzanzibar hata mmoja. Namba kumi, *Directorate of Finance and Marketing*, pana watu wane, hakuna Mzanzibar hata mmoja. Ukija namba kumi na mmoja, *Directorate of Management Information System*, pana watu wanen, hapana Mzanzibar hata mmoja na zipo kumi na sita muda unapotea, lakini katika watu 84 amba ni *Directors* na Meneja katika Benki Kuu ambayo ni taasisi ya Muungano, pana Mzanzibar mmoja, hii ndiyo hoja ya kila siku ambayo mara nyangi Wazanzibar wamekuwa wakiizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sielewi kwamba, hii ni taasisi ya Muungano au ni taaasi gani. Labda Waziri Mkuu angenieleza utaratibu gani au njia gani zinazotumika katika kuwapata Mameneja katika Benki Kuu. Namwomba Waziri Mkuu atakapokuja kufanya *winding up* basi anipe habari hii kwa sababu hata *Miss Tanzania* kupatikana kwake kunajulikana taratibu zake na watu wote wanajua *Tanzania Miss* anapatikanaje. Sembuse hiki chombo cha Muungano ambacho kinawakilisha pande zote mbili, mambo mengine tufunike kombe mwanaharamu apite. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Waziri atanisaidia, juzi Waziri wa Mambo ya Nje alipokuwa akiwasilisha *paper* yake alikuwa akionyesha kuhusu rada. Sasa sielewi vizuri labda nieleweshwe kwamba rada ni ulinzi na ulinzi ni Mambo ya Muungano, kama ni mambo ya Muungano makubaliano ya kutumia fedha, tayari fedha zilishagawiwa wala hazijapatikana zote zimeelekezwa, naomba ninukuu. Ununuzi wa vitabu milioni 4.4 kwa ajili ya wanafunzi wa shule ya msingi nchini, si suala la Muungano, kwa hiyo, Wazanzibar hawapati pamoja na ulinzi ni mambo ya Muungano. Ununuzi wa vitabu 192,000 kwa ajili ya kufundishia walimu wa shule ya msingi, shule ya msingi siyo mambo ya Muungano. Kwa hiyo, hizi fedha ukitazama zote ujengaji wa nyumba, hata zikipatikana, Zanzibar hawana faida yoyote na hizi fedha. Kwa hiyo, hata haja ya kuchangia hoja hii hakuna. Sasa nafikiri labda nieleweshwe kwamba hii raba ya ulinzi siyo mambo ya Muungano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ubaya mkubwa ikiwa fedha hizi nyangi sizizungumzi lakini kuna pesa kidogo tu, *TF* wanapata dola 400,000 kwa mwaka, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wao, wamejiunga sijui kwa idhini ya nani katika *FIFA*, Zanzibar tukitaka kujiunga tunaambiwa hamuwezi kujiunga kwa sababu tayari Tanzania wameshajiunga lakini dola 400,000 hawampi *ZFA* hata dola 50,000 hawawapi na tumekubaliana. Sasa huu ni wizi na wale ni majambazi kabisa siyo wezi, wale *TF* ni majambazi wanazungumzia wizi mdogo mdogo, wale ni majambazi kabisa. Kwa hiyo, hali kama hii ikiendelea, tunategemea watu wasilaumu Muungano wakati mambo ni mabaya hivi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua hiki kitabu cha *Annual Report ya Tanzania Revenue Authority* ukifungua nyuma kuna watu 34 katika *organization structure* lakini Mzanzibari ni mmoja tu. Hiki ni chombo cha Muungano. Sasa utakuta mambo kama haya unapokuja kuyatazama halafu usiseme watu kama wanalamika, hizi Kamati zinazoundwa zina mamlaka gani? Mfumo wa Muungano uliokuwepo Rais anawea kukataliwa Zanzibar, Wazanzibari wakamkataa lakini Rais akakubalika upande mmoja tu wa Muungano na akawa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Hata mfumo wenyelewa wa Muungano haufai. Kwa sababu tunaweza kusema hatumtaki Rais aliyesimamishwa, lakini kura nyingi ziko wapi. Kura nyingi ziko huku, kule itakuwa CCM mnatuchagulia Rais kila siku hata kama hatumtaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo yako mengi, tukianza kuyasema haya hatuyamalizi mpaka saa mbili usiku. Kwa hiyo, inabidi tuseme tu kwamba, siwezi kuunga mkono hoja mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapokuja hapa akaja akatuambia ni utaratibu gani. Siungi mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali. Sasa nitamwita Mheshimiwa Moza Abedi Saidy na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad ajiandae.

MHE. MOZA ABEDI SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia jioni hii ya leo. Awali ya yote napenda kuwashukuru viongozi wangu wa Chama hasa Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba anayeumiza kichwa chake usiku na mchana ili kuweza kutetea uchumi wa nchi ya Tanzania. (*Makofi*)

Pia, napenda kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais Zanzibar, Mheshimiwa Shariff Hamad na Viongozi wote wa Chama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache ambayo yanajiri katika nchi yetu ya Tanzania pamoja na kwamba yameongeleka lakini nitaongelea hasa suala zima la elimu. Kuna suala la elimu, afya, maji, kilimo ambayo nitaweza kugusia masuala machache kidogo kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, naomba unilinde. Kwa kuwa Wilaya ya Kondoaa ninapotoka mimi ipo katika Mkoa wa Dodoma na ndio Makao Makuu ya Nchi ya Tanzania. Wilaya hii ndio ambayo inaonekana ya kwanza kwa wanafunzi wengi kufeli mtihani ambaa ni Taifa la kesho kielimu hasa katika kufeli katika mitihani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, umepewa dhamana kubwa ya kuongoza Taifa lijalo kuwa na wasomi na siyo Taifa ambalo litakuwa na elimu ambayo kwamba ni bora elimu na si elimu bora.

Sasa Wilaya yetu ya Kondoaa inacho Chuo cha Elimu cha Bustani ambacho kinatoa *diploma* ya ualimu na *certificate* ya ualimu ya kufundishia. Walimu wengi wanaotoka katika chuo hicho hawafundishi katika Wilaya yetu ya Kondoaa, kuna uhaba

mkubwa wa walimu. Walimu imekuwa ni *source* kubwa katika Wilaya yetu, katika shule za msingi hata za Sekondari. Kwa kweli niwashukuru wananchi wa Wilaya ya Kondo ya Kondo ni wasikivu na wana amani kubwa, wameweza kuvumilia na kuweza kujitolea kujenga shule lakini shule hizi hazina nyumba za walimu, hazina maabara, zingine hazina hata choo, hazina walimu, wanalala kwenye madarasa asubuhi wanaamka ndio wanakwenda kufundisha. Wananchi hawaridhiki na Chuo hiki kielimu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa umepewa dhamana hii naomba ufile katika Wilaya hii na utembelee uweze kuona adha na matatizo makubwa yanayotokea katika Wilaya yetu ya Kondo kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kondo shule nyingi za Kata watoto hulazimiki kupanga nyumba kwani wanatoka maeneo mbalimbali na makwao na shule ni mbali, utakuta mtoto wa kike anashirikiana na mtoto wa kiume, wote wanachangia nyumba moja hii ni kuwakuza watoto katika namna moja ama nyingine na si kwenda kuwapatia elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vingi vya elimu havifiki kwa wakati muafaka katika Halmashauri zetu za Wilaya. Mfano, vifaa vya kufundishia somo la sayansi kwa kweli limekuwa ni tatizo kubwa sana, ndio maana unakuta watoto wengi hupelekeea kufeli na hawapati elimu nzuri ya kuweza kuendeleza Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kondo pia ina Chuo cha *MCH* kilichopo Hospitali kuu ya Kondo, hiki kinatoa wauguzi. Lakini wananchi hawanufaiki na chuo kilichopo Wilayani Kondo. Wauguzi wakishapata mafunzo yao tayari hupangwa sehemu nyingine mbali tofauti na Wilaya yenye ilipo. Hospitali ya Kondo ina uhaba mkubwa wa vifaa vifuatavyo: ina uhaba wa watumishi, ina uhaba wa vifaa vya kutendea kazi vya hospitali, ukizingatia hospitali ile ndio inayobeba Wilaya mbili zote kwa pamoa. Madawa yamekuwa ni tatizo kubwa sana katika Wilaya ya Kondo. Ajali inapotokea utakuta wale wanafunzi ndio wanakuja kutoa huduma pale badala ya kwamba wale ambao wamekwishahitimu wangeweza kubakizwa pale na wakaweza kufanya kazi. Kwa kweli imekuwa ni kero kubwa katika Hospitali ya Kondo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko vijijini nako kumejengwa zahanati katika Kata mbalimbali na zimeshakuwa tayari, lakini hazina watumishi, hazina madawa, wananchi wanapata kero kubwa kulazimika tena kwenda Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kondo ni Wilaya ambayo kwa kweli ina sifa kubwa, Wilaya ya Kondo ndio kioo ambacho Tanzania nzima inakiangalia. inapaswa ikumbukwe kwamba, ndiyo Wilaya iliopotiwa na Wakoloni na ndio Wilaya ambayo ina michoro yote ya mapangoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, Wilaya hii inalima mazao yafuatayo, inalima ufuta, inalima mbaazi, inalima kunde inalima ulezi, inalima msimusimu, alizeti, inalima mahindi, haya yote ni mazao ya biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linalowakuta wakulima wa Wilaya ya Kondo wanapokuwa tayari wamelima mazao yao, kwa kweli wanapata adha kubwa ya soko kwa

ajili ya kuuza mazao yao hasa kwa kukosa mawasiliano. Mawasiliano ya Kata kwa Kata, Wilaya kwa Wilaya hadi Mkoa. Mtu kujua bei leo imepanda ama imeshuka imekuwa ni shida, anavizia yule ambaye ni mlanguzi anayesimamisha gari lake mlangoni kwa mkulima na kumwambia bei anayotaka ye. Hebu Serikali iangalie inamtendea nini huyu mkulima ambaye hapewi mafunzo yoyote ya ukulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo mkulima anakutana na adha kubwa ya mageti yaliyoko katika Wilaya. Kuna mageti ya kutoka Kata hadi Kata, kwa mfano, ukitoka Bumbuta mpaka Masange geti na hutozwa sh. 1,000/= kwa gunia, ukitoka Masange mpaka ufile eneo la Babati geti. Wakati huo wananchi wa Wilaya hiyo wakilima alizeti au ufuta hulazimika kwenda kukamua mafuta hayo Babati kwa sababu ya unafuu wa bei. Hivi kweli umeme ungekuwepo vijijini katika Wilaya yetu ya Kondoa hawa wananchi wasingepata adha hiyo. Pia zao hili lingekua kwa kiwango kikubwa mno na kuweza kunufaisha hata Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina suala lingine, simu ni mawasiliano ya haraka mno. Wilaya ya Kondoa inapaswa kuwa na mawasiliano, haya mawasiliano ni mazuri zaidi pia tunawaita wawekezaji pale Kondoa au watalii wanaokuja pale Kondoa. Mtalii anaingia pangoni anaweza kupatwa na tatizo lolote, simu hakuna. Naomba tuletewe mitandao katika maeneo ambayo yana watu wengi. Tukipata mitandao ya simu za mikononi itakuwa imetuina kwa kiasi kikubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nimalizie na suala moja kuwa, Wilaya ya Kondoa pia ina Chuo cha Maendeleo cha Munguri. Kwa kuwa wanafunzi wengi wamefeli na tunao wengi pale ambao hawana ajira yoyote, wala kazi yoyote. Basi kama Chuo kile wangekipandisha hadhi na kuwa VETA na kuleta walimu ambao watawafundisha wale wanafunzi ili tuweze kupata wajenzi amba ni bora na siyo kwamba wajenzi tuwatoe katika Mikoa mingine kuja kutujengea nyumba zetu katika Wilaya yetu ya Kondoa, kwa mfano, mafundi umeme, wajenzi, madereva, *mechanic* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba muiangalie Wilaya ya Kondoa kwa jicho la huruma. Wilaya ya Kondoa pia imekosa miundombinu mingi ya barabara, kutoka Kata kwenda Kata imekuwa ni kero kubwa sana. Pia Wilaya ya Kondoa inakutana na adha kubwa, wananchi wa Kondoa wamekuwa kama wafugaji wanahama au kama vile wahamaji. Tunaomba kuwepo na Sera ya Ardhi, ingawa ipo lakini haitumiki ipasavyo. Tanzania nafikiri kungekuwa na Sera ya matumizi ya Ardhi, haya yote yasingekuwepo. Ningeomba kuishauri Serikali vitu kama hivyo viwepo. Pia walemavu wapatiwe shule Mkoa wa Dodoma na mafuta yao, kwani wakipata uwezeshaji wanaweza, pia wana miradi ya utengenezaji baiskeli hapa Dodoma ila hawana elimu nao wana haki ya kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, kwa kuwa bajeti hii haikidhi mahitaji ya wananchi, siko tayari kuunga mkono. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili na mimi nichangie katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia na akaniwezesha kuwa mionganini mwa Wabunge wa Bunge hili la Kumi, nashukuru sana. Lakini niwashukuru pia viongozi wangu wa Chama walionipa imani na kunituea kuwa mgombea kwa nafasi hii katika Jimbo langu la Magogoni. Shukrani maalum ziwaendee wananchi na wapiga kura wa Jimbo la Magogoni, kwa namna ambavyo waliamua kunipa nafasi yao hii ya kuwawakilisha katika Bunge hili na *Inshallah* ninawaahidi kwamba, nitajitahidi kuwawakilisha kwa kadri ya uwezo wangu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Katibu wangu Mkuu wa Chama Maalim Seif Shariff Hamad pamoja na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa maamuzi yao ya kuunda Serikali ya pamoja pale Zanzibar. Ni jambo zuri linafaa kuenziwa. Nina imani huko tunakokwenda yale ambayo yalijitokeza kwenye chaguzi zilizopita hayatajirejea. Kwa kuwa ni jambo zuri pia nina furaha kuona ndugu zangu wa CHADEMA na wao wameanza kuona kwamba inafaa. Juzi walifanya Muungano huu na Chama cha Mapinduzi pale Arusha, nawapongeza. Wala wasidhani kwamba sisi tutakuwa na mashaka kwamba wao wamekuwa CCM (C), maana CCM (B) walishatupa sisi *CUF*, lakini sisi hatutaona hivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na vijana na ajira. Kwa taarifa na kwa namna ambavyo Serikali, Mawaziri mbalimbali, Wabunge, watendaji wengine Wilayani kwamba tuna tatizo kubwa la vijana wasio na kazi ndani ya Taifa letu. Kwa taarifa tuliyonayo ni kwamba kila mwaka taifa hili linazalisha vijana 700,000 amba wanaingia kwenye soko la ajira, katika ya 700,000, ni vijana 400 pekee amba wanaajiriwa na vijana 660,000 wanaingia mitaani wakiwa hawajui nini cha kufanya. Sambamba na hao kuna vijana wale amba wanashindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya ugumu wa maisha ndani ya familia, ni wale amba wanafeli katika madarasa ya saba na darasa la kumi, nao hali kadhalika wanatumbukia mitaani sambamba na wale wa kundi la mwanzo wakiwa hawana kazi na hawana matumaini juu ya maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kundi lingine ambalo ni wale amba kwa namna yoyote hawaendi shule au hawakupita shule kabisa. Makundi yote haya bado ni jukumu letu, ni jukumu la Serikali yetu kuhakikisha kwamba vijana wote hawa, makundi yote haya, wanapata maisha yao na wanaishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa sisi katika Chama cha Wananchi (*CUF*) tunaamini kwamba vijana ni Taifa la leo. Lakini nadhani upande wa Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi wao wanaamini kwamba vijana ni Taifa la kesho, ndio maana Mzee Kingunge Ngombale Mwiru amekuwa Kamanda wa Vijana wa CCM, hii ni kuthibitisha kwamba mpaka uwe na makamo ya kama Mzee Kingunge ndio uonekane sasa ni kijana unastahiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi pia kusema kwamba tumepiga hatua kubwa ya maendeleo wakati kundi kubwa la vijana tumeliacha nyuma likiwa halina matumaini na maisha yao. Lakini naomba niishauri Serikali iwe na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba viwanda vile ambavyo vimekufa vinafufuliwa, viwanda ambavyo vipo vinafanyiwa marekebisho na tunaanzisha viwanda vipyta kusudi makundi haya ya vijana tuyaelekeze huko ili na yenyewe yaweze kuwa na matumaini ya maisha yao, tutakuwa tumewasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya suala la habari. Tuna Wizara ya Habari na pale Mikocheni kuna kituo cha *TBC*, kituo kile ni kituo cha Taifa na nawapongeza sana kwa jitihada zao na namna ambavyo ndani ya Tanzania maeneo mengi *TBC* wanasihika katika *televisions* zao na hata redio. Lakini Serikali inatumia fedha nyingi za wavuja jasho kukodi majengo ambayo *TBC*, kituo cha Taifa kinatumia majengo hayo katika kuendesha shughuli zao. Ingekuwa busara sana na kwa sababu ndani ya Mikocheni walipo *TBC*, kuna jengo kubwa, jengo lile ni madhubuti sana, ni la zamani na ukienda pale kuna kibao cha jiwe la msingi lililowekwa na Mheshimiwa aliyejikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mzee Mwinyi, jiwe lile la msingi limewekwa tangu tarehe 13 Aprili, mwaka, 1995 mpaka leo jengo liko vile vile alivyoliacha Mzee Mwinyi na inawezekana likaendelea mpaka awamu hii ya Mzee Kikwete itakapomalizika. Sasa sipendi iwe hivyo na naomba niishauri Serikali kwamba lile jengo limalizwe katika bajeti hii itakayoanza tarehe 1 Julai, 2011 ili tuweze kuokoa fedha nyingi za wavuja jasho na maeneo ambayo *TBC* walikuwa wanakodisha waweze kuhamia pale ili tuwe tumeokoa hizo fedha za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kwa sababu hatuna sera endelevu, hatuna sera ya Taifa na inaonekana wazi kwamba kila awamu inayokuja inakuja na mambo yake mapya, lakini ingejuwa ni sera endelevu, basi jengo lile zuri madhubuti sana isingefika mpaka leo tunazungumza hapa kuwa bado halijamaliziwa. Hili ni tatizo ambalo linatia mashaka, hata huu Mpango wa Taifa wa Mheshimiwa Kikwete wa Miaka Mitano, inawezekana hata ukiwa ni mpango ambao umekubalika, lakini akiondoka ataondoka nao mwenyewe, ndiyo sababu jengo lile mpaka leo bado halijamaliziwa, watendaji wapo wanajua, lakini bila kujali fedha za wananchi zinatumika kwa kukodisha majengo mengine, jengo linaangaliwa hivi hivi siku zinapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Watanzania wastaafu, baada ya muda wao wa kulitumikia Taifa unapomalizika. Wastaafu hawa ni Watanzania ambao wamepoteza muda wao, wametumia umri wao, nguvu zao zote kulitumikia Taifa letu hili, lakini inashangaza na kustaajabisha sana kwamba mstaafu au mtumishi anapostaafu anaonekana kama ni kero kwa Serikali wakati anapofuutilia posho zake au stahili zake za ustaafu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tajiri anawekeza kwenye biashara akiamini kwamba akifikia izeeni biashara zingeweza kumsaidia wakati atakapokuwa hana nguvu tena, lakini mtumishi wa Serikali anaamini naye nikimaliza nitapata kitu cha kuanzia maisha mapya, lakini kwa Serikali inaonekana kana kwamba jambo hili halipewi nafasi inayostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni hatari sana na hii ni kuwadhalilisha wastaafu na ndiyo maana kwa wale ambao mpaka sasa ni watumishi wa Serikali wanapopata nafasi kuchukua chao mapema wakijua kwamba nikimaliza nitaondoka mimi na shati langu na suruali, aidha na baiskeli yangu ambayo nimekuja nayo kazini. Hili si jambo zuri hata kidogo na inafaa Serikali ione kwamba wastaafu wale ni watu ambao wamelifikisha Taifa letu hapa tulipo ambapo leo tunajidai kwamba tulisoma, lakini aliyekusomesha ni Mwalimu ambaye amestaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajidai kwamba Tanzania tuna hali ya amani na usalama, tuna utulivu mkubwa, hii ni kwa sababu ya majeshi, Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi na majeshi mengine yalivyowajibika na ndiyo maana leo tunajisifia kwa amani iliyoko. Lakini sote tumepita Hospitali kupata tiba kuangaliwa na Madaktari, lakini leo Madaktari hao ndiyo ambao wamestaafu, inashangaza kuona kwamba Serikali inaona kama inapoteza muda, inapoteza fedha bure kuwapa stahili zao waastafu hawa, si jambo zuri hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala au sehemu ya zile kero za Muungano. Baada ya kufa kwa Jumuiya ile ya Afrika Mashariki, Zanzibar kama sehemu ya Jumuiya ile tulikuwa na fedha zetu au tulipata mgao wetu, mgao ule uliishia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, hadi leo Wazanzibari hawajui mustakabali wao juu ya fedha ile kutoka miaka ile na mpaka sasa. Lakini kulikuwa na utaratibu na hili ni jambo la kisheria limo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 133 imeelezwa wazi kwamba: “Kutakuwa na *account* ya pamoja baina ya SMZ na SMT. Jambo hili limekuwa likizungumzwa muda mrefu sasa, tangu mie sijawa Mbunge mpaka leo niko Mbunge na bado hakujawa na mustakabali mzuri juu ya *account* hii ya pamoja. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kufanya majumuisho atwambie habari hii itakwisha lini, ni lini Wazanzibari watajua mustakabali wao juu ya kuwepo kwa *account* hii ya pamoja. Kuna haki za Wazanzibari ambao hapa zinaonekana zinamezwu na hizi ni sehemu ya kero za Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna *TRA*, kuna *ZRB* pale Zanzibar ambavyo vyote ni vyombo vya kukusanya kodi. *TRA* inakusanya kodi zile za Muungano au za nje, lakini *ZRB* inakusanya kodi zile za Zanzibar, lakini kwa kuwa ni ndugu mmoja tuliuungana kwa nia safi na kwamba tunapendana kama inavyoelezwa, kwa nini Zanzibar *ZRB* isiachiwe ikusanye kodi zote mbili ikiainisha tu kwamba, hii ni ya nje au ni ya Muungano na hii ni ya Zanzibar. Kwa nini kuna haja ya kuwepo vyombo viwili, wakati tukijua tunaongeza urasimu wa matumizi ya Serikali kwa kuweka vyombo viwili ambavyo vyote vinafanya kazi zinazofanana? Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote niliyochangia juu ya hotuba hii, naomba nizungumzie pia suala la michezo kidogo. Tanzania tumekuwa tukilalamikia kwamba vilabu vyetu aidha, hata timu zetu za Taifa imekuwa ni kichwa cha mwendawazimu, nawashukuru timu ya vijana chini ya miaka ishirini na tatu wametukosha uso kidogo. Naomba tuwaenzi, tuwaendeleze ili tupate jina kuitia timu hii. Lakini nchi nyingi duniani... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata muda wa kuchangia hotuba hii, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa tunakushukuru.

TAARIFA YA SPIKA

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge ambaye ametoa taarifa wakati anachangia, ndugu yangu Ahmed kwa mujibu wa Kanuni namba 64(a) alitoa taarifa ambayo sio sahihi kuhusiana na *TFF*. Nilipenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu, ili nchi kuwa mwanachama wa *FIFA* kwa mujibu wa *Katiba ya FIFA*, aya ya kwanza, nchi inatakiwa iwe mwanachama wa *United Nations*. Zanzibar sio wanachama wa Umoja wa Mataifa. Kwa misingi hiyo, inakuwa vigumu, hata hivyo, katika kuendeleza Muungano wetu, zimeundwa Kamati inayoongozwa kwa upande wa Zanzibar na ndugu Hafidhi Ali, kwa upande wa Tanzania Bara Alex kwa ajili ya kuwezesha mafao yote yanayotolewa na *FIFA* ili nchi zote hizi mbili ziweze kufaidika. (*Makofit*)

Mfano kuna uwanja sehemu zote mbili za Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, kwa mfano, uwanja wa Pemba tumepewaa msaada.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rage kama ni taarifa basi iwe fupi maana sasa unachangia.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana kwa mfano, uwanja wa Pemba kuna majani ya *artificial* ambayo yaliletwa Bara ili kuimarisha Muungano wetu yalipelekwa Pemba. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, namna ya kutoa taarifa tutumie tu fursa wakati ule yule mse maji anapokuwa anasema, unampa taarifa yeye au kisha tu kumaliza kusema unampa taarifa. Kwa sasa hivi Mheshimiwa Rage alichokifanya basi tu, kwa sababu taarifa yake pia imetusaidia, lakini kimsingi haikuwa na nafasi maana yake nilidhani anampa taarifa huyu aliyetoka kusema sasa, kumbe anampa taarifa aliye maliza kusema muda mrefu. Basi tuendele, Waheshimiwa Wabunge basi anayefuatiwa sasa ni Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah na baada ya hapo Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ajiandae.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kusimama hapa ili kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini la pili, niwashukuru viongozi wangu wa Chama Taifa na tatu sina budi pia niwashukuru wanachama wangu na wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Tumbe na nawatakia kila la heri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama Taifa lolote duniani, linahitaji mipango mizuri ili kufikia malengo iliyokusudia. Nilipitia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nimeona kuna baadhi ya maeneo hakutoa uzito unaostahiki. Eneo ambalo nimeliona hakutoa uzito unaostahiki ni haki na uhuru wa raia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sana sasa haki na uhuru wa raia unaingiliwa kati na wadau wakubwa wanaoingilia uhuru huu ni vyombo vyetu nya dola. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia ana haki zake chini ya Katiba, kifungu cha 13-24, ana uhuru wa kutoa maoni yake *either* iwe kwa vyombo nya habari au iwe kwenye maandamano au iwe kwenye mikutano. Hili ni jambo la kusikitisha sana, raia wanapotumia haki zao wanaingilia kati na hatimaye hakuna kiongozi yeoyote ambaye anasimama na anakemea kwa nguvu zote vitendo hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia ndiyo tunamtegemea katika Taifa hili, ndiye mlipa kodi, ndiye ambaye atakayeleta hicho kilimo kwanza, lakini leo hii kama wanafunzi wanaandama, wanapeleka ujumbe wao, wanapeleka matatizo yao, kwa nini wanafunzi wanapigwa? Kwa nini wanafunzi hawa wanafukuzwa chuoni? Hivi jamani tumetumia akili yetu *to the maximum* ni nini cha kufanya, kwa nini wanapigwa, kwa nini wanatiwa ndani hovyo hovyo? Raia lazima tuwaheshimu kama Mataifa mengine yanavyoheshimu raia wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika utawala bora, utawala bora ndiyo msingi wa haki na usawa wa mwanadamu katika Taifa lolote lile, ndiyo unaojenga utumishi bora, ndiyo unajenga mazingira mazuri ya kuleta uchumi bora katika Taifa, lakini yote haya hayakupewa kipaumbele na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo na takwimu niliyonayo ni kwamba Watanzania wengi ambaao wanafikishwa mbele ya sheria basi kesi zao zinafutwa na wachache sana kesi zao zinathibiti. Sasa nilikuwa najiuliza nini tufanye ili wimbi hili la dhuluma liweze kuondoka kwa raia wa Tanzania. Nina wazo moja, nilisema kama kuna mshtakiwa ambaye amefikishwa Mahakamani na hatimaye akaonekana hana hatia, Serikali imlipe fidia kwa mazingira na athari aliyopata. Lakini kama kuna Polisi ambaao wamemkamata raia huyo, wamempeleka Mahakamani na kesi ikathibiti kama huyu ni mkosaji, basi askari huyo apongezwe na aongezwe mshahara wake. Lakini pia kama kuna askari amefanya uzembe, ameshindwa kuthibitisha kesi mahakamani na kesi hiyo imefutwa, amelitia hasara Taifa na kwa maana hiyo apunguziwe mshahara wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake unajenga ile dhana kwamba haki kwa raia lazima itendeke, huwezi kumkamata mtu hovyo hovyo, uwe na ushahidi wa kutosha wa kwenda kuthibitisha Mahakamani kama huyu ametenda kosa. Msiachie hivi hivi tu, hawa raia wanatutegemea sisi na sisi ni wachungaji. Kila kiongozi atakwenda kujibu, wewe umeongoza vipi, lazima hawa raia tuwaonee imani sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamechangia sana masuala ya Muungano, lakini nilikuwa natafuta *suggestion* sijaipata. Nataka nichangie kidogo ili nitoe *suggestion* kuhusu masuala ya Muungano. Muungano wetu una uhai wa miaka arobaini na saba, nchi zote duniani ambazo ni tajiri wameimarisha Muungano wao, Marekani wameungana kwa kumwaga damu na sasa ni nchi ambayo inasaidia ulimwengu mzima. Muungano ni mzuri sana, lakini sasa tatizo kubwa ni muundo wa Muungano, watu wanaopiga kelele sasa wanaona kwamba mgawanyo wa mapato baina ya Serikali ya Muungano wa Zanzibar hawatendewi haki, wanasema hivyo, wanaona kwamba ajira katika vyombo vya Muungano havitendi haki, wanaona kwamba Rais wa Zanzibar kuondolewa Kikatiba kutokuwa Makamu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumeidhalilisha Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wenzangu nahisi waliangalia sana kule kwenye mfumo wa Vyama Vingi *in case* kama Zanzibar wamepata Rais, huku atakuaje? Lakini suluhisho hapa ninavyoliona, ili kujenga upendo baina ya Taifa hili, Wanzanzibari na Watanganyika, Wazanzibari wako Mbeya, wako kila sehemu, wamejenga majumba yao, wameoa, wanafurahi katika Taifa lao, lakini ili kuimarisha Muungano wetu, lazima tubadili muundo wa Muungano na aina pekee ni kufuata sera za Chama cha CUF, sera ya CUF inasema ni lazima tuwe na Serikali tatu. (*Makofi*)

Kuwe na Serikali ya Zanzibar, ambayo Zanzibar itajenga uchumi wake, itajenga heshima yake na kuwe na Serikali ya Tanganyika ambayo nayo itafanya shughuli zake za kiuchumi. Ili kuimarisha Muungano na umoja wetu wa Kitaifa basi kuwe na Serikali ndogo ya Muungano. Hii itakuwa inaangalia nani anataka nini, nani ameshindwa, nani anataka msaada gani, tunajenga umoja mzuri tu, tutafurahi katika Taifa letu, hakuna haja ya kuvutana. Mzee wangu Lowassa alisema CCM itoe maamuzi, juzi nimemsikia, “toeni maamuzi msiogope”. Tunataka tujenge Tanzania mpya, tunataka kupata *new generation*, wanasahau kwa miaka 64 ilikuwaje, tuwajengee mazuri waishi katika Tanzania yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sehemu nyingine ya TAMISEMI. Mimi na-declare interest ni Mjumbe katika Kamati ya Sheria Ndogo, tulijaribu kuzipitia sheria mbalimbali. Lakini kitu cha kusikitisha sana Waziri anapitisha Sheria bila kuelewa ile adhabu ya *Principal Act* ni kubwa lakini ukienda huko chini Sheria iliyotolewa ni ndogo. Au inakuwa *vice versa*, kama faini ni shilingi laki moja basi ye ye atasema ni laki moja na nusu. Kama kifungo ni miezi sita ye ye atasema ni mwaka mmoja na sheria hiyo imepita kwa Waziri mwenyewe. Kwa kweli ni kitendo cha hatari sana. Tuna ushahidi wa kutosha, Mwenyekiti wangu ndiyo Mwenyekiti yule pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hawa Watanzania tunawapeleka wapi? Kwamba hata hata kutunga sheria hatupo *careful*. Sheria huko *careful why?* Unakwenda wapi, mnafanya nini, kama unafuata sheria huko *careful*. Ndiyo maana hii tunaandaa mikataba mibovu, kwa uzembe tu. Tunalitia hasara Taifa kwa mikataba mibovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nitaligusia kidogo ni mtazamo wa Tanzania itakayokuja. Tunaona watu wa barabara waweka alama wale wanaendesha gari

kama huko mbele kuna mpindo basi kuna “L” huku inakuonyesha kwamba kuna mpindo. Sisi tunatoa *indications* kwamba tunasubiri marekebisho ya Katiba, hii ndiyo *indications* zetu, Katiba mpya, tunataka muundo mzuri wa Tanzania, tunataka Watanzania wapendane. Watanzania ni ndugu. Huwezi hata ukachukua kipimo gani, huwezi ukambagua Mtanzania, huwezi kubagua Tanzania, ni kitu kimoja na Taifa ni moja. Tunataka tuone mazingira mazuri, tufanye kazi zetu vizuri ili vizazi vijavyo visije kutulaumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ahsante sana. Siungi mkono hoja. (*Makofî*)

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA): Kutohana na Kanuni ya 64(A) inasema kwamba: “Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge (a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Napenda kutoa ufanuzi kuhusu migomo ya Vyuo Vikuu. Migomo ya Vyuo Vikuu inapoanza wanafunzi huwa wanakuwa *advised* kuingia madarasani kwa muda wa siku tatu. Sasa kama siku tatu hawaingii madarasani, basi chuo inabidi kifungwe. Sasa wanafunzi wanavyofanya wanawalazimisha wanafunzi kugoma na hasa watoto wa kike. Ni taarifa ambazo watu hawazijui lakini wanafunzi wanapigwa sana. Sasa inapofikia hapo huwezi kuacha wanafunzi wanaumizwa, mwaka juzi tulishaona kuna mwanafunzi alikuwa amechinjwa kwa sababu ambazo hazikueleweka. Kwa hiyo, ili kuokoa maisha ya wanafunzi inabidi polisi waingilie kati na kuhakikisha wanafunzi wanatoka chuoni kwa usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofî*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITU: Taarifa unampa yupi sasa?

MHE. MOSES J. MACHALI: Nampa Mheshimiwa Waziri aliymaliza kutoa taarifa yake hivi sasa.

MWENYEKITU: Hakuna utaratibu wa taarifa juu ya taarifa bwana. Waheshimiwa Wabunge aliyepewa taarifa naamini kabisa ameisikia. Kwa hivyo, tunaendelea tusipoteze muda hapa.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Siikubali taarifa hiyo. (*Makofî*)

MWENYEKITU: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kushukuru kwa kupata fursa hii. Awali ya yote niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Busanda kwa kunichagua tena kwa mara ya pili baada ya kuwa Mbunge kwa

kipindi cha mwaka mmoja. Hakika ni imani ya kipekee sana na mimi natoa ahadi kabisa ya kuwatumikia kwa moyo wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Wizara au Sekta ya Nishati na Madini. Sekta hii ni sekta muhimu sana ambapo napenda kushukuru Serikali kwa mradi wa *MCC* ambao utapeleka umeme katika Kijiji cha Bukoli Nyarugusu, Lumgasa na Katoro. Pamoja na shukrani hizi, katika sekta ya madini kwa kweli bado kuna kero kubwa ambayo ningeomba Serikali iangalie kwa makini. Katika Jimbo la Busanda Mungu ametubariki sana kwa sababu maeneo mengi tuna madini. Sisi wenyeewe tunajivunia sana kutokana na madini hayo. Sasa basi kutokana na madini haya wachimbaji wadogo wadogo ambao wanachimba katika maeneo haya bado wana changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi napenda kuishukuru Serikali kwa sheria ambayo ilitungwa mwaka 2010, Sheria mpya ya Madini ambayo inaonyesha kabisa ambavyo itasaidia sana wananchi kwa kiwango kikubwa ili waweze kupata kipato chao. Pamoja na sheria hii naona utekelezaji wake bado haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa kama ilivyosema ndani ya Sheria mpya kwamba, itaweka maeneo rasmi kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Niiombe Serikali iweze kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Katika maeneo ya Nyarugusu, Nyarugusu kuna eneo ambalo linaitwa *Buziba Small Scale Gold Mine* ambalo lilianzishwa mwaka 1983. Sasa basi niiombe Serikali eneo hili iwapatie au iwatengenee wachimbaji wadogo wadogo. Ni kweli kabisa tunahitaji wachimbaji wakubwa ndani ya nchi hii ili kuweza kuongeza kipato cha Taifa, lakini sasa naomba pia wachimbaji wadogo wadogo tusiwasahau. Ndiyo maana naiomba Serikali, katika eneo hili la *Buziba Small Scale* ambalo lilitengwa siku za nyuma, basi litengewe wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kunufaika, waweze kuchimba kwa uhuru kabisa bila kero yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu wananchi wengi wa Nyarugusu wameteseka sana hasa eneo hili lilipochukuliwa wakawekwa walinzi ambao wakiona mwananchi amekatiza ndani ya eneo hili wamebeba moko, tayari wale maaskari wanaanza kuwanyanya kumbe moko ni zana tu ambayo ni muhimu, ambayo inatumika katika maeneo hayo. Lakini pia hata wale wananchi ambao wanaishi katika maeneo hayo wafugaji wakiona mifugo inakatiza ndani ya eneo hilo tayari walinzi wanaanza kuwaletaa wananchi bugudha. Kwa hiyo, niombe Serikali, sasa ni wakati muafaka iweze kutenga eneo rasmi ya Nyarugusu kwa ajili ya wachimbaji hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuja Nyarugusu mwaka 2010 ye ye mwenyeewe alitoa ahadi kwamba atatenga au atatoa eneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, niombe rasmi kwamba, isiwe basi ahadi hii ikawa ni ahadi hewa. Niiombe Serikali izingatie suala hili kwa kuwatengea maeneo katika eneo hili la Nyarugusu. Pamoja na Nyarugusu pia katika eneo la Ramgasa pamoja na Kaseme kuna eneo linaitwa *Tembo Mine* ambapo ni sehemu ambayo wachimbaji wadogo wadogo wachimbaji wadogo wadogo wanachimba madini. Eneo hili Serikali imeweza kutoa leseni kwa wachimbaji wakubwa. Lakini kabla ya hapo kulikuwa na wananchi ambao

walikuwa wakichimba madini pale kwa muda mrefu. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwakatia wananchi angalau lile eneo walilopo sasa, siyo kubwa sana, ni eneo lenye ukubwa kama wa hekari mbili tu ili waweze kuruhusiwa kuchimba kwa sababu wananchi hawa wanategemea machimbo, hawana kitu kingine cha kuwapatia kipato kwa ajili ya kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, kweli eneo la *Tembo Mine* ni eneo ambalo leseni imetolewa kwa wachimbaji wakubwa. Lakini basi hiki kieneo kidogo tu ekari mbili. Niiombe Serikali iweze kuwapatia wananchi kwa sababu tayari kuna mashimo yako pale. Nilitembelea eneo hilo, nikazungukia eneo lote, kuna mashimo na kuna wananchi wengi sana yaani utakuta kuna wananchi 20,000 wako pale wakiendelea na shughuli zao. Kwa hiyo, nina wasiwasi kwamba eneo hili likichukuliwa na wachimbaji wakubwa bila kuwapa wananchi hawa kunaweza kukatokea migogoro isiyokuwa na manufaa. Najua Serikali imesikia suala hili. Pia niendelee kuomba hata *Bingwa Leef* Serikali iangalie namna ya kuwapa wachimbaji wadogo wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika Sekta ya Kilimo. Tunaishukuru Serikali kwa sekta hii ya Kilimo. Ni kweli kabisa imeanzisha masuala ya Kilimo Kwanza. Lakini Sekta hii bado naona kuna changamoto. Kwa sababu mbolea za ruzuku zinapewa kwa wakulima wachache sana na katika vijiji vyetu kila ninavyotembelea naulizwa kwamba mbona sisi hatupati hizi mbegu za ruzuku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe ruzuku kwa wananchi wote bila kujali. Unakuta katika kijiji wanatoa kwa kaya 400 tu wakati kijiji kina kaya 1,000. Huu ni ubaguzi na imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi hawa. Ili basi kuweza kuwaendeleza wananchi hawa naiomba Serikali itoe ruzuku kwa watu wote bila kujali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifurahi sana niliposikia mpango wa SAGCOT katika Mikoa ya Kusini. Lakini sikusikia mpango wowote kwa Kanda ya Kati au kwa Kanda ya Ziwa. Naiomba Serikali kama ilivyoweka mpango wa SAGCOT kule Kusini na sisi Kanda ya Ziwa na sehemu zingine tupewe mpango mwengine kabambe, ili kuweza kuinua hali ya kilimo chetu. Kwa sababu zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wetu wanaishi vijijini na wanajishughulisha na kilimo. Kwa kuwapa mpango mkubwa kabambe wa kilimo nina uhakika kweli kabisa tutaweza kuinua hali za wananchi hawa kiuchumi, tukizingatia katika mikoa iliyoko kando kando ya Ziwa Victoria, Mikoa ya Mara, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Geita, Mkoa wa Kagera, ni mikoa ambayo imejaliwa neema kwani imezungukwa na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Wilaya yetu ya Geita vile vile katika Jimbo langu ndiyo usiseme, sehemu za Bukondo, Nungwe, kwa kweli ni mahali pazuri sana ambapo tukiweka mpango kabambe kabisa wa umwagiliaji najua teknolojia hii labda pengine hatuna, lakini kuna Mataifa mengine kama Israel, kuna utaratibu mzuri tu wa umwagiliaji ambao wanatumia pengine *drip irrigation*, Tukifanya hivyo, kwa hakika tutaweza kunufaika pamoja na watu wa Mkoa wa Mwanza na Mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa pamoja na Jimbo langu kwa ujumla. Kwa hiyo basi, niiombe Serikali na

Mheshimiwa Waziri Mkuu anapofanya majumuisho aeleze mpango kabambe kwa ajili ya Kanda ya Ziwa ili kuweza kunusuru hali ya uchumi kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikienda katika mikutano yangu ya mara kwa mara huko Kanda ya Ziwa. Wananchi wamekuwa wakiniuliza mbona mara nyingi kwenye redio, kwa sababu siku hizi ni utandawazi huwezi ukaficha kitu, tunasikia tu Kusini wanapewa mbolea bure, wanapewa mbegu, wanapewa hiki. Mbona sisi huku Kanda ya Ziwa hatupati? Kwa hiyo basi, nitumie fursa hii pia hata mimi kuiomba Serikali kwamba, tuweke mpango kabambe kwa ajili ya Kanda ya Ziwa ili kuweza kunusuru au kuongeza hali ya uchumi wa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la elimu. Elimu ni kitu muhimu sana kwa ajili ya Taifa. Katika Mkoa wa Mwanza kwa kweli katika Sekta hii tuna upungufu mkubwa sana. Nilikuwa nikiangalia zile takwimu ambazo Waziri Mkuu amezitoa, Mkoa wa Mwanza tu, kuna upungufu wa nyumba za walimu, 15,000; madarasa 9,958 na madawati 215,911. Siyo tu katika Mkoa lakini pia katika Wilaya ya Geita upungufu wa madawati ni 31,080 ikifuatia na Mkoa wa Shinyanga pamoja na Kagera. Lakini ukiangalia mikoa mingine kama Kilimanjaro, kuna upungufu wa madawati 19,000 na Lindi ni madawati 16,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali itusaidie kwani katika Mkoa wa Mwanza hasa katika Wilaya ya Geita tuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu, madarasa na madawati. Mimi mwenyewe ninapotembelea kule naona jinsi ambavyo watoto wanakaa chini. Kuna shule moja pale Katoro nilipotembelea, kwanza Mkuu wa Shule ile au Mwalimu Mkuu alitoa machozi mbele yangu ili niweze kumwonea huruma kwa jinsi ambavyo wanakaa chini. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba, umefika wakati sasa ifanye hatua za makusudi ili kuweza kuangalia maeneo haya muhimu ambapo huduma zipo kwa kiasi kidogo na mapungufu ni makubwa sana. Kwa hiyo, niombe pia katika Wilaya yetu ya Geita, tuna upungufu pia katika huduma muhimu kama magari ya ukaguzi.

Yalikuwepo magari mawili, lakini mabovu sana. Lakini pia kwa upande wa elimu ya sekondari, tangu Idara hii imeanzishwa hakuna gari kabisa. Wilaya yenye ya Geita ina shule za msingi zaidi ya 200, zaidi ya 40 shule za sekondari. Kwa hiyo, naiona ni kazi kubwa sana ambapo Serikali inatakiwa itujali, iletu magari kwa ajili ya kuwezesha kazi hii kufanyika kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya. Katika Wilaya yetu ya Geita na hasa katika Jimbo la Busanda tuna upungufu mkubwa. Kila kijiji nilichokuwa nikitembelea tatizo hata madawa ya kutibu malaria, dawa ya mseto haipo. Kila nikienda kila kituo hivyo hivyo, zahanati hakuna, Kituo cha afya hakuna. Sasa mimi binafsi nilikuwa najiuliza kwamba sasa huyu mwananchi wa kawaida anapataje huduma hii. Niiombe sasa Serikali iangalie utaratibu nzuri wa kuhakikisha kwamba dawa za malaria na dawa zingine muhimu zinakuwepo katika zahanati zetu pamoja na Vituo vya Afya ili kunusuru hali ya maisha ya wananchi wetu. Kwa kweli wananchi wanahangaika sana

huku na kule kupata matibabu, matokeo yake wanaambiwa nenda kanunue dawa. Sasa mwananchi wa kawaida hata kipato chenyewe hana, inakuwaje? (*Makofi*)

Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie utaratibu muhimu wa kuhakikisha madawa yanakuwepo wakati wote. Lakini vile vile kuna malimbikizo ya mishahara ya watumishi katika Sekta ya Afya, ni tatizo kubwa sana. Katika Wilaya ya Geita pekee, wanadai takriban milioni 400 ambazo mpaka sasa ni madai na wanahangaika kweli watumishi hawa. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye uchunguzi katika suala hili ione namna ya kusaidia Sekta hii ili watumishi waweze kufanya kazi zao kwa amani na furaha na kuwatibusi wananchi wetu vizuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu iliahidi gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Chikobe. Nitumie nafasi hii kuiomba Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe katika bajeti ya mwaka huu gari la wagonjwa Chikobe linapatikana. Kwa sababu kituo hiki kiko mbali sana na Wilayani Geita na wananchi wanateseka *bus* lenyewe ni moja, linatoka asubuhi linearudi jioni. Kwa hiyo, kunapotokea shida yoyote hasa kwa akinamama wajawazito wanaotaka kujifungua inakuwa kero kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la gari Chikobe alikumbuke. Naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kusimama hapa tena katika awamu yangu hii ya pili wakati nachangia Bajeti ya kipindi hiki cha awamu ya pili katika Ubunge wangu. Pia naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi na wanawake wote wa Mkoa wa Pwani, kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuhakikisha kwamba Chama cha Mapinduzi kinashinda na hali kadhalika kunipatia mimi ushindi na kuweza kurudi tena ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme machache kwanza kwa kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa katika kipindi hiki ambacho tumetimiza miaka 50 ya Uhuru. Mengi yamefanyika, sote ni mashuhuda. Nchi yetu hii wakati tunaichukua, kwa maana ya kupata Uhuru, tulikuwa na maendeleo duni kabisa. Lakini sasa hivi tumeweza kupata maendeleo makubwa sana. Nianze na sifa tuliyoiopata katika ujenzi wa barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za nchi ya Tanzania Bara, tukiiacha Zanzibar, ukubwa wake unavuruga nchi ya Kenya, unavuruga nchi ya Uganda, hali kadhalika unaivuruga nchi ya Burundi ambayo ina watu 4,000,000 tu sawa na watu wa Wilaya moja ya Kinondoni. Haya tuliyoyafanya ni sifa kubwa na tuna haja ya kujipongeza. Hayo yanayosemwa, nawaomba wenzangu mliokuwa humu ndani, ni sawa na mvuvi anapokuwa baharini, akipishana na wimbi la nyuma hana habari nalo anasonga mbele. Kwa hiyo, sisi kejeli na bughudha zao tusizitilie maanani, la msingi tuangalie

tulichokifanya ni kitu gani na tunataka kufanya nini kuleta maendeleo katika nchi hii.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na madaktari tisa tu, sasa hivi madaktari mpaka wanafanya kazi nchi za nje. Tulikuwa na walimu wachache, sasa hivi kila Kata ina walimu pamoja na upungufu uliokuwepo. Sasa haya ndugu zangu ni mambo ya kujivunia, usipojisifia mwenyewe akusifu nani? Niwaombe ndugu zangu, haya tuliyoyafanya ni mwanzo wa maendeleo na pia tuhakikishe tunayaendeleza, tusibweteke.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipi kifanyike? Serikali ili kuyaendeleza haya, niwaombe sana tuweke mkakati madhubuti wa kufuatilia mambo haya ili tusiweze kurudi nyuma. Kwa maana ya kwamba kuwe na usimamizi madhubuti na uadilifu wa kutosha. Tunapopeleka maendeleo katika mikoa na wilaya zetu, basi ni muhimu sana tuhakikishe pesa zinakwenda kwa wakati na watekelezaji wanasimamiwa na kufanya kazi kwa wakati, hili jahazi ni letu sote. Madiwani wapo wanafanya hizo kazi, Wabunge ndio sisi, bila kujali itikadi ya vyama vyetu, litakapooza tumeoza sote; niwaombe tuwe wasimamizi wazuri na waadilifu wazuri kwa kuweza kutekeleza haya yote tuliyokuwa tumeyafanya ili tuweze kuendelea.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi nyingi zinatolewa, wafadhili wengi wanakuja na ahadi nyingine huwa zinatokea humu ndani ya Bunge, wakati tunapouliza maswali. Lakini utekelezaji wake ninaomba sana kama itawezekana, tuna Kamati nyingi, si vibaya tukaunda Kamati ambayo itasimamia ahadi za Mawaziri wetu wanazozitoa katika maeneo yetu ya kazi. Kwa sababu tukishazisimamia tutajua upungufu upo wapi, tumuwijabishe nani ambaye hakutekeleza hizo ahadi kwa wakati unaotakiwa. Kwa sababu sasa hivi kilichobaki ni kwamba tunapeleka maendeleo mbele zaidi, kama ilikuwa mara 100 basi iwe mara 1,000. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie suala la kutengeneza Kamati ambayo itasaidia kutathmini na kuangalia zile ahadi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Mawaziri, katika Bunge hili na hata huko nje wakati wanapofanya kazi zao.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nirejee katika Mkoa wangu. Nitakuwa mchache wa fadhila kama sikuishukuru Serikali kwa maendeleo ambayo angalau yametusogelea. Mafia, tumejata gati karibu litakwisha, uwanja wa ndege tunatarajia nao utamalizika; yote haya ni maendeleo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wake. Rufiji, hali kadhalika kuna maendeleo ambayo yamepatikana, Mkuranga, Bagamoyo, Kisarawe; nakumbuka katika kipindi kilichopita kila nikisimama nilikuwa naomba, jamani unapokuwa karibu na waridi basi na wewe unukie! Tunashukuru, umeme tumeona nguzo zimefika Kisarawe, tunachoomba sasa tathmini kama imekamilika watu walipwe pesa zao, nguzo za umeme ziwekwe, umeme nao ufike, hali kadhalika shida ya maji ambayo imetukabili, tunaomba nayo iweze kupatiwa ufumbuzi.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo yanaletwa na sisi wenyewe. Lakini pia na sisi inabidi tuangalie nani zaidi ana mchango mkubwa katika maendeleo haya. Naomba mniwie radhi katika hili kwa sababu, ninazungumza na ninataka niwatetee wanawake

wenzangu. Sehemu kubwa ya kilimo ambayo ndio sehemu kubwa ya Mkoa wa Pwani, walimaji wakuu ni wanawake wakisaidiwa na akinababa na vijana. Sasa ili tuwawezeshe wanawake hawa, nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkoo katika hotuba yake ameelezea kiasi gani cha pesa ambacho imetenga kwa ajili ya kuinua na kuibua miradi ya akinamama. Lakini kwa kuwa tuna ardhi kubwa, tuna bonde kubwa la kutosha, ni vyema tukatumia wahitimu wa Vyuo Vikuu vya Kilimo, wengi wanatoka kwenye Vyuo vya Kilimo, hawana kazi! Wapeni mikopo akinamama, wapeni ajira hao wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo, wahakikishe kila mama anayelima katika kila heka yake moja atakayouza mpunga; mimi nazungumzia mpunga kwa sababu Mswahili chakula chake kikuu ni mpunga na ndio kilimo kikuu cha kule Mkoa wa Pwani na tuna mabonde mengi sana na bahati nzuri akinamama ndio wanaohodhi hiyo ardhi na Wasukuma waliokuwa kule na Wanyamwezi ndio vibarua wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba muwasaidie hawa akinamama kuwapa mikopo na katika mikopo hiyo mtakayowapa, itawasaidia kutoa ajira kwa wale vijana ambao watakuwa wamemaliza kwenye Vyuo Vikuu. Kila heka moja katika heka 400, wapewe akinamama na katika kila heka moja yule mama atakapolima atatoa magunia sio chini ya 20. Kila gunia moja atoe shilingi 5,000/= tu, katika heka 400 kuna magunia mangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi ngapi zimepatikana na watu wakapewa mshahara? Taaluma gani tuliyoweza kuitumia na wale waliohitimu vyuo, watajiona kwamba hawakuachwa peke yao; wamepata ajira na kazi wanafanya na kilimo kiko pale pale, hali kadhalika chakula tena tutakuwa sio omnia omnia. Wala hatutaagiza chakula nje, badala yake tutaaagiza mpunga kutoka Rufiji, mpunga kutoka Bagamoyo, mpunga kutoka Kisarawe na kipeleka katika maeneo mengine ambayo hayana vyakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia tuna watoto wengi, vijana wengi wanaomiliza darasa la saba, *form four* na *form six*, hawana ajira. Ombi langu, vijengwe Vyuo vya Ufundu katika hizo Wilaya, vikishapatikana hivyo Vyuo vya Ufundu, tusikurupuke; tuangalie kwa mfano Kisarawe tunalima mihogo, katika mihogo tunayolima basi ufundu utakaotolewa pale ni jinsi gani ya kuweza kuuchakachua ule muhogo upatikane unga, makopa na kadhalika, ile inakuwa ni ajira tosha! Ukienda Rufiji unakuta wao ni wavuvi wa samaki, ukienda Mafia unakuta wao ni wavuvi wa samaki, kwa hiyo, na wao wapewe taaluma itakayolingana na wilaya zao. Ndani hapo hapo katika hizo wilaya, tayari tumepata Vyuo vya Ufundu, tayari tumepata ajira kwa vijana, tayari tumeweza kupata soko la kuweza kununua mazao yanayozalishwa na wakulima katika maeneo yale. Hili likifanyika, nina hakika tutapunguza vurugu za vijana. Tatizo kubwa la vijana ni ajira, laiti tukipata ajira ya namna hiyo, itatosha. Niwaombe sana Serikali, mliangalie kwa makini suala hilo bila kulipuuza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaobeza Uhuru wa nchi hii; jamani, humu ndani nani hakusoma baada ya kupata Uhuru? Sote timesomesha kwa hela ya nchi hii! Wapo watu wachache, wapinzani leo wanasema wao hawaoni faida ya miaka 50 ya Uhuru, nataka niwaulize! Kama si kaka yangu, mdogo wangu Kabwe Zitto, Kafulila, sijui...

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hao hao!

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hao hao eeh! Hao wote, wamesomeshwu kwa hela ya Tanzania. Labda Mheshimiwa Mbewe, kwa kuwa yeye, aah, basi niachie hapo hapo, Itakuwa namzungumza mtu. (*Makofi*)

Lakini naomba niyazungumze hayo ili nisiwe na mimi, kuna Mheshimiwa mmoja humu ndani alisimama akasema ndimi mbili, sasa sijui maana hii maana yake ndimi mbili au kitu gani? Sisi tunazungumza ukweli, hatuna haja ya ndimi mbili. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali, tunashukuru viongozi wa nchi hii waliotuletea Uhuru hadi leo hii akina Zaynabu Matitu Vullu, tumesimama ndani ya Bunge hili, tunatetea hoja, tunatetea maslahi ya nchi na tunahakikisha waliokuwepo wataendeleza na tutapata maendeleo yakutoshua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuliangalie hilo na pia narudia tena naomba sana miradi iangaliwe kwa akinamama ili wawezeshwe, tukomeshe unyanyasaji wa wanawake. Wako wanaume wanaopigwa na wake zao kwa sababu, hawana uwezo! Kwa hiyo, ninaomba sana hili, litasaidia hata Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, itakuwa haina kesi wala hizo Sheria hatutazidai sana. Tunaomba tuliangalie hilo ili tuwakwamue wanawake kimaendeleo. Asanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba maendeleo yaongezeke. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Vullu, ingawa nilitegemea hapo Wasukuma wataomba Mwongozo, lakini hawakufanya hivyo, kwa hiyo, wamekubali. Tunaendelea, anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Eugen Mwaiposa na baadaye Mheshimiwa Catherine Magige, atafuatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwaiposa? Mheshimiwa Mwaiposa, simuoni! Mheshimiwa Catherine Magige.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza, ningependa nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kuongoza Tanzania. Pili, napenda kuwashukuru Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi na Baraza la Vijana wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Arusha, kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao. Kwa uweza wa Mwenyezi Mungu, nina imani nitawatumikia kwa kadri niwezavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninapenda nichangie suala la ajira kwa vijana. Ajira kwa vijana imekuwa tatizo kubwa sana katika nchi yetu kiasi ambacho kinapelekea vijana wetu kujingiza katika uhalifu, kukaa vijiweni na mambo mengine yasiyo na msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuahidi kujenga VETA kwa kila Wilaya. Lakini pia naona hiyo haitoshi, ningeishauri Serikali ijenge VETA kwa kila Halmashauri ya Wilaya ingawa kujenga VETA moja ni gharama kubwa, ni shilingi bilioni sita kwa kila VETA, lakini ninaishauri Serikali ikiwezekana iingie mkataba na Mifuko ya Pensheni, itusaidie kujenga VETA kwa kila Halmashauri, *then* tuje kuwalipa kutokana na Bajeti yetu ya kila mwaka. Mitaani kuna vijana wengi ambao wamemaliza Vyuo vya Ufundı Stadi na kuna vijana wengi waliomaliza Chuo Kikuu, hawana ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunajitahidi kupunguza tatizo la ajira, lakini vijana wengi ambao wapo mitaani hawana ajira inatakiwa Serikali iwawezeshe wale vijana. Kama ni mafundi ujenzi, wanapomaliza chuo inabidi wapatiwe vifaa vya kuanzia, ikiwezekana wapewe mikopo. Pia kwa vijana ambao wanamaliza Chuo Kikuu, inasikitisha sana kuona matangazo mengi ya kazi yanataka uzoefu, labda uzoefu wa miaka miwili, mitano! Lakini kwa vijana wetu ambao wanamaliza Chuo Kikuu, uzoefu huo wataupata wapi? Ninaomba sana Serikali ijaribu kuangalia upya, iongee na waajiri, wawe wanawachukua vijana wetu waliomaliza vyuo kutokana na taaluma zao na wakifika huko maofisini, wawape *training*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda kuchangia suala la magereza. Nilipata nafasi ya kutembelea Magereza ya Mkoa wa Arusha ya Kisongo. Kwa kweli hali ya magereza katika nchi yetu inasikitisha sana. Niliongea na wafungwa, niliongea na mahabusu; mahabusu wanakaa gerezani zaidi ya miaka kumi bila kuhukumiwa! Ninaomba Serikali ijitatihidi kuliangalia suala hili, wahalifu wanapokosa inapofikia wamepelekwa Mahakamani, hukumu zao zitolewe mapema waanze kutumikia kifungo kuliko kuaweka mahabusu miaka mkingi bila hukumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafungwa. Wafungwa wana matatizo mengi sana gerezani. Nilisikita sana, nilikutana na wafungwa wawili, mmoja mzee ana miaka 83 na mwagine ana miaka 85, wazee wale wamehukumiwa kwa kosa la ubakaji. Mmoja amehukumiwa mwaka jana na mwagine mwaka huu, wamehukumiwa miaka 30, mzee wa miaka 85! Wazee wale hata kusimama hawawezi, kutembea hawawezi, hata kuona hawaoni vizuri, lakini wamehukumiwa kwa kosa la ubakaji! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ijaribu kuangalia matatizo kama haya. Wale wazee walinigusa sana, nikajaribu kuuliza lakini nikapata taarifa kuwa wale wazee walikuwa wana kesi na ndugu zao ya kugombea mashamba, wakasema ngoja tuwaweke huko ndani ili sisi tuuze mashamba. Hatutafika kwa hali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea kuhusu hawa wafungwa. Wafungwa wanapata milo miwili kwa siku. Wanapata uji saa 12.00 asubuhi na chakula cha mchana wanapata saa 8.00 mchana, wanaingia kulala mpaka kesho yake asubuhi. Kwa kweli wafungwa wanahitaji haki kama sisi ingawa wenyewe wapo huko wanatumikia kifungo. Nadhani hiyo ni dhana ya zamani, naomba Serikali ijaribu tena kuangalia upya suala la wafungwa angalau wapatiwe milo mitatu kama sisi wengine ambao tuko uraiani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa ninaomba Serikali iangalie ni jinsi gani itawaruhusu Waandishi wa Habari angalau wawe wanatembelea gerezani hata mara mbili kwa miezi miwili. Nadhani Waandishi wa Habari wakiwa wanatembelea gerezani na kujaribu kuongea na wafungwa, italeta haki kiasi fulani na uwajibikaji katika magereza yetu. Kwa sababu hata mimi nilipotembelea gerezani, waandishi wa habari walikatazwa kabisa kufika katika lile eneo la gereza, sasa kule gerezani sijui kuna kitu gani ambacho kinafichwa? Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie upya ni jinsi gani Waandishi wa Habari, watakuwa wanapata muda wa kwenda kuwatembelea wafungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa ninaomba Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuwasaidia wafungwa mara baada ya kumaliza kutumikia kifungo chao. Wafungwa wamekuwa wakimaliza, kwa mfano labda mfungwa anakaa Dodoma anatumikia kifungo chake Arusha, wamekuwa wakitoka wanapewa tu nauli ya kuwafikisha majumbani mwao. Lakini mimi naona hii inazidi kuhatarisha usalama wetu, kwa sababu mfungwa anapofika kwenye mkoa wake hajui pa kuanzia. Unakuta mfungwa amekaa miaka 20, 10, 30, anapofika katika mkoa wake, hana pa kuanzia! Kwa sababu hajui ataanzia wapi, amekaa ndani muda mrefu, kwa hiyo, Serikali ijaribu kuangalia ni jinsi gani itawasidia wafungwa mara wanapomaliza vifungo vyao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hotuba ya Waziri Mkuu, alisema wataangalia ni jinsi gani ya kupunguza vifungo. Gerezani kuna watuhumiwa ambao wamehukumiwa kwa makosa ambayo ni madogo ambayo wanaweza wakapangiwa hata shughuli za kijamii wakazifanya badala ya kwenda kujazana magerezani. Unakuta mfungwa labda aliongea tu kwa nguvu nje ya Mahakama, lakini amehukumiwa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iliangularie suala hili. Pia nilikuwa naomba Serikali iangalie ni jinsi gani itawashirikisha wafugwa katika kuchangia katika kuunda Katiba Mpya, nadhani wafungwa wana haki ingawa wako kule wanatumikia kifungo lakini Serikali inahitajika kuwafikiria wafungwa nao ili washiriki katika kuchangia Katiba Mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu wakinamama, nilikuwa naomba Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuwasaidia wanawake wenye matatizo, naweza nikatolea mfano kuna mwanamke mmoja mkoa wa Arusha anaitwa Chausiku, yule mwanamke ana matatizo makubwa sana alizaa watoto 18 wengine wakafariki, lakini yule mwanamke anasumbuliwa na tatizo la kupata ujauzito hata asipokutana na mume wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mama nilipoenda kumtembelea nilimkuta ana ujazito wa miaka miwili, mama yule ana hali mbaya, hawezo hata kusimama anatembea kidogo anasumbuliwa na mgongo na hata akienda kujifungua huwa anabakia na mimba ya miezi miwili, kwa hiyo, amezunguka sehemu nyingi hospitali bado ana tatizo hilo. Naomba sana Serikali ijitahidi kuangalia wanawake wenye matatizo makubwa wawatafutie madaktari hata ikishindakana wawapeleke nje ya nchi kutibiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea wodi ya akinamama ya hospitali ya *Mount Meru* katika Mkoa wa Arusha, hali niliyoikuta kule kwa kweli inasikitisha sana nimekutana na wanawake wanne wanaumwa uchungu wote kwa pamoja, uchungu wa kujifungua lakini wamelala katika kitanda kimoja kwa hiyo, pale ni vurugu, kusukumana wanawake wanne wote wanaumwa uchungu kitanda kimoja na bado wale ambao wamejifungua watoto wote wanalala kitanda kimoja. Naomba tuwape uzito akinamama na tuwasaidie, hospitali yetu ya Mkoa wa Arusha ya *Mount Meru* ili na wenyeve wapate vitanda vingi, Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi itafanyia kazi matatizo yote haya, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru huo ndiyo Ubunge, Mbunge lazima utembelee sehemu na ufanye utafiti halafu unakuja kueleza Serikali ndani ya Bunge, yaani naamini kwa yale ya magereza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu wake wameyasikia. Waheshimiwa Wabunge tuendelee. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi walau na mimi nichangie katika hoja ambayo ipo mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii vilevile kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini kwa imani yao kubwa walijonionyesha kwangu na kunipa kura za kishindo katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 31 Oktoba, 2010. Naomba niwaahidi kitu kimoja kwamba sitowaangusha, nitawatumikia kadri ya uwezo wangu na kwa nguvu ambazo Mwenyezi Mungu atanipatia katika utumishi wangu katika kipindi cha miaka mitano. Ombi langu kwao ni kwamba lazima tushirikiane, lazima tuwe wamoja ili tuweze kuleta maendeleo ya kweli kwa Jimbo la Morogoro Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jioni hii ya leo na mimi katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitumie nafasi hii vilevile kuwashukuru viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi, Wilaya na Mkoa wa Arusha, lakini vilevile niwashukuru viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Wilaya na Mkoa wa Arusha kwa muafaka ambao wameufanya katika Halmashauri ya Jiji na Wilaya ya Arusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya ambayo yamefanyika, Zanzibar na Arusha ni kielelezo tosha kumbe kwamba maandamano, vurugu hazina tija, kitu stahiki kwa Watanzania katika kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zinajitokeza katika suala la maendeleo au katika suala la kutawala kukaa mezani ni hoja ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna sababu ya kufanya maandamano kwa sababu wakati wa kufanya maandamano lolote linaweza likatoka, kuna Mheshimiwa mmoja Mbunge wakati anachangia alizungumza neno moja namnukuu kwamba; “Kaka Mbewe endelea, tumewashika pabaya.” (*Makofi*)

Mimi ninachojua mtu akishikwa pabaya huwa hapigi kelele, ananyamaza kimya na akishikwa pabaya mtu anakuwa na hiyari ya kukubali. Lakini sisi kama Chama cha Mapinduzi, sisi kama wananchi tunapopiga kelele ya kuwaambia wenzetu maandamano hayafai, vurugu hazifai, tunachoogopa ni kwamba tutawapeleka pabaya Watanzania. (*Makofi*)

Leo hii tayari kwa maandamano yetu na uchochezi wetu wa kisiasa tulishawapeleka pabaya baadhi ya vijana pale Arusha wapo waliokufa, wapo waliopata vilema vyta maisha lakini vilevile katika uchochezi wetu na maandamano yetu tumeshawapeleka pabaya vijana wetu katika Vyuo Vikuu sasa hivi wapo nyumbani. Niwaombe sisi kama wanasiasa tuwaeleze vizuri wananchi wetu tuwaambie vizuri vijana wetu lakini kubwa tuwaambie Watanzania nini wajibu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimpongeze vilevile Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa katika Bunge hili wakieleza nini ambacho Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya katika mwaka uliopita, lakini nini ambacho Serikali ya Chama cha Mapinduzi kitafanya katika Bajeti ya Serikali ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kitu kimoja, kupongeza si kosa na katika kila jambo zuri ambalo litafanyika sisi kama wananchi, sisi kama viongozi na Wabunge tuna kila sababu ya kupongeza. Lakini vilevile tuna kila sababu ya kukosoa pale ambapo tunadhani ni makosa ambayo yanatupeleka kule ambako hatupataki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuiambie Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, TAMISEMI, kila siku katika vyombo vyta habari lakini vilevile humu ndani ya Bunge tumekuwa tukisikia ubadhilifu mkubwa ambao unafanyika ndani ya Wizara na Ofisi ya TAMISEMI. Serikali inajitahidi kila siku kushusha pesa na hata hapa tunapitisha Bajeti za Wizara mbalimbali tukishusha pesa ili ziweze kuleta maendeleo kwa wananchi. Ombi langu na naamini ndani ya kipindi kifupi nilichokuwa Mbunge nilichogundua katika Halmashauri kuna upungufu katika Sheria na Kanuni za kuwajibisha watendaji wazembe. Nadhani wakati umefika kuititia Bunge lako Mheshimiwa Mwenyekiti lakini kuititia Ofisi za Menejimenti Utumishi wa Umma na TAMISEMI hebu tuangalie upya sheria ambazo zimepitwa na wakati. (*Makofi*)

Ni imani yangu tukiweza kurekebisha sheria lakini ni imani yangu vilevile Waheshimiwa Wabunge katika kila siku katika hotuba zetu tumekuwa walalamikaji tu, tunajiona kwamba na sisi siyo sehemu ya Serikali, nataka niwaambie na sisi ni sehemu ya Serikali, kuna mapungufu ambayo katika utendaji wetu wengi hatushiriki katika vikao vinavyotuhusu katika Halmashauri zetu hii imepelekea watumishi katika Halmashauri kuwa wabadhilifu na kikubwa zaidi inaonekana kwamba watumishi wanaogopa Wabunge kuliko Madiwani katika Halmashauri zetu.

Niwaombe tutapeleka pesa katika Halmashauri basi ndani ya kipindi hiki na sisi kama Wabunge twende tukashiriki katika vikao vyetu katika Halmashauri zetu, ninaamini mwakani haya mambo ya CAG kusema kwamba kuna ubadhilifu kwenye Halmashauri lakini vilevile Kamati ya Kudumu ya Bunge inayokwenda kukagua Halmashauri kusema kwamba kuna upungufu hayatotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nianze kuchangia kwenye upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ambayo ndiyo Halmashauri ninakotoka kwenye Jimbo la Morogoro Kusini. Katika Bajeti ya Serikali ya mwaka jana Wilaya ya Morogoro Vijijini tumeazimia kwenda mahali ambapo tunatarajia kujenga Makao Mkuu ya Wilaya, Wilaya ya Morogoro Vijijini Makao Mkuu yatakuwa Mvuha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya mwaka jana tuliomba na tukapata shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Makao Mkuu ya Wilaya hiyo. Mwaka huu tumeomba tena shilingi milioni 500, lakini hatukupata pesa hiyo na tulipoomba tena tukaambiwa tuandike ombi maalum ili tuweze kufikiriwa. Nikuombe Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu tunadhamira ya kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini, Wilaya ya Morogoro Vijijini ambayo vilevile ina jimbo la Morogoro Kusini Mashariki. Utumishi wetu utakuwa wenyewe maana, utumishi wetu utakuwa uliotukuka kama tutakuwa ndani ya Wilaya ya Morogoro Vijijini, Makao Mkuu yakiwa Mvuha sasa hivi tuko Morogoro Mjini, inatuwia vigumu kufanya kazi kwa watumishi katika Wilaya ya Morogoro Vijijini kutembelea majimbo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri wakati utakapokuwa unafanya *wind-up* ya Bajeti basi walau nipate na njue nini ambacho Serikali inasema, dhamira yetu ni kufika kwa karibu kwa wananchi, tunataka twende Mvuha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nichangie vilevile katika upande wa barabara, ninaomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo imeifanya ya kuunganisha barabara nchi nzima, mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya, lakini kijiji kwa kijiji. (*Makofi*)

Naomba nitoe pongeze za dhati kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini na Morogoro Kusini Mashariki kwa uamuvi wa Serikali kuifanya barabara ya kutoka Morogoro ambayo inaitwa Bigwa Kisaki, kutoka Morogoro hadi Mvuha kuwa katika kiwango cha lami ambapo naamni sasa wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru watakuwa walau wamefurahi au kuona kwamba Serikali inawajali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii vilevile kupongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya katika sekta ya afya, wote tunajua ndani ya Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imesema kwamba katika kila kijiji tunahitaji kuwa na zahanati, kazi kubwa imefanyika na hata ndani ya Jimbo la Morogoro Kusini na Wilaya ya Morogoro Vijijini haya mambo yamefanyika hadi hivi sasa tuna vituo vitatu vya afya, lakini tayari tuna zananati 59. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambazo zinatukabili katika zahanati zetu, katika vituo vyetu vya afya ni upungufu wa wataalam kama madaktari wasaidizi, wataalam wa maabara ya meno na wauguzi. Lakini vilevile tuna upungufu mkubwa wa dawa, wananchi wanaomba Serikali yao na mimi kama Mbunge na mwakilishi wao naiomba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, hebu na sisi wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Wilaya ya Morogoro Vijiji tupatiwe wataalam hao kutoka kata ya Kisaki hadi Morogoro Mjini kwenye hospitali kuu ya mkoa ni kilomita 150. Ukosefu wa madaktari bingwa kwa kuweza kufanya upasuaji kwenye vituo vyetu vya afya umesababisha vifo vya akinamama na watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itusaidie kupunguza vifo vya akinamama na watoto, watupatie madaktari bingwa hao katika vituo vyetu vya afya vya Dutumi, Tawa na cha Ngerere. Lakini vilevile katika upande wa afya tuna tatizo kubwa la usafirishaji wa wagonjwa katika vituo vyetu vitatu vya afya tuna gari za *ambulance* mbili tu, jiografia ya Morogoro Vijijini ni ngumu, tunaomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ituongezee walau gari moja katika kila kituo cha afya kiwe na gari ya kubeba wagonjwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili Mheshimiwa Rais alipofanya ziara katika mkoa wa Morogoro alipotembelea zahanati ya Kiloka, aliahidi kutupatia gari la wagonjwa toka mwaka 2008 mpaka leo hii gari hilo hatujapata, niombe kupitia kikao hiki nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu basi atusaidie hilo gari tulipate ili liweze kusaidia kazi ambayo itatatura matatizo mbalimbali kama kwa wananchi kama Mheshimiwa Rais alivyoona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe nitumie nafasi hii vilevile kuipongeza Serikali kwa dharti toka sakafu ya moyo wangu kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kusambaza umeme katika nchi hii. Pamoja na upungufu ambao umejitokeza wa mgao wa umeme lakini dhamira ya Serikali ipo pale pale. Nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini kuipongeza Serikali katika mpango wake wa kupeleka umeme vijijini. Tayari nguzo tumezunga zilishafika mpaka kijiji cha Kibangire, tuna imani kabisa kwamba kama Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alivyoantuambia kwamba mpaka kufikia mwakani umeme utawaka. Niiombe Serikali kwamba mradi huu wa umeme wa Morogoro Vijijini ambao utaishia Kata ya Lundi, kilomita 10 kutoka Makao Mkuu ya Wilaya ambayo tunatarajia kujenga Mvuha Serikali ingeongeza fungu uende sambamba na kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya tunayotarajia kujenga kata ya Mvuha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, woga wangu kwa nini naiomba Serikali kuacha mradi huu ukaishia hapo ulipo na kwa kuwa ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba kila Makao Makuu ya Wilaya yanapata umeme tukija kuanza upya mradi wa kutoa umeme hapo ulipoishia na kupeleka Makao Mkuu ya Wilaya tutakuwa na kazi kubwa ya kuweka *mobilization*, lakini vilevile *sight establishment* ambayo itaiongezea gharama kubwa Serikali. Kwa hiyo, niombe tu utusaidie katika hilo. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kalogeris.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENG: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niwe ni mmoja wa wazungumzaji katika jioni hii kwene *agenda* muhimu ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana ambayo imeelezea ukweli na hali halisi iliyopo katika sekta mbalimbali ya nchi yetu. (*Makofi*)

Lakini nimesimama kwa furaha kubwa sana na nimesimama kwa heshima na kwa ujasiri mkubwa kwa sababu najivunia mafanikio yaliyopatikana katika nchi yetu na hasa katika jimbo langu la Makete. Ninadhani ipo haja niliseme hili kuitia jimbo langu la Makete na naamini wote mnafahamu hali halisi ya Makete ilivyokuwa huko nyuma na tatizo kubwa la janga la UKIMWI ambalo limeacha watoto wengi yatima ambao wamesaidiwa sana na Serikali hii ya Awamu ya Nne na katika msaada mkubwa Mheshimiwa Mwenyekiti, ambao Serikali hii itakumbukwa milele na wana Makete ni kujenga Chuo cha Ufundı cha VETA ambacho kitakamilika mwezi wa saba. Ni dhahiri kabisa kwamba watoto hawa sasa watapata nafasi ya kupata mafunzo pale na baadaye waweze kuwijiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hakuna ambaye hakujuu tatizo kubwa la barabara za Makete, barabara zilikuwa hazipitiki. Ilikuwa mwananchi wa Kata ya Matamba akitaka kwenda mjini Makete ni lazima aende Igawa, Makambako na Njombe ndiyo aje Makete, anazunguka kukwepa kilomita 55 kwa sababu barabara hazipitiki lakini leo zinapitika. Ilikuwa wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete wakitaka kwenda Matamba ni lazima waende Njombe, Makambako na Chimala ndiyo wafike Matamba kwene Kata kisha watoe huduma, lakini leo tendo hilo halipo. Leo barabara zote zimefunguliwa mabasi yanapita kutoka Njombe mpaka Makete na kutoka Makete yanakwenda mpaka Mbeya. Mabasi ni mengi tunachotaka wenzetu waendelee kuongeza mabasi ili watu wasipate taabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tulikuwa na tatizo la umeme, ni kweli hatujamaliza kutatua lakini kuitia miradi ya MCC leo tayari wananchi wa Tandala wameanza kulipwa fidia, umeme utakaosaidia vijiji vya Ndulamo, Kisinga, Lupalilo na Tandala. Haya yote ni mafanikio yanayotakiwa kuenziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonuma sana ni pale wenzetu wanapokwenda Makete ambako kulikuwa hakufikiki miaka ya nyuma wamepita kwenye barabara zile zilizojengwa na Serikali ya Awamu ya Nne wakifika Makete wanasema hawaoni kitu wakati wamepita kwenye zile barabara hawakuruka angani, wamepita kwenye barabara ambazo zimetengenezwa na Serikali ya Awamu ya Nne. Lakini

wameweza kuzunguka nchi nzima kwenye mtandao wa barabara zilizojengwa na Serikali ya Awamu ya Nne.

Kwa hiyo, Serikali ya Awamu ya Nne imewapa demokrasia ya kuwawekea miundombinu ili wakatoe sera zao lakini wakifika kule wanatukana. Nataka niwaombe wananchi wangu wa Makete kwamba wasisahau msemo unaosema msafara wa mamba haukosi kenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishukuru sana Serikali kwa mkakati wake wa kuendeleza Nyanda za Juu Kusini *SAGCOT* yaani *Southern Agricultural Growth of Tanzania*, nawapongeza sana. Lakini ninachoomba kwenye mkakati huu basi tuisahau kujenga masoko makubwa kama yale ambayo yalikuwa yamebuniwa Makambako ili baadaye haya mazao yakipatikana Nyanda za Juu Kusini yasijengwe masoko nje ya kule ambako ni mbali na itakuwa ni vigumu ku-realise hilo. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niishukuru Serikali kwa mradi mkubwa wa Mchuchuma na Liganga. Tumesikia mara nydingi lakini tunaamini Serikali yetu sasa hivi imefikia mahali itakamilisha mradi huu na utakamilika kabla ya mwaka 2015. Nataka niishukuru Serikali kwa miradi yetu ya kufua umeme ile nane na hasa ukiwemo wa Ruhuji ulioko Njombe na ule wa Lumakali uliopo Makete na niwaombe wataalamu wa *TANESCO* kwamba Mito ya Ruhuji na Mito ya Rumakali ni mito ambayo haikauki wala haipungui maji kwa sababu mvua katika maeneo yale zinaonesha miezi nane kwa hiyo, kina cha maji kwenye mito ile haipungui kuogopa kwamba maji yatapungua waache.

Chanzo cha maji cha Rumakali kinatoka Kitulo ambapo tayari kuna Hifadhi ya Kitulo kwa hiyo, yale maji yanahifadhiwa vizuri. Nawaomba wenzetu walione hilo, waharakishe na kwa sababu ule Mto wa Rumakali tayari wameshasaini *memorandum of understanding*, tunaamini kwamba hii inaweza ikaenda haraka zaidi na umeme ukaanza kuzalishwa wa *megawatt* 222. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya niingie kwenye sehemu ya pili na ninaomba niongelee suala la barabara za vijijini. Tumejenga barabara kuu nydingi sana na zinaendelea kujengwa na tunaipongeza Serikali yetu. Lakini ili barabara hizi kubwa ziwe na manufaa ni lazima tutengeneze barabara za vijijini, barabara za vijijini ndiyo *engine* ya uchumi wa nchi hii na nchi nydingine mahali popote pale. Pale utakapofikisha barabara kijijini utakuwa umewahakikishia wananchi wa kijijini kwanza kupata huduma za kiafya na kupata huduma za elimu bila matatizo, lakini vilevile kutoa mazao yao kutoka kijijini na kuyapeleka kwenye soko mahali panapotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mfumo ambao tunatumia kujenga barabara hizi sasa hivi bado haujaleta mafanikio. Ninazo takwimu ambazo naomba nizitumie kwenye Jimbo langu la Makete kwamba mwaka 2006/2007 tulipewa shilingi milioni 147, mwaka 2007/2008 tulipewa shilingi milioni 243, mwaka 2008/2009 tulipewa shilingi milioni 268 na mwaka 2009/2010 tulipewa shilingi milioni 494. Kwanza niishukuru Serikali kwa sababu kama unavyoona pesa zimekuwa zikiongezeka kwa hiyo, hii ni Serikali sikivu,

inapanga mikakati yake na inawapenda watu wake. Lakini kuna tatizo kwamba hizi barabara pamoja na hela zote ambazo zinafikia karibu shilingi bilioni 1.5, bado barabara zile za vijijini hazipitiki. Kwa hiyo, nadhani inabidi tuangalie upya mfumo tunaoutumia kusimamia ujenzi wa barabara hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo ninapoleta pendekezo kwamba barabara za *TANROADS* za Wakala wa Mkoa tunazisimamia vizuri kwa sababu tunahoji Mkoani na tunahoji hapa Bungeni. Lakini barabara za vijijini zina nafasi moja tu kwenye Halmashauri, naomba basi mfumo amba ni bora kuliko vyote ni vizuri tukaunda Wakala wa Barabara za Vijijini yaani *Rural Roads Development Agency* na hiki siyo kitu kigeni hata wenzetu wa India wanatumia utaratibu huu. Hii itatusaidia kwanza kuwa na mtandao unaoeleweka wa barabara zetu lakini vilevile tatizo mojawapo ambalo linafanya hizi barabara zisitengenezwe kwa kiwango kizuri ni kwa sababu zile fedha ni kidogo kwa hiyo, zinapokuwa kidogo wakandarasi wanaokuja kupata kazi ni wale amba hawana uwezo mzuri kwa sababu mwenye uwezo mzuri hawezi kwenda kuchukua hizi fedha ndogo.

Kwa hiyo, tunadhani tukiwa na Wakala hizi fedha zitaunganishwa na anawenza akapewa Mkandarasi mmoja mwenye vyombo vizuri na akawenza kujenga barabara hizi vizuri. Hiyo ni hoja yangu ya pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ni kuhusu umeme vijijini. Hoja yangu hapa na wenzangu wote ni mashahidi, mimi nina wasiwaso kwamba mfumo amba tunautumia wa kufuatilia utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na *TANESCO* na ile inayosimamiwa na wenzetu wa *REA* bado haujawa wazi. Kwa mfano, mimi katika uzofu wangu wa miaka mitano hakuna siku nimeona kwenye Baraza la Madiwani tumejadili mpango wa usambazaji wa umeme katika Wilaya. Hakuna siku kwenye vikao vyetu vya *RCC* tumejadili kuhusu mpango wa usambazaji umeme katika ngazi ya Mkoa, hawa watu huwa wanaalikwa katika ngazi ya Mkoa na katika ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, ile *ownership* ya usambazaji wa ule umeme iko kwao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninashauri kwamba ni vizuri wenzetu wa *TANESCO* wakawajibika na wakawa wanatoa taarifa kwenye Baraza la Madiwani lakini vilevile katika ngazi ya Mkoa napo watoe taarifa na tuweze kuwapa vipaumbele ambavyo tunadhani labda kama ingefaa katika mkoa wetu ama ule Mkoa au katika Wilaya. Hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye eneo la umeme ni kweli tunajua kwenye maji kuna tatizo kwani yanaweza yakapungua na siyo chanzo kizuri cha kufua umeme, lakini iko mikoa ambayo ina mito mingi sana ikiwemo Mkoa wa Iringa na hususani Wilaya ya Makete, ina vyanzo vingi ambavyo unaweza kufua umeme na wananchi wakautumia lakini baadaye uliobaki ukaingizwa kwenye Gridi ya Taifa na yale maji hayakauki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tufahamu kwamba ili kuweka umuhimu wa barabara hizi tutakazokuwa tumezijenga vijijini *complementary infrastructure* ni umeme kwa sababu ukishapeleka umeme mahali ambapo barabara inapitika, una maana

kwamba wananchi hawatasaga mahindi kwa kutumia mashine zinazotumia dizeli badala yake watasaga mahindi kwa kutumia mashine zinazotumia umeme. Lakini vilevile kutakuwa na vioski na sehemu mbalimbali ambazo zinatumia umeme.

Kwa hiyo, ninashauri kwamba kwanza Serikali pamoja na miradi mingine yote ijielekeze kwenye miradi ya umeme wa maji ambaa unaweza ukawasaidia na kuwafikia wananchi walio wengi. Lakini vilevile Serikali iendelee na mikakati yake mikubwa ya kufua umeme ili kukidhi mahitaji ya Taifa ambaa umekadiriwa kufikia 2,780 tufikapo kipindi cha kwanza cha miaka mitano ambayo mimi naipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Jimboni kwangu naomba sekta ya mawasiliano kwani hiyo ni muhimu sana pale inapokuwa barabara na umeme zimefika, mawasiliano ni muhimu. Katika Jimbo langu kuna Kata za Ikuwo na Mang'oto ambazo maombi yake nimeshampelekea Mheshimiwa Waziri na ameyapokea vizuri, anayafanya kazi. Nina hakika kwamba baada ya muda mfupi wananchi wangu wa Ikuwo watapata mawasiliano mazuri. (*Makofi*)

Ombi langu lingine ni kwamba kama mnavyojuu mazingira ya Makete ni magumu kwa hiyo watumishi ni wachache. Ninaomba Serikali kwa kuanzia itusaidie kupeleka watumishi katika sekta ya afya, pengine kwa sababu watu wanaogopa kwenda Makete kwa sababu ya kuambiwa tu. Basi ninaomba mtupe nafasi sisi Wanamakete tuna vijana wetu waliomaliza *form four*, wapewe nafasi wakasomee uganga ili wafanye kazi kule jiboni Makete. Hili namuomba Mheshimiwa Waziri alifikirie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho mimi naendelea kuipongeza Serikali yangu kwa kazi nzuri inayofanya na ninawaomba vijana wetu wa Vyuo Vikuu, sisi tumefika hapa ndani kwa sababu tulipata elimu nzuri. Elimu nzuri haiwezi kupatikana kwa migomo, nchi haiwezi kuendeshwa na maandamano, hatuwezi tukamsikia mtu amesimama humu ndani ameonyesha uzoefu wa migomo wa miaka ya 1964, ule uzoefu hauwezi kutusaidia leo, hatuhitaji migomo. Leo hii wanaoathirika ni watoto wetu, akigoma atakaporudi chuoni ataambiwa afanye mtihani, vipindi vimepita muda wake kwa hiyo, anapata elimu nusu nusu. Pia niwaombe wanasiasa ambaa wanapenda kupandia ngazi Chuo Kikuu cha Dodoma waache huo mchezo, wanaharibu watoto wetu, pale ni mahali pa elimu na niwaombe wote tumuunge Makamu Mkuu wa Chuo Mheshimiwa Profesa Idrisa Kikula alivyosema kwenye toleo lake juzi kwamba wanasiasa msiende kule ili watoto wasome. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapa mimi nakushukuru na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushuru sana Mheshimiwa Mahenge kwa mchango wako na sasa nitamuita mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo naye atakuwani Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid. (*Makofi*)

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa kuteuliwa tena kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa na Bunge hili Tukufu. Pia napenda nichukue fursa hii kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama niwashukuru wapiga kura wangu ambao ni vijana wa Mkoa wa Dar es Salaam na pia Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia hotuba ya Waziri kwa kuanzia na sekta ya afya. Napenda kuzungumzia sekta ya afya katika sehemu ya huduma ya afya ya uzazi kwa vijana kwani 64% ya Watanzania ni vijana ambao wako kati ya umri kati ya miaka 14 - 25 hivyo naona kuna umuhimu wa kulinda afya za vijana hawa. Nashukuru sera za sasa zilivyoweza kuweka kipaumbele kwa vijana lakini pamoja na hayo yote bado kuna changamoto nyingi ambazo zinatukabili vijana katika suala zima la huduma ya afya ya uzazi na kukosekana kwa huduma rafiki katika suala hili la huduma ya uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma rafiki katika suala la huduma ya afya ya uzazi ni 30% tu ambayo inapelekea 50% ya vijana tunaongoza katika kupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa na pia hatari ya kupata na kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ninaomba Serikali katika suala zima la kutoa huduma rafiki katika suala hili la huduma ya uzazi kwa vijana iweze kuangalia mambo muhimu pamoja na mazingira mazuri ya kutolea huduma. Vijana wanapokwenda sehemu ya kutolea huduma waweze kupata vifaa na pia waweze kupata huduma kwa muda muafaka vilevile wale watoaji wa huduma wawe wanaendana na vijana wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nzungumzie suala la chanjo ya kansa ya shingo ya uzazi. Ninaomba Serikali iweze kutupatia vijana chanjo ya kansa ya shingo ya uzazi kwa kuwa ugonjwa huu ni hatari sana na unahatarisha maisha ya Watanzania wengi ukizingatia kwamba asilimia kubwa ya Watanzania ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza na kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kupunguza vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi kutoka 578 hadi 454 mwaka 2007/2008 hadi mwaka 2009/2010. Lakini 15% ya vijana wenye umri kati ya miaka 14 - 19 ambayo ni *adolescence age* wanaolewa na vijana hawa wanatakiwa wapate ujauzito. Hivyo basi, ninaomba Serikali iangalie na kupitia mila zetu na kuweza kuwakinga vijana hawa wasiweze kupata matatizo wakati wa kujifungua na ikiwezekana ile Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 iweze kurekebishwa au kufutwa kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nzungumzie suala la ajira kwa vijana. Katika suala la ajira kwa vijana napenda niipongeze Serikali kwa jitihada kubwa ya kuweza kutupatia mikopo vijana wa elimu ya juu ambayo takribani shilingi bilioni 185 ambayo walipatiwa vijana 96,328. Pia napenda kuipongeza Serikali kwa jinsi inavyoendelea kuwawezesha wananchi katika kuongeza ajira kupitia sera, mikakati na programu mbalimbali ambazo zitawasaidia wananchi katika kupata ajira. Lakini kwa

masikitiko makubwa napenda kusema kwamba katika sera hizo mipango na mikakati hiyo sijaona sehemu ambayo kijana ametajwa moja kwa moja. Hivyo basi, bado naona kuna changamoto kubwa kwa vijana katika suala zima la kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda ku-*declare interest* kwamba nilipokuwa namaliza Shahada yangu ya Kwanza nikaamua niunganishe Shahada ya Pili. Baada ya kurudi mtaani na kuanza kutafuta kazi, kwa kweli ilinichukua takribani miaka miwili sikuweza kupata kazi. Nilipojaribu kuomba kazi ngazi ya Afisa katika ofisi mbalimbali walikuwa wanafikiri kwamba labda huyu mtu tukimuajiri katika ngazi ya Afisa anataka tu kupata uzoefu na kisha baadaye atukimbie. Nilipojaribu kuomba ngazi ya Meneja walikuwa wanahitaji mtu mwenye uzoefu wa miaka kumi, kazi nyingine uzoefu wa miaka nane na nyingine miaka saba. Sasa kijana wa Kitanzania ambaye anamaliza shahada yake akiwa na miaka 22 au 23 au 25 uzoefu huu wa kazi *ten years* atatoa wapi wakati ndio kwanza anaanza kutafuta kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naiomba Serikali iweze kutujengea uzoefu vijana kuanzia katika shule za msingi/awali ikiwezekana iweze kufundisha masomo maalum ambayo yatawajengea uwezo vijana katika suala zima na kujenga dhana ya kujiajiri zaidi ya kuajiriwa. (*Makofi*)

Pili, ninapendekeza kwa vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu Serikali ichukue CV zao na kuwatafutia kazi katika mashirika au makampuni ambayo yanakuja kuwekeza hapa nchini ambayo yanapitia kwenye taasisi za *TIC* na *EPZ*. Kwa kuwa makampuni ya kigeni yanapokuja kuwekeza hapa nchini ni lazima yapitie Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Kazi kwa ajili ya kuwapatia vibali wafanyakazi. Hivyo basi, ninaiomba Wizara ya Kazi kupitia mwanya huu iweze kuwapatia kazi vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu. Hoja yangu ni kwamba kama ni sheria ileteni Bungeni tuipitishe ili kuweza kuwapatia ajira vijana wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Napenda kuipongeza Serikali kwa kutengeneza barabara nyingi na kwa kutengeneza madaraja mengi hapa nchini.

Lakini bado katika Jiji la Dar es Salaam kuna changamoto kubwa sana ambayo inapelekea kuwa na msongamano mkubwa wa magari kiasi cha kuwafanya watu kuchelewa kufika ofisini, vijana kuchelewa kufika shulen na hivyo inapunguza ufanisi wa kazi na pia kupunguza nguvukazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga shule za sekondari nyingi za Kata katika kila Kata hapa nchini. Lakini napenda kuikumbusha Serikali kwamba shule za msingi nyingi zipo katika hali mbaya hivyo zinahitaji uboreshwaji na kufanyiwa ukarabati. Kwa mfano, shule za Mkoa wa Njombe kwenye vijiji kama vya Duram, Parangarano, Ifanya, Masimbwe, Kilolo na kadhalika. Shule zipo kwenye hali mbaya sana hivyo tunaomba ziweze kufanyiwa ukarabati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalize kwa kusema kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki ina Baraza la Vijana la Afrika Mashariki hivyo basi naiomba Serikali na sisi vijana wa Tanzania tuweze kuwa na Baraza la Vijana Tanzania ambalo halitaangalia itikadi ya chama chochote ili tuweze kupata nafasi ya kwenda kuzungumza, kushauriana na kubadilisha mawazo na vijana wenzetu ambao wako kwenye Baraza la Afrika Mashariki, kwa kupata nafasi hiyo tutaweza kujua changamoto nyingi zinazokabili nchi za jirani kwa upande wa vijana na jinsi gani ya kukabiliana nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mwongozo, Kifungu cha ngapi?

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 68(7) kinasema; “Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba “*Mwongozo wa Spika*” kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatorewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji aliyejita amezungumza kwamba kuna mama mmoja ambaye anapata ujauzito bila kukutana na mwanaume. Jambo hili ni kinyume kabisa na sayansi na Watanzania wanasilia linaweza likasababisha upotoshaji sana katika Taifa letu. Ninaomba Mwongozo wako. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ni kweli Mheshimiwa Catherine Magige alilisema jambo hili lakini mimi ni mara yangu ya pili kulisikia maana nilishasoma kwenye vyombo vyahabari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mbunge, sasa mimi nadhani mwongozo wangu ni kwamba kwa sababu ye ye amefanya utafiti, amekwenda akauliza na akaambiwa, mimi nadhani na wewe ufanye utafiti nenda na wewe kamuulize kwa sababu mhusika yupo Arusha, nenda na wewe kafanye utafiti na wewe pengine utakuja na *observations* zako. Kwa hiyo, Mwongozo wangu ni kwamba na wewe uende Arusha ukamuulize huyo mama. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho na kwamba kwa leo tunaishia hapa na mimi hapa sina matangazo yoyote na kwa sababu hiyo basi nachukua nafasi hii kulahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.43 usiku Bunge lilahirisha mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 28 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)

